Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Tisa – Tarehe 23 Juni, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA – MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha Uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA WAZIRI MKUU BUNGENI – MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani *Dr*. Wilbrod Slaa napenda kuwasilisha Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 74

**Barabara Kuunganisha vijiji vya Kata za Mwamala na Kikubiji-Kwimba**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, sehemu kubwa ya Kata za Mwamala na Kikubiji Wilayani Kwimba ni eneo la mbuga ambalo wakati wa masika vijiji vya Shilembo, Shigangama, Nghulika, Ngwanghanga na Mwamitenje havifikiki kabisa kutokana na maji na matope; na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kwa muda mrefu imeshindwa kabisa kujenga barabara zinazounganisha vijiji hivyo kutokana na kiasi kidogo cha fedha kinachotengwa kwa Wilaya kwa ajili hiyo ikilinganishwa na gharama kubwa ya ujenzi wa barabara hizo kwenye maeneo ya mbuga;-

(a) Je, Serikali iko tayari kutuma wataalam wakashirikiane na wataalam wa Wilaya ya Kwimba kufanya tathmini ya gharama halisi ya kuunganisha vijiji hivyo kwa barabara hadi barabara ya Mkoa ya Mwamhaya hadi Itongwitale?

(b) Je, baada ya tathmini hiyo kufanyika, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo kulingana na tathmini hiyo?

(c ) Je, Serikali itakuwa tayari kutoa fedha za kuimarisha barabara ndogo ya kutoka Shigangama hadi barabara kuu ya Mwanza – Shinyanga kama mpango wa dharura ili iweze kupitika kwa kipindi chote cha mwaka wakati kazi ya kuviunganisha vijiji vyote vilivyotajwa kwenye barabara ya Mkoa ikiendelea kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a )Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kutuma wataalam ili wakashirikiane na wataalam wa Wilaya ya Kwimba kufanya tathmini ya gharama halisi ya kuunganisha vijiji hivyo hadi barabara ya Mkoa ya Ng’wamhaya hadi Itongoitale.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini, Serikali itaangalia iwapo kuna uwezekano wa kutenga fedha za ujenzi wa barabara hiyo kulingana na Bajeti iliyopo kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba imeomba fedha kiasi cha shilingi milioni 96 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi kwa ajili ya Ilula – Shilembo - Milyungu yenye urefu wa kilomita 28

inayounganisha Kijiji cha Shilembo hadi barabara kuu itokayo Mwanza kwenda Shinyanga.

(c) Mheshimiwa Spika, barabara ndogo kutoka Shiyangama hadi barabara kuu ya Mwanza – Shinyanga yenye urefu wa kilomita 23 iko katika hali ya kutotengenezeka hivyo kuhitaji matengenezo makubwa (ukarabati).

Hata hivyo, iwapo barabara hiyo ni kipaumbele kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, Halmashauri inaweza kuangalia uwezekano wa kuitengea barabara hiyo fedha za matengenezo ya sehemu korofi ili iweze kupitika wakati inasubiri uwezekano wa utekelezaji wa kazi ya kuviunganisha vijiji vyote vilivyotajwa kwenye Barabara ya Mkoa.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa ahadi nyingi sana katika jimbo lake, ahadi ya kutuma wale wataalam vilevile na ombi la Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kuunganisha Ilula na Milyungu. Je, haya maombi haya na ahadi hizi zitatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bujiku Sakila wa Kwimba kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapa barabara hii iko katika mipango na ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge barabara hii inaonekana kwamba ina matatizo, kama nilivyoeleza hapa katika jibu la msingi wao wameweka katika Bajeti yao pesa kwa ajili ya barabara na sisi tunaamini kwamba kama wameweka ni kazi ya Halmashauri ya Kwimba kuhakikisha kwamba barabara hii anayoizungumza na zile nyingine anazozungumza zinapewa kipaumbele ili ziweze kujengwa.

Sasa suala la kwamba itakuwa ni lini, mimi ninataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama wataipa kipaumbele kwa sababu tunakuja hapa leo kuja kuomba bajeti kwa ajili ya mikoa, kwa ajili ya Wilaya zetu kwa maana Halmashauri zikipita basi hii barabara kama wataipa kipaumbele itakuwa ni moja ya maeneo ambayo tutaya-*consider* kwa wakati huo.

Na. 75

**Kuimarisha Barabara Vijijini**

**MHE. MOHAMMED S. SINANI (K.n.y. MHE. SULEIMAN OMAR KUMCHAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu inakaribia kuwa na idadi ya watu 37.5 milioni na asilimia 85 ya Watanzania wanaishi Vijijini ambapo kazi kubwa kwa Watanzania walio wengi ni kilimo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja kubwa ya kuongeza Bajeti ya kutengeneza barabara vijijini ambako ndiko yanatoka mazao mengi?

(b )Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kuanzisha chombo ambacho kitakuwa kinasimamia maendeleo ya vijijini tu kama vile barabara za vijijini, zahanati, shule za vijijini na kadhalika ili kurahisisha Maendeleo ya wananchi wanaoish i vijijini?

(c) Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kuwa na mpango au utaratibu rasmi wa viongozi wa juu kama vile Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu kufanya ziara kwenye vijiji hasa vile vyenye taabu kupitika ili waone hali halisi ya Watanzania wanaoishi huko ili kupata upeo wa kutosha wa kuwasaidia wananchi hao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara za Vijijini kama kiungo muhimu cha kuunganisha usafirishaji wa mazao kutoka Vijijini hadi kwenye maeneo mbalimbali ya masoko. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imekuwa ikiongeza Bajeti ya matengenezo ya barabara zinazohudumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (kwa maana ya Halmashauri) kulingana na uwezo wa Serikali. Serikali kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara ilizitengea Halmashauri zote nchini kiasi cha shilingi bilioni 22.4 mwaka 2006/2007 kwa matengenezo ya barabara zenye jumla ya urefu wa kilometa 13,353. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi 65 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 27,229. Mwaka ujao wa fedha 2008/2009 Serikali inakusudia kuongeza Bajeti ya matengenezo ya barabara kwenye Halmashauri hadi kufikia shilingi bilioni 65.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inao mfumo mzuri wa kusimamia Maendeleo ya Sekta mbalimbali katika maeneo yote ya nchi. Kwa kupitia Sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi, (*Decentralization by Devolution*) utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kisekta na uratibu wa miradi mbalimbali ya Maendeleo hufanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kila Sekta huandaa na kuweka vigezo vya kusimamia Maendeleo ya

Sekta hiyo kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (*Vision 2025*), MKUKUTA na Malengo ya Milenia. Aidha, kwa kushirikiana na Mikoa, Serikali inasimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuhakikisha yaliyokusudiwa. Hivyo basi, bado haijajitokeza haja ya kuanzisha chombo kingine cha kuratibu Maendeleo ya wananchi vijijini.

(c) Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi kuwa Viongozi wetu wa juu Serikalini wamekuwa wakifanya ziara sehemu mbalimbali nchi ili kukagua shughuli za Maendeleo. Nachukua fursa hii kuwashauri Viongozi wa Mikoa na Halmashauri kwamba, pindi Viongozi mbalimbali wanapofanya ziara katika maeneo yao wawapangie ratiba itakayowawezesha kujiongea hatua iliyofikiwa katika sekta mbalimbali huko Vijijini badala ya kuwapangia maeneo ya Mijini tu.

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miradi mingi inayokwenda wilayani na wakandarasi wanaopata zabuni katika miradi hii kama vile barabara na miradi mingine mbalimbali, wanashindwa kuendeleza miradi ile na kujitoa.

Je, Serikali hivi sasa itakuwa iko tayari kutoa *secular* maalum wakandarasi wale wanaoshindwa kutekeleza miradi hiyo wasipewe tena zabuni hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah, kama ifutatavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah anazungumzia kuhusu wakandarasi ambao wanapewa majukumu ya kujenga barabara halafu wanafika mahali wanashindwa kuendelea na shughuli na anaitaka Serikali itoe tamko. Nataka tu niseme kwamba katika Halmashauri zetu kwanza tunayo Kamati inayoshughulikia masuala yote yanayohusu *procurement* kwa maana ya kuweza kupata wale wakandarasi ambao wanahitajika kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni wajibu wa Halmashauri kupitia Kamati ile ambao kwa sasa Mwenyekiti anakuwa mara nyingi ni Mkurugenzi mwenyewe kuhakikisha kwamba wanampata mkandarasi ambaye ni makini katika kutengeneza barabara zao. Ni lazima wahakikishe kwamba wanapata taarifa zote muhimu ili wasije wakafika mahali ukakuta barabara inakwama, mkandarasi amejiondoa na kwa hiyo ukakuta matatizo yanaendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge mimi ninachoweza kusema hapa ni kwamba tutaendelea kuwakumbusha Halmashauri kuhakikisha kwamba wanakuwa makini ili tusipe wakandarasi wanaofanana na hivyo anavyozungumza Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, mtambo ulileta ukorofi kidogo. Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa

kuwa miaka hii miwili iliyopita mvua kubwa zilizonyesha zimevuruga kabisa mifumo ya barabara vijijini na hizi hela Mheshimiwa Waziri anazosema Serikali itatenga hazitatosheleza kutengeneza hizi barabara zote.

Je, Serikali haioni kama kuna umuhimu wa kuongeza Bajeti ya barabara vijijini na vilevile kuomba kutoka kwa *partners* wetu watusaidie ili tuwasaidie wananchi wanaokaa kule vijijini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama nimekosea Iramba Magharibi, Mashariki atanisamehe lakini ninaamini ni ya Mashariki, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mgana Msindai kwamba katika kipindi hiki cha miaka miwili barabara zetu nyingi zimeharibika ni kweli kabisa na ninakubaliana kwamba kwa hali hiyo sasa maana yake ni kwamba tunayo maeneo mengi katika nchi yetu ambayo hayapitiki kwa sababu ya huu uharibifu ambao unazungumzwa hapa. Sasa Mheshimiwa Mgana Msindai anataka kujua kama Serikali itakuwa tayari kuongeza pesa kwa ajili ya jukumu hilo la kuhakikisha kwamba tunarekebisha barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niseme kwamba *issue* sasa ya kuongeza pesa kwa ajili ya hizi barabara ni *issue* ambayo sasa leo ndio tunaizungumza.

Leo Mheshimiwa Waziri Mkuu ataleta hapa sasa maombi ya kuomba pesa kwa ajili ya kutumia kwa ajili ya barabara. Sasa ili majibu haya yaweze kuwa mazuri moja ya majukumu tutakayofanya hapa ni kuhakikisha kwamba hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na hoja anayoleta inapitishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kuhusu suala la wahisani kwa maana yake wale tunawaita wafadhili, mfadhili ni Mungu, mhisani ndiyo tunamwita binadamu. Sisi tutaendelea kufanya hivyo lakini nafikiri sera zetu sasa hivi kama tumeelewa vizuri ni suala zima la kujitegemea.

Katika Bajeti hii tumeomba kwamba tujitegemee zaidi kuliko kwenda wa wahisani ambao hatuna hakika sana na kama hela hizi watazileta. (*Makofi*)

**SPIKA:** Bado unataka kuongeza? Basi amejibu vya kutosha, ahsante sana.

Na. 76

**Mabango ya Biashara**

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kipindi hiki cha ushindani wa biashara Kampuni mbalimbali zinazotangaza biashara zake kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabango makubwa yenye picha na maandishi makubwa:-

(a) Je, ni mamlaka gani inasimamia uwekaji wa mabango hayo na yanadhibitiwa na nani?

(b) Je, ni nini madhara yatokanayo na mabango hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mamlaka zinazosimamia na kudhibiti Uwekaji wa Mabango ya Biashara ni Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Majiji. Uwezo wa kusimamia na kudhibiti Uwekaji wa Mabango unatokana na Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288 (awali Sheria Na.8/1982) kipengele cha 97 cha Jedwali la Sheria hiyo na kwa upande wa Mamlaka za Halmashauri za Wilaya ni sura 287 (awali Sheria Na.7/1982 kipengele cha 97 cha Jedwali la kwanza la Sheria hiyo. Aidha, Mamlaka hizi za Serikali za Mitaa hutunga Sheria Ndogo kwa lengo la kusimamia na kudhibiti Uwekaji wa Mabango kwenye maeneo ya Mamlaka hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, madhara yatokanayo na Mabango hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Spika, mabango yasipohakikiwa vizuri kabla hayajaandikwa yanaweza kusababisha mmomonyoko wa maadili hususan watoto na vijana ambao ni wepesi sana wa kuiga mambo wanayoyaona.

(ii) Mabango yasipopangiliwa vizuri yanaweza kuharibu mandhari na mazingira ya maeneo husika kwa kuwa na msongamano na kuonekana kama uchafu.

(iii) Mabango yasipopangiliwa ipasavyo yanaweza kuzuia alama za barabarani na hivyo kuweza kusababisha ajali kwa vile madereva hawataweza kuziona alama hizo vizuri.

(iv) Wakati mwingine huvuta hisia na kuharibu utulivu na umakini wa madereva wawapo barabarani na hivyo kuweza pia kusababisha ajali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na athari hizo zipo faida za mabango kwa mfano, kuhamasisha na kukumbusha wananchi kuhusu masuala ya kuzuia UKIMWI, kutoa taarifa za biashara kwa kuweka mifano inayovutia na vilevile kutengeneza mandhari ya barabara na mji kwa kuweka picha mbalimbali zenye ujumbe unaofaa.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anakubaliana na mimi kwamba uwekaji wa mabango usiozingatia utaratibu unachangia sana katika uharibifu wa mazingira lakini vilevile unachangia katika kuwaharibia vision watumiaji wa barabara yaani madereva lakini vilevile na kuharibu mandhari ya miji na majiji yetu. Je, sasa Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutoa maelekezo kwa Halmashauri zote za miji na majiji pamoja na miji midogo kurekebisha hali hiyo mara moja? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nitamke kwamba Mheshimiwa Cynthia Ngoye ndiye Mwenyekiti wa *NEMC* katika nchi yetu na kwa hiyo swali analouliza hapa linahusiana na mazingira. Ni swali la msingi sana na mimi kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kukubali kwamba hili jambo ambalo analizungumza hapa ni jambo muhimu ambalo limetiliwa mkazo na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nataka sasa nijibu kwamba yeye anataka nitoe maelekezo kwamba wapeleke, mimi nataka niseme kwa kifupi sana kwa maana yake hili suala la kutoa maelekezo, utaratibu mzima wa kupanga bango hili likae hapa, miti hii ikae hapa, bustani ikae pale uko katika plan unit ambayo ni Halmashauri za Wilaya na Miji kama nilivyoeleza katika majibu haya. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kutoa maelekezo katika Halmashauri zetu na manispaa zetu na majiji kwamba wao ndio wanaotakiwa kuratibu utaratibu mzima wa kuweka mabango katika barabara na wahakikishe wanafanya hivyo kwa kufuata taratibu za mipango miji ambazo zinawekwa katika Halmashauri zao. (*Makofi*)

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sambamba na mabango hayo yapo makampuni ya biashara hususan yale ya simu kama vile *VODACOM, CELTEL, ZANTEL* na *TIGO* wanaopaka mtaa mzima majengo ya Serikali kama lile la Sayansi na Teknolojia au nyumba za *National Housing* mtaa mzima unapakwa rangi nyekundu au rangi za bluu halafu unaandikwa *VODACOM* bila kuhusisha mamlaka husika. Serikali inaona ni vizuri

mtaa mzima unakuwa na bango umepakwa rangi za biashara za kampuni husika, Serikali inasema nini kuhusu hayo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa James Musalika anazungumzia kuhusu makampuni mbalimbali ambayo yanaweka mabango katika maeneo yetu na wakati mwingine wanafika mpaka wanapaka rangi katika nyumba.

Naomba nirudie na niseme jibu lake ni hili lifuatalo, mamlaka ambayo inatoa kibari cha kwamba tangazo liwekwe pale ni Manispaa, ni Halmashauri zetu za Wilaya ndizo zinazofanya hivyo. Kwa hiyo hata kama unaenda kwenye barabara ya *TANROADs*, *TANROADs* atakurudisha kwenye Halmashauri kwanza ukapate kibari kule kinachokuruhusu wewe kwenda kulipaka jengo zima kama linavyopakwa sasa hivi.

Kwa hiyo, katika Maelekezo ambayo tumetoa hapa ni pamoja na kuzielekeza Halmashauri zetu zihakikishe kwamba kabla rangi yeyote haijawekwa hata kama ni nyumba ambayo ni ya mtu binafsi, wao Halmashauri wanatoa kibali hicho kwa kusema kwamba ni sawa au si sawa. (*Makofi*)

**MHE. IBRAHIM M. SANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Duniani kote mabango ya kibiashara huwa yanalipa kodi maalum yanapotangaza biashara zao, na kwa kuwa, Tanzania kuna mabango ya aina mbili ya *electronics* na ya michoro.

Je, mamlaka husika huwa zinapata kiasi gani cha malipo hayo na kwa muda gani ili Serikali ifaidike na biashara hiyo, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Jibu hili linahitaji takwimu, kwa kweli si rahisi kujua mara moja kiasi cha fedha kinachopatikana kwa mabango yote nchini. Kwa hiyo, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Sasa ni zamu ya Wizara ya Nishati na Madini. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula Mkoani Tabora.

Na. 77

**Wawekezaji na Watafiti wa Madini Kuchukua Rasilimali za Wananchi**

**MHE. TATU M. NTIMIZI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali na Wananchi kwa ujumla wamekubali wawekezaji katika sekta ya Madini wawepo kwa nia ya kuinua wananchi na Maendeleo ya watu kwa ujumla:-

(a) Je, wawekezaji au watafiti wa madini katika Jimbo la Igalula katika vijiji Loya na Tura ambao mwaka 2004 walichukua mchanga kwenda kupima mbona hawajatoa majibu yeyote ili wananchi wajue rasilimali yao ikoje?

(b) Je, nini, hatma ya mchanga uliochukuliwa kijijini tura na Kampuni toka nje mwezi Januari mwaka 2008, tena bila kuwajulisha wananchi na viongozi wao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, Mbunge wa Igaulula, lenye sehemu (a) na (b), naomba nitoe maelezo ya utangulizi yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utafutaji madini hufanyika ili kujua aina ya madini yaliyopo kwenye eneo husika pamoja na wingi na ubora wake. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998 na Kanuni za Madini za mwaka 1999, mwenye leseni ya utafuataji madini hulazimika kuwasilisha Wizarani taarifa za kazi alizozifanya kila baada ya miezi mitatu. Taarifa hizi huwa ni siri hadi hapo kampuni itakapokuwa imeliachia eneo la leseni husika kwa kuhofia eneo kuvamiwa au kuingiliwa na watu pindi ikibainika kuwa lina hazina ya madini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Loya na maeneo jirani kampuni ya *Williamson Diamonds* ilifanya utafiti wa almasi kuanzia 1959 hadi 1976 katika utafiti wa almasi uliofanyika nchi nzima.

Katika eneo hilo kuligundulika kuwepo miamba ya *kimberlite*, ambayo hufahamika kujiolojia kuandamana na almasi. Miamba hiyo ni sehemu ya kundi la miamba ya *kimberlite* inayojumuishwa kama Loya *Group of Kimberlite Field*.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa *Kimberlite* katika eneo hilo kulivutia wawekezaji ambapo kampuni za *Azia International, Savannah Exploration Limited* na *Echo Mining Limited* kwa nyakati zilimiliki leseni katika maeneo ya Loya na Tura.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, Mbunge wa Igalula, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utafutaji wa madini katika vijiji vya Loya na Tura uliofanywa na kampuni ya *Savannah Exploration Limited* mwaka 2005 ulijumuisha upimaji wa sumaku ya Dunia kwa kutumia ndege *(High Resolution Airborne magnetic surveys)* ili kubaini maeneo yenye miamba ya *kimberlite*.

Kazi zingine zilizofanyika ni uchukuaji wa mchanga kwenye mito na sampuli za udongo kwenye maeneo yenye miamba ya *kimberlite* pamoja na uchukuaji wa sampuli kutoka kwenye kila eneo la leseni, katika sehemu ambazo miamba ya *kimberlite* imejitokeza juu ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sampuli hizo zimefanyiwa uchambuzi ili kuona kama kuna madini aina ya *ilmenite* na *garnet* ambayo yanaambatana na miamba ya *kimberlite* na almasi *(indicator minerals).* Sampuli kubwa zilizochukuliwa zimefanyiwa uchenjuaji kwenye mtambo wa kampuni ulioko Tabora ili kubaini kama kuna almasi.

Mheshimiwa Spika, taarifa kamili ya matokeo ya shughuli hizo za utafutaji madini zilizofanyika katika vijiji vya Loya na Tura itatolewa Serikalini pindi utafiti utakapo kamilika. Matokeo ya mwisho ya utafiti ndiyo yatakayobainisha kama maeneo hayo yana mashapo ya madini ambayo yanaweza kuchimbwa kwa faida au hapana.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri wananchi na viongozi wa maeneo hayo wanafahamu uwepo wa kampuni hizo kwani mmiliki wa leseni ya utafutaji au uchimbaji madini hujitambulisha katika ofisi za mkoa, Wilaya hadi vijiji kabla ya kuanza shughuli za utafutaji au uchumbaji wa madini.

Vilevile, kampuni za utafutaji madini huajiri wananchi waishio kwenye maeneo ya leseni zao katika kazi mbalimbali za muda.

Hata hivyo, katika hatua ya kazi zinazofanywa na makampuni haya, bado kazi hizi ni za utafiti tu. Kampuni itakapobaini uwepo wa madini ya kutosha kufanya kazi uchambaji wa faida, inaomba leseni ya uchimbaji kulingana na kiwango cha uwekezaji inachokusudiwa.

Kwa maana hiyo hatma ya mchanga uliochukuliwa ni kubaini kwa uhakika ni viwango gani vya madini vinavyotakiwa na maeneo yalipo ili kutoa mwongozo wa uwekezaji unaokusudiwa. *(Makofi)*

**MHE. TATU M NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu aliyojibu.

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba wananchi wa Tura na Loya walijua nini kinafanyika. Wamekuja kuona wawekezaji wameingia katika eneo lile na kuanza kuchimba Serikali ya Kijij haikuwa na habari, wananchi hawakuwa na habari.

Walichukulia wananchi tu kama vibarua, ndipo Viongozi wa Serikali wakaja kunitafuta Mbunge wao kuja kujua ni kitu gani kinafanyika. Baadaye ndiyo Halmashauri ikajua, Mkuu wa Wilaya naye akajua.

Kwa hiyo, si kweli. Kwa nini inafanyika hivyo bila ya kuwashirikisha wananchi kwa usalama wa Wachimbaji na kwa usalama wa wananchi wenyewe?

La pili ni kwamba hamwoni kwamba ni vema Kampuni inapochimba mchanga huu na kupeleka kufanya utafiti baada ya muda kupita ni vizuri Viongozi wao kurudi kwa wananchi kuwaeleza ni kitu gani kinafanyika. Kwa sababu hivi sasa wanabaki na mashimo kwa muda mrefu bila kujua hatma ya machimbo hayo? Hamjui kwamba yanahatarisha mazingira ya eneo lile? Na kama wananchi hawana habari ni kitu gani kinafanyika, hamwoni kwamba mnawaweka katika hali ngumu wananchi hawa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mama yangu Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, mimi nimezungumzia utaratibu unaofanywa wakati wawekezaji wanapokusudia kufanya utafiti wanapokuja Wizarani na wanapewa leseni. Wanatakiwa baada ya hatua ya kupewa leseni taarifa zinakwenda kwa Afisa wetu wa Madini Mkoa na yeye anapeleka taarifa hizo katika ngazi ya uongozi wa Wilaya na ngazi ya ungozi wa Vijiji.

Mheshimiwa Spika, kama jambo hili limetokea na kama jambo hili limetokea la kwamba wananchi hawakujua basi mimi ni lazima nikubali kwamba kuna uzembe ambao umetokea ndani ya Idara yetu ya Madini na hivyo tutaifuatilia na kuangalia ni hatua gani tunachukua. Kusema kweli siyo utaratibu mzuri kwamba katika maeneo ya wananchi mgeni tu aje tu aje aanze kuchimba bila Viongozi wa pale kuwa na taarifa. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tutalifuatilia na nitawasiliana na Mheshimiwa Mbunge nimpe majibu ya uhakika ni nini kilichotokea.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu *sampling*. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, *sampling* inafanywa kubaini kiasi cha madini yaliyopo na maeneo yaliyopo na leseni ile hutolewa kwa muda. Kwa hiyo, ni kipindi kile ambacho tunamruhusu mwekezaji afanye kazi zake ili abaini maeneo yaliyokusidiwa na leseni pindi itakapokwisha kama hakuna maeneo yaliyobainika au kama hataendelea na ile kazi anaturudishia leseni na sisi kama Wizara na Idara ya Madini tunaangalia utaratibu mwingine kwa waombaji wengine wanaokuja na ndiyo maana katika maeneo hayo hayo nimetoa majina ya wawekezaji mbalimbali ambao wamekuja kuomba leseni katika kipindi tofauti kwa eneo hilo hilo.

Kwa hiyo, kuna wengine wamefanya kazi wameshindwa, wengine wamekuja na kadhalika lakini kama tunavyosema ni kweli kwamba atakapomaliza kazi mwekezaji au mtafiti mmoja akishindwa anatupatia taarifa Wizarani na sisi tunapata sababu ya kumpa mtafiti mwingine anayekusudia eneo hilo.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA :** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa wawekezaji hawa watafiti na hawa wawekezaji ambao wapo sasa hivi tatizo la kuchukua mchanga limekuwa ni kero kubwa, na kwa kuwa tatizo hili limekuwa ni kero na linaleta mgogoro mkubwa kwa mchanga huu kuchukuliwa kwenda kufanyiwa utafiti nje. Je, Serikali sasa itaweza kuahidi kujenga *smelter* hapa nchini ili tatizo hili kama kero iondoke? Na lini wataweza kufanya hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nadhani labda niseme tu kwamba tatizo la kuchukua mchanga linapewa tafsiri kidogo tofauti na linaweza likaeleweka tofauti.

Mheshimiwa Spika, lakini lazima tukubali kwamba wakati mwingine maeneo ambayo yanazingatiwa na leseni ni maeneo makubwa sana labda *square kilometre 20 hadi 25* na mtu anapofanya utafiti anakwenda kwa awamu. Kwa hiyo, anakwenda akidokoa hapa na hapa ili kubaini hasa ni eneo gani linakusudiwa kuwekewa au litakalokuwa lina manufaa katika kutumika kufanya huo uwekezaji.

Kwa hiyo, kwanza hiyo kazi yenyewe ya kuchukua mchanga ni kubwa kulingana na ukubwa wa leseni na Madini yanayotafutwa na wakati mwingine Madini yenyewe yanakuwa yana kina kirefu yaani *underground*.

Sasa naomba pia nikubali kwamba kama nilivyosema kwanza katika hii hali hatuna ushahidi wa hawa waliochukua mchanga katika maeneo haya wamekwenda kufanyia utafiti Tabora na baada ya uchenjuaji kufanywa pale wamechukua *concentrate* ile kwenda kuifanyia utafiti Mwanza.

Kama kuna wengine wanapeleka nje ya nchi nadhani ni kwa sababu za *complications* za utaalamu wa kufanya uchenguaji wa Madini yanayokusudiwa. Lakini nadhani nikubali kwamba ni wakati muafaka kwa Serikali au kwa Taasisi za Umma kufanya utafiti na kufanya uwekezaji ili kuwa na *smelter*, kwa sababu *smelter* si kwa ajili ya Madini haya tu smelter pia ni kwa ajili ya dhahabu na Madini mengine. Kwa hiyo, huenda tukipata *smelter* kubwa kiwango cha kuweza kufanya kazi kubwa itakidhi mahitaji ya kufanya uchenjuaji wa Madini mengi tu siyo haya ya Almasi tu.

Kwa hiyo, nadhani ni wazo zuri na tutalifikiria Wizarani namna ya kulitekeleza. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kuongezea kwenye majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali la nyongeza aliloulizwa na Mheshimiwa Mnyaa.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Serikali imekuwa ikiuelezea umma suala la ujenzi wa *smelter* kama yalivyo maeneo mengine ni suala la kisera na mwelekeo wa sera zetu kama inavyojulikana sasa hivi ni ushirikishi wa Serikali pamoja na sekta binafsi.

Kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Mnyaa ameuliza angependa kuona kama Serikali ina *commitment* sasa ya kujenga *smelter* nchini lakini kwa sababu mwelekeo wa Sera zetu ni shirikishi naomba niuarifu umma kupitia Bunge lako Tukufu kwamba tunaendelea kuwakaribisha pia wawekezaji binafsi wanaoweza kujenga *smelter* zao hapa baada ya kufanya *assessment* yote kuona kama ni jambo ambalo lina tija na lina manufaa na faida kubwa ambayo wanaweza kuipata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa sababu tunaamini wawekezaji wapo wa ndani ambao wana uwezo tuwakaribishe sana waweze kushirikiana na Serikali ili tujenge *smelters* hapa nchini kwa ajili ya ku-*save* kile ambacho kinaweza kufanyiwa uchenjuaji nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rwilomba hujamaliza tu? Haya swali la nyongeza!

**MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu niulize nami swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo la migogoro ya madini linatokana na sera na sheria ya madini, sheria ya madini ina mapungufu makubwa sana na imeshatumiwa tume nyingi sana na zimekuwa zikirudia mara nyingi. Sheria ya madini haimtambui *DC* wala mwenyekiti wa Halmashauri wala Viongozi wa Vijiji, inam- *fever* sana mwekezaji na inahitaji kurekebishwa. Tumeomba sana sheria hiyo irekebishwe iletwe hapa.

Mheshimiwa Spika, kuna kiwingu gani na kwa nini sheria hiyo isiletwe sasa hivi ikarekebishwa ili nchi iweze kufaidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rwilomba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, migogoro ya madini ina vyanzo vingi na moja wapo kusema kweli kama alivyosema ni tafsiri ya sheria. Lakini tumeshalizungumza hapa Bungeni mara kadhaa na kwamba taratibu za kupitia sheria ya madini zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba tukubali kwamba kwa sasa hivi kuna tume ya Rais ambayo imepitia mambo mbalimbali ya sekta ya madini ikiwa ni pamoja na Sheria ya madini. Sasa sisi tumeletewa Wizarani tumeipitia na tumeirudisha kwa Mheshimiwa Rais na tunasubiri tupate miongozo ya Sheria hiyo halafu na sisi tutaifanyia kazi baada ya hapo tutaleta mbele ye Bunge lako siyo mabadiliko ya Sheria tu lakini pia huenda

tukahitaji pia kufanya marekebisho katika sera ya madini ambayo yote yatakuja hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuridhiwa kwa niaba ya wananchi. (M*akofi*)

Na. 78

**Kupanda kwa Ada za Uwindaji**

**MHE. JOHN PAUL LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ada za uwindaji zimepanda sana kiasi kwamba wananchi wa kawaida wanashindwa kumudu gharama hizo:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kupanda sana kwa gharama hizo kunachangia watu kukwepa gharama hizo na kujiingiza katika uwindaji haramu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, hatua ya kupandisha ada hizo imechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko kubwa la wanyamapori waharibifu wa mazao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi haramu ya rasilimali ya wanyamapori (ujangili) yamekuwepo kabla na baada ya ada za uwindaji kuongezwa. Suala la kuwepo kwa ujangili linachangiwa na sababu mbalimbali kama vile:-

- Hulka ya baadhi ya watu ya kutaka kujipatia nyamapori na utajiri kutokana na matumizi haramu ya wanyamapori;

- Upungufu wa Chakula nyakati nyingine;

- Imani ya kutumia baadhi ya sehemu za wanyamapori kwa tiba za asili, shughuli za utamaduni na mapambo;

- Uwezo mdogo kwa baadhi ya wananchi kununua nyama ya wanyama wafugwao na kushindwa kukidhi matakwa ya sheria, kwa mfano kuwinda wanyamapori kwa kutumia silaha stahili;

- Elimu ya kutojua thamani ya wanyama na kuwaona kama ni mali isiyo na wenyewe.

Kwa mtazamo huo, ongezeko la ada lina nafasi ndogo katika kuchochea ongezeko la ujangili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo niliyotoa, napenda kufahamisha Bunge lako Tukufu kuwa gharama za usimamizi wa shughuli za uhifadhi wa wanyamapori zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku. Aidha, sambamba na hilo, mwenendo wa kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania pia umekuwa chanzo cha ongezeko la mahitaji na huduma mbalimbali zitolewazo kugharamia uhifadhi. Hivyo ilikuwa muhimu kufanya marekebisho ya ada ili fedha zitakapopatikana ziweze kukidhi mahitaji makubwa ya shughuli za uhifadhi.

(b) Tatizo la ongezeko la uharibu unaotokana na wanyamapori wakali unasababishwa na sababu nyingi zikiwemo za kuboreshwa kwa shughli za uhifadhi pamoja na ongezeko la shughuli za binadamu zinazoingilia maeneo ya wanyama. Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo hilo kwa maisha na mali za wananchi. Kutokana na ukweli huo Serikali imejiwekea utaratibu wa kudhibiti tatizo hilo kwa kushirikisha wananchi na wadau mbalimbali ili kuwaondolea kero wananchi. Hivyo hatua ya kupandisha ada za uwindaji wa wanyamapori haiwezi kuwa sababu ya ongezeko la wanyamapori waharibifu wa maisha na mali.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika**,** pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mojawapo ya sababu alizojitaja Mheshimiwa naibu Waziri za kuwafanya watu wajiingize kwenye uwindaji haramu ni upungufu wa chakula ambao hao husababishwa na wanyama haohao. Je, Serikali italeta lini sera ya kuwafidia wakulima kutokana na uharibifu wa mazao haya?

Tuliambiwa na serikali kwamba wanatarajia kuanzisha *Wildlife management areas* katika kila kijiji ni lini sehemu zetu hizo za Rungwa, Mhesi na Kizigo wataanzisha?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa John Paul Lwanji kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa sasa tumekuwa na utaratibu wa kutoa kifuta machozi nafikiri Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kwamba tumekuwa tukitoa shilingi 100,000/= kwa shamba linalozidi ekari moja kama linakuwa limeharibiwa na wanyamapori na hii tunaiita ni kifuta machozi siyo fidia kwa sababu utaratibu halisi wa kuhifadhi wanyamapori hawa unajumuisha wananchi wenyewe kwa hiyo si jukumu la nani amfidie nani kwa serikali na wananchi kwenye hili tupo pamoja.

Kuhusu utaratibu wa *WMA* Sera na kanuni za kuanzisha *WMA* zimeshaanzishwa na tayari zipo. Mwanzo tulikuwa na maeneo 16 nchini ambayo tuliweka kama *pilot areas* tulishakamilisha hayo na sasa mradi huu unakwend akwenye maeneo yote karibia wilaya zote 42 ambazo zinazunguka wanyamapori.

Changamoto ni uongozi wa wilaya kushirikiana na wananchi wenyewe kwa sababu tumekuwa tukipata matatizo maeneo mengine kwamba baadhi ya wananchi wamekuwa hawapendi au wamekuwa na wasiwasi kuyaachia maeneo hayo ili yatumike kwa ajili ya *WMAs.* Kwa hiyo, maeneo ambayo yapo tayari sisi Wizara tunalihimiza sana jambo hili na tupo tayari kushirikiana nao na tayari tumeshamaliza kwenye maeneo 16 na kama Manyoni wako tayari na sisi tupo tayari kushirikiana nao pia.(*Makofi*)

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, bei za leseni za wenyeji za kuwinda wanyamapori zimepanda sana na maeneo wananchi waliyokuwa wanatumia kuwinda yamechukuliwa na wawindaji wa kitalii. Je, ni lini bei za wanyamapori zitapunguzwakwa wananchi sambamba na maeneo ya wazi waliyokuwa wanayatumia kurudishwa kwa wananchi kwa ajili ya kuyamiliki wao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu *technically* maswali mawili ya Mheshimiwa Said Nkumba kama ifuatavyo:-

Kwanza amezungumzia kwamba bei za wanyama kwa wenyeji zimepanda sana ukiziangalia kiharakaharaka unaweza ukaona kama zimepanda lakini nigependa kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba gharama ambazo tuna-*charge* kuwinda wanyama hawa ni ndogo sana.

Nyati tunatoza shilingi 42,000, nyati mwenye kilo zaidi ya 300. 42,000 maana yake ni chini ya shilingi 800 kwa kilo bei ambayo ndogo sana ukilinganisha na wanyama ambao wanafungwa. Kwa hiyo, bei ninaweza nikasema hazijapanda sana ukilinganisha na bei ya nyama kwenye soko.

Kuhusu maeneo kurudishwa kwa wananchi. Kuna maeneo mengi ambayo tayari yako kwa wananchi na mchakato wa kuyatumia kwa ajili ya *WMAs* unaendelea na kwa maana hiyo hakuna mpango wa kuyaachai maeneo ambayo tayari yako kwenye *reserves* za kisheria au yaliyohifadhiwa kisheria kwa ajili ya wananchi isipokuwa yale maeneo ambayo ni *open areas* na yanajulikana.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kumwuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, kuna wananyamapori wakali ambao wamekuwa wakiingia kwenye maeneo ya makazi ya watu na kudhuru hata kupoteza maisha yao. Watu hao wanapotaka kuwawinda wanyamapori hawa hutozwa ada. Lakini wanyamapori hawa wakali wanapowadhuru binadamu hakuna fidia yoyote inayotolewa. Je, Wizara inasema nini kuhusu hili?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Martha M. Mlata Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza, Sheria ya wanyamapori sura namba 283 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 kifungu namba 53 kinaruhusu Askari wa Wanyamapori kuua wanyama wanaokuwa wamesababisha madhara kwa binadamu na kwa kutumia Kanuni na Sheria hiyo tumekuwa tukisaidiana na wananchi kwanza inapowezekana kuwarudisha wanyama hayo kwenye hifadhi lakini mara nyingine tumekuwa tukiwaua na kwa miaka mitano iliyopita tumeua Tembo 277, Simba 171, Nyani 324 na wanyama wengine wengi na hawa wamekuwa wakiuawa na Askari wa Wanyamapori kwa kushirikiana na wananchi bila tozo lolote.

Kwa maana hiyo hatutozi chochote pale ambapo ni mapambano ya kuokoa maisha na mali za wananchi na hii inafanyika kwa kushirikiana na Askari wa wanyamapori.

Na. 79

**Maeneo Yanayozunguka Mlima Kilimanjaro**
**Kufaidika Kiuchumi**

**MHE. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna uhaba mkubwa wa ardhi Mkoani Kilimanjaro, hali inayochangia kushuka kwa kipato cha wananchi:-

(a) Je, ni kwa nini mipaka ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro imeongezwa hata pasipo maafikiano na Serikali za Vijiji husika wilayani Hai?

(b) Ikiwa Tarafa moja tu ya Ngorongoro hupatiwa Tshs. 1.4 bilioni kwa mwaka kutokana na mapato ya Hifadhi ya Ngorongoro. Je, ni kwa nini Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro hazipatiwi gawio rasmi kutokana na mapato makubwa sana yanayotokana na Mlima huo?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kuweka viwango rasmi ili kusaidia shughuli za maendeleo katika Halmashauri husika katika mwaka wa fedha 2008/2009?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita , Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli eneo la Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro liliongezwa kufuata Mipaka ya Hifadhi ya Misitu ya Asili yaani (*Catchment Forests*). Katika zoezi la kuainisha mipaka kumetokana na kasoro chache na hivi sasa Serikali imeunda Kamati Maalum kushguhulikia kasoro hizo. Kasoro hizo zinategemea kumalizika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 pale ambapo Kamati hiyo tuliyoiunda itakuwa imemaliza kazi yake.

(b) Kuna Mazingira tofauti ya kiutendaji kati ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Mazingira ya kiutendaji yanatofautiana kama ifuatavyo:-

(i) Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro mbali na kutunza wanyamapori, inayoghulikia pia kuendeleza jamii ya Kimasai wanaoishi ndani ya Mamlaka ya Hifadhi na vilevile wale walio jirani na hifadhi hiyo.

(ii) Kwa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro wananchi hawaishi ndani ya Hifadhi. Wananchi wanaishi kuzunguka Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro wanapatiwa misaada ya kimaendeleo kupitia mpango wa Ujirani mwema uanoendeshwa na *TANAPA.*

(iii)Katika kulinganisha mapato yatokanayo na Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, wananchi waishio jirani na Mlima huo wanafaidi mapato makubwa zaidi kuliko wananchi wanaoishi katika Mamlaka ya Hifadhi ya ya Ngorongoro kutokana na ajira za wanaohudumia watalii mliami yaani (*Guide and Porters*), faida itokanayo na biashara ya utalii kama vile mahoteli na kampuni za utalii zilizopo jirani na mlima huo.

Hivyo Mlima Kilimanjaro unatoa fursa ya uchumi mpana zaidi ya wananchi unaokadiriwa kuwa shilingi bilioni 40 kwa mwaka katika biashara ya utalii. Aidha, faida nyingine za Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro kwa wananchi wa Kilimanjaro ni pamoja na hali ya hewa nzuri kutokana na mazingira mazuri ya misitu iliyo ndani ya Hifadhi. Hali hii imewezesha kuwepo kwa uhakika wa mvua kwa ajili ya mazao ya kudumu kama Ndizi na Kahawa na hivyo umaskini kutokuwa mkubwa kama sehemu nyingine za nchi yetu.

(c) Serikali haiko tayari kubadilisha mpango wa sasa wa Ujirani Mwema unaofanywa na *TANAPA* ambayo hutenga 7.5 – 10% ya mapato ya bajeti ya matumizi ya kawaida ya Hifadhi hiyo kusaidia shughuli za maendeleo za jamii inayozunguka hifadhi husika. Katika mwaka 2007/2008 kiasi cha shilingi 406,050,000/= kwa ajili ya jamii inayozunguka mlima huo. Aidha, hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro katika bajeti yake ya mwaka ujao wa fedha yaani 2008/2009 imetenga kiasi cha shilingi milioni 426, na elfu 50,000 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ya ujirani mwema.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake licha ya kwamba hayafurashi.

Mheshimiwa Spika,ningeomba niulize maswali mawili yafuatayo:-

La kwanza, kutokana na uhaba wa ardhi tunaouzungumzia kule Mkoani Kilimanjaro na huo upanuzi wa mipaka uliofanyika. Wale wananchi wanazunguka Mlima Kilimanjaro walipata usumbufu na kutokuweza kulimayale mazao ambayo wamezoea kuyalima kwa nyakati tofauti kuzunguka hilo eneo.

Je, sasa Serikali au Wizara yake Mheshimiwa Waziri itakuwa tayari kuwafidia wale wananchi kwa usumbufu walioupata?

La pili, kabla ya hilo swali la pili ningeomba Mheshimiwa Waziri arekebishe hii sentensi ya kusema kwamba wananchi wanafaidika na haya mapato ya bilioni 40.

Kutokana na jibu inaonekana kama vile hivi bilioni 40 zinakwenda kwa wananchi wa Kilimanjaro sayo sahihi. hizi bilioni au zaidi ya bilioni 40 mapato yanayotokana na mlima Kilimanjaro wanachokifaidi ni kidogo sana.

Swali langu linakuja hivi, kwa sababu kumekuwa na urasimu mkubwa sana kupitia *KINAPA* katika kusaidia shughuli za wananchi ni kwa nini kusiwepo na utaratibu wa kuweka fungu rasmi litakaloelekezwa katika shughuli za maendeleo kwenye hizi Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fuya G. Kimbita Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza amezungumzia upanuzi wa hifadhi na wananchi kutokuwa na naeneo yao ambayo wamekuwa wakiyatumia kulima na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, jibu fupi kuhusu hili kama nilivyosema kwenye jibu letu la msingi kwamba kuna Kamati ambayo tumeiunda Kamati hiyo inazungumzia utaratibu mzima ulivyokuwa na malalamiko mbalimbali ya wananchi kuhusu shughuli yote ilivyofanyika na tumesema tunategemea Kamati hii itamaliza kazi yake.

Mwisho wa mwaka huu nafikiri na nina uhakika kwamba itakuwa imejumuisha maoni ya wananchi na malalamiko yao kuhusu madai yoyote ambayo yanajitokeza au yamejitokeza kutokana na zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili amesema hizi bilioni 40 ambazo zinatokana na uchumi unaotokana na kuwepo kwa mlima Kilimanjaro kwamba hawazipati wananchi wananchi wa Kilimanjaro na kuomba utaratibu wa kuweka fungu rasmi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuomba tu kwanza nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Mlima Kilimanjaro ulipo na hifadhi ile vinatoa fursa, *opportunity* inayotokea inampa nafasi kubwa zaidi yule aliye karibu kwa sababu wale wanakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuweza kuitumia fursa hiyo na ndiyo maana ukienda pale Kilimanjaro wale wanaobeba mizigo ya watalii ukihesabu watu waliotoka Kigoma hawafikia 1%, asilimia karibia 90 wote ni wa palepale.

Ukiangalia ile *spiral effect* ya mzunguko wa fedha zinakuwa Kilimanjaro kwa hiyo naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba fursa hii inawalenga zaidi hawa wananchi wa Kilimanjaro, changamoto ni namna gani wao wanajipanga kutumia fursa hii kuliko kusubiria kidogo ambacho kinakusanywa na *TANAPA* wakati hawa wanaweza kuweka hoteli na kufanya biashara nyingine ambazo zitawapatia mapato makubwa zaidi.

Kuhusu utaratibu wa kuweka fungu maalum, tumesema kwamba tumekuwa tukiweka wastani wa 7 – 10% hilo ndiyo fungu maalum kwa maana hiyo utaratibu huo upo na tumekuwa tukiuboresha mwaka hadi mwaka.

Niliambie tu Bunge lako Tukufu kwamba mwaka 2005/2006 tuliweka wastani wa shilingi milioni 243 lakini mwaka wa fedha uliopita yaani mwaka 2007/2008 tumeweka shilingi milioni 406 kama nilivyosema ambao tumeongeza na tutaendelea kuongeza jinsi mapato ya *TANAPA* yanavyoongezeka.

Na. 80

**Shirikisho la Afrika Mashariki**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kusogeza mbele suala zima la uunganisho wa Shirikisho:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kimkakati/mahsusi wa uhamasishaji wa mipango ya kiuchumi ili muda utakapofika Watanzania tusiwe na kigugumizi?

(b) Je, Serikali inawashauri Watanzania wajiweke kwenye vipaumbele gani ili Shirikisho litakapoanza waweze kuendelea vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha akijibu swali Na. 3 la tarehe 8/4/2008 katika Mkutano wa Kumi na Moja (11) wa Bunge lako Tukufu alielezea jitihada za Serikali zinazoelekeza kuimarisha na kukuza uchumi kupitia Dira yake ya Taifa ya Maendeleo 2025 na nyenzo za utekelezaji wake. Baadhi ya mikakati ya mipango ya kiuchumi ni pamoja na:-

· Kuongeza kasi ya upatikanaji wa elimu kwa wananchi wetu:-

· Kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA);

· Kuimarisha miundombinu ikiwemo mawasiliano, uchukuzi, barabara na nishati ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji;

· Kukuza biashara ya ndani na nje pamoja na kuwavutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi;

· Kuimarisha sekta binafsi ili iweze kushiriki kikamilifu katika uwekezaji, uzalishaji na biashara na hivyo kuinua uchumi;

· Kuimarisha Kituo cha Uwekezaji ili kuweza kufanya uhamasishaji ndani na nje ya nchi;

· Kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za Kikanda kama vile, Jumuiya ya Afrika Mashariki na kadhalika; na

· Kuimarisha ushiriki wetu na uwezo wa kujadiliana na Jumuiya za Uchumi za Kimataifa kama vile Shirika la Biashara Duniano (*WTO*), Benki ya Dunia (*WB*) na Shirika la Fedha Duniani (*IMF*) na kufikia maamuzi yenye maslahi kwa Taifa letu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inawashauri Watanzania kuweka vipaumbele katika maeneo yafuatayo ili Shirikisho litakapoanza tuweze kuendelea vizuri:-

· Kukubali mabadiliko na kujitayarisha kwa kuunga mkono jitihada za Serikali za kukuza uchumi na kupunguza umaskini;

· Kuwa sehemu ya kuimarisha kasi ya Sekta ya Elimu nchini;

· Kuendelea kuimarisha Sekta binafsi na kuvutia uwekezaji kwa Watanzania wenyewe kuwa sehemu ya uwekezaji huo kwa kushiriki kikamilifu katika kuanzisha miradi hasa ya Sekta ya Kilimo, Mifugo, Utalii, Uvuvi, Madini na kadhalika;

· Kubadili mtazamo wa biashara ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje na badala yake tushiriki kikamilifu katika uzalishaji wa ndani hasa katika sekta ya viwanda kwa kuanzisha viwanda vidogovidogo vya kati na vikubwa kwa kuzalisha bidhaa zenye ubora wa viwango pamoja na kuzitumia raslimali zetu za ndani kwa ukamilifu kwa kuuza bidhaa zilizokamilika (*Finished Product*) badala ya kuuza kama malighafi;

· Kuheshimu matumizi bora ya ardhi, kuhifadhi mazingira na kuongeza bidii ya kufanya kazi kwa maarifa na tija; na

· Kuendelea kuimarisha umoja, amani na utulivu uliopo ili Tanzania iendelee kuwa Kisiwa cha amani.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano. Je, itafaidika vipi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, licha ya kufaidika na fursa mbalimbali ambayo inaipata kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia Zanzibar tayari imewasilisha miradi yake mbalimbali kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa kuendeleza Bandari ya Maruhubi ambao utakuwa na thamani ya Dola milioni 400;

(ii) Mradi wa kuendeleza *Airport* ya Zanzibar ambao una thamani ya Dola milioni 78;

(iii) Miradi ya kilimo ambayo ina thamani ya zaidi ya Dola milioni 100;

(iv) Kuna miradi ya kuendeleza uzalishaji wa umeme kwa kutumia upepo ambayo itakuwa na thamani zaidi ya Dola milioni 70; na

(v) Aidha, Kiwanja cha Ndege cha Karume, Pemba tayari kimepata ufadhili kutoka *ADB.* (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, bahati mbaya leo maswali yalikuwa marefu na majibu marefu. Kwa hiyo, maswali yale matatu yaliyosalia tutayapangia siku nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo. Kwanza wageni waliopo leo ni wengi mtaniwia radhi kwa sababu nadhani wamekuja kumsikiliza Mheshimiwa Waziri

Mkuu, Mgeni wa kwanza Mashuhuri ni Mheshimiwa Mama Tunu Pinda, mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Karibu sana. (*Makofi*)

Pia tunaye Mheshimiwa Jaji Joseph Warioba na Mkewe, ahitaji kutambulishwa hapa kwa sababu historia yake na umaarufu wake unajieleza wenyewe. Karibu sana Mheshimiwa Jaji Warioba na Mama Warioba. (*Makofi*)

Nafurahi kuwatambulisha kwenu Waheshimiwa Wabunge, Wabunge wenzetu kutoka Denmark ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Mahesabu ya Fedha za Serikali na Kamati ya Fedha ya Bunge la Denmark. *Our Guests from Denmark will you please stand up to be acknowledged*. Ni hao hapo. (*Makofi*)

Wanaongozwa na Bwana Crowds Akrab lakini pia kuna bwana Jean Peter Sen na Sbain Erick Havnad na wasaidizi wao. *We are very happy to receive you because all of us know the close relations between Denmark and Tanzania staying over a period of more than four decades*. *Thank you very much.* (*Makofi*)

Nafurahi kutambulisha wageni wengine Mzee wetu Peter Kisumo, Waziri wa zamani wa TAMISEMI kwenye awamu ya kwanza, simuoni nadhani labda ametoka. Pia nafurahi kusema miongoni mwa wageni waliopo pale kwenye *Gallery* ni Mwalimu Mwakasege ambaye ni maarufu sana. Karibu sana baba na ahsante sana kwa kazi njema unayoifanya pamoja na wenzio ndugu Kyombo na wote walioko hapo ambao wanakusaidia naomba wasimame. Karibuni sana, mmefanya kazi kubwa na jana nilipata faraja sana kuhudhuria mahubiri yako, kilikuwa ni kitu cha faraja kubwa, ahsante na Mungu akuendeleze katika kazi hiyo. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Peter Msolla, Waziri wa Mawasiliano ni Mzee Lazaro Nyamoga, Thomas Nyamoga, Paul Nyamoga, naona hawapo. Basi pengine wanakuja kesho.

Wageni wa Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri wa Nishati na Madini ni Mama Sharifa Kalala kutoka Washington Marekani, inasemekana huyu ni wifi yake Mheshimiwa Asha-Rose Migiro. Ahsante sana. (*Makofi*)

Kuna Mama sijui ni mama au, Vian Nauru, aha! yule pale ni Bwana, karibu sana, mwalimu wa kujitolea wa Kiingereza. Ahmed Dau na Hassan Dau, wanawe Mheshimiwa, Kelly Mahimbali na Karama Ali. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa James Musalika ni Joseline Musalika ambaye ni mkewe Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Ernest Mabina ni Liberata Mabina, mke wake na Mama Kalwani. (*Makofi*)

Leo nilisikia kwenye kipindi cha redio mtangazaji mmoja akiwasifu Waheshimiwa ambao wanakuja na wake zao au waume zao. Kwa hiyo, nilipenda nizifikishe tu salaam hizo.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Yono Kevela na Mheshimiwa Pindi Chana ambao ni Mchungaji Mlelwa na vijana arobaini wa UKWATA kutoka Njombe. Yule pale na vijana wale. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Aggrey Mwanri ni Mama Grace Mwanri ambaye ni mkewe na watoto wao Erick, Collins, Hollyness na Derick. Karibuni sana leo Mwanri *family* iko hapa, tunashukuru sana kwa wale ambao mnakwenda shule tunawatakia mema na kwa shemeji yetu tunakupongeza unamtunza vizuri Mzee maana yake anajibu vizuri sana maswali. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni mwanawe Goodluck yupo Mzumbe *University*, yule pale anatupungia mkono na mwanawe mwingine yupo form four Ruaha Secondary anaitwa Joel. Karibuni, tunawatakia mema katika masomo yenu. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Sikonge. Naomba wasimame, ahsanteni sana. Wanaongozwa na Mheshimiwa Daniel Khamsin, naomba apunge mkono, wote wamepunga mkono, huyu ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, karibuni sana, tunafurahi sana kuwaona hapa Bungeni, karibuni sana baadaye nitaonana nanyi. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji, ni Wajumbe kumi kutoka Kata ya Sanjaranda, Burungu na Manyoni. Wale pale karibuni sana. (*Makofi*)

Kuna wageni pia wa Mheshimiwa Mohammed Mnyaa, ni Juma Mohammed Juma, Khalifan Yussuf na Ndugu Suleiman Ali Ishaka, wanatoka Kijiji cha Kizungu, Pemba, sijui hili jina sahihi. Nao ni wafanyabiashara na ni wapiga debe mahiri sana kwa Mheshimiwa huyu, hongera sana kwa kuwakumbuka.

Jamani tusiwe tunawasahau wapiga debe kuja hapa kutusalimia, siku zinakaribia karibia. (*Makofi/Kicheko*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa John Momose Cheyo, Daniel Loyal, Mkurugenzi wa Tanzania *Centre for Democracy* (*TCD*), yule pale, karibu sana na Ndugu Isaac Cheyo, Mwenyekiti wa *TCD Technical Committee*, yule pale mtamkumbuka Mheshimiwa Isaac alikuwa humu humu Bungeni, karibu sana. Natumaini kuja kwako hakuashirii mambo ambayo yanaweza kumletea mwenzetu mmoja mambo magumu hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Amenisikia lakini Mheshimiwa Chenge anasema yuko imara tu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge ninayo heshima kuutambua uwepo wa Waheshimiwa Wakuu wote wa Mikoa ishirini na moja ya Tanzania Bara, naomba wasimame pale walipo. Wale pale, karibuni sana. (*Makofi*)

Makofi mengi haya ni ishara ya jinsi tunavyotambua kazi yenu ngumu, kubwa, yenye lawama nyingi lakini mnayoitenda vizuri. Mungu awaendeleze na hekima hizo. Wapo pia Makatibu Tawala wa Mikoa thelathini na moja. Hao hapo, karibuni sana, nanyi pia tunawatakia kazi njema, kazi ya kuendesha utawala ndani ya Mkoa sio kazi ndogo. Mheshimiwa Aggrey Mwanri amenikumbusha kwamba mjomba wake ana Anasaili Maimu sikumtambulisha, Mzee Maimu, ahsante. Kumbe sio mzee, nadhani Mheshimiwa Mwanri una maana mpwao huyu. Yote sawa, karibu sana. (*Makofi*)

Tunao viongozi na wataalam wa ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI wako ishirini na tisa, nadhani na wengine wapo hapo. Karibuni sana. Tunao wanafunzi hamsini na sita pamoja na walimu wao kutoka Kata ya Zanka, nadhani ni kundi lingine tena. Hii shule kubwa sana hili ni kundi la tatu la vijana kutoka shule ya Kata ya Zanka, Wilaya ya Bahi, karibuni vijana msome kwa bidii, Taifa linawategemea sana. (*Makofi*)

Sijui kama nimewaruka wengine, ooh, kuna mtu muhimu sana, leo tuna watu mashuhuri kweli, jamani tunaye Dr. Ferdinand Masau, Muasisi wa Tanzania *Heart Institute*, huyu ni Mzalendo aliyewekeza katika hospitali ambayo inatibu maradhi ya moyo na kufanya *operations* za moyo. Karibu sana Dr. Masau na natumaini Waheshimiwa Wabunge wakija Dar es Salaam watapata fursa ya kutembelea hospitali yako kwa sababu kazi ya upasuaji moyo umeishika pamoja na vikwazo vigumu sana lakini umefika pazuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi mkutane leo mara baada ya hotuba ya Waziri Mkuu Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali ameniomba nitangaze kuwepo kwa kikao cha *PAC* yaani Kamati ya Hesabu za Serikali, saa tano na nusu asubuhi ama mara baada ya kumalizika kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ukumbi Na. 219, ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Ali Ameir, Katibu wa Kamati ya Chama cha Mapinduzi ameniomba nitangaze kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati ya Wabunge wote wa CCM leo saa saba mchana.

Huu ndiyo mwisho wa matangazo, naomba sasa tuendelee na shughuli inayofuata, Katibu endelea na *Order Paper*.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, jambo la dharura, Kanuni ya 47 na 48, asubuhi leo nimewasilisha kwako taarifa ya kutaka kuwasilisha jambo la dharura, nilikuwa naomba idhini yako ili niweze kuliwasilisha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto Kabwe ameniletea leo asubuhi hapa mezani, chini ya Kanuni ya 47 ombi la kuahirisha shughuli nyingine ili Bunge lijadili jambo la dharura.

Jambo hilo linahusu Zimbabwe, sasa nimesoma maudhui ya aliyoandika mwenzetu, ni kweli yana uzito lakini nimetoa maelekezo na naagiza hivi sasa Kamati ya Nje iweze kukaa ili ilione hili jambo.

Kwa maoni yangu ni kwamba tukilijadili kabla halijafika kwenye Kamati linaweza kuharibu zaidi kuliko kutengeneza. Kwa hiyo, naomba Kamati ya Nje iweze kushughulika. (*Makofi*)

Tuendelee, Katibu endelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2007/2008 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2008/2009.

Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Taasisi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge, kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani kubwa aliyonipa kuniteua kuwa Msaidizi wake wa karibu wa kuongoza shughuli za Serikali ya Awamu ya Nne.

Nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge chini ya uongozi wako kwa kuthibitisha uteuzi wangu kwa kura nyingi. (*Makofi*)

Changamoto zilizo mbele yetu ni nyingi, lakini imani yenu kubwa kwangu na ushirikiano mnaoendelea kunipa, unanipa moyo kwamba kwa pamoja tutaweza kukuza Uchumi, kuongeza ufanisi katika utoaji huduma za jamii na hatimaye kuleta maisha bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei 2008, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alifanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri. Katika mabadiliko hayo, Mheshimiwa Rais alimteua Mheshimiwa Celina Kombani kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Waziri wa Sayansi, Mawasiliano na Teknolojia; Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu na Mheshimiwa Stephen Wasira, kuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Aidha, alimteua Mheshimiwa Aggrey Mwanri kuwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje kuwa Naibu Waziri wa Miundombinu na Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga kuwa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana. Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2007/2008, Bunge lako Tukufu lilipata msiba wa Marehemu Salome Mbatia aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Marehemu Benedict Losurutia aliyekuwa Mbunge wa Kiteto. Nichukue fursa hii kuwapa pole Ndugu, jamaa na marafiki wa familia za Marehemu hawa. Mwenyezi Mungu azilaze Roho za Marehemu Mahali Pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kisichopungua siku tano Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakijadili Taarifa kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2007 na Bajeti na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2008/2009 na hatimaye kuipitisha. Napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba yake nzuri na jinsi alivyoweza kutoa maelezo ya ufasaha kuhusu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Vilevile, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri na michango yenu mizuri mliyoitoa wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Serikali. Ninawahakikishia kwamba michango hiyo itazingatiwa wakati wa utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa kupitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge. Nazishukuru Kamati za Kudumu za Bunge lako Tukufu kwa michango na ushauri waliotoa wakati wa kupitia Makadirio ya Matumizi ya kila Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea na Taasisi zilizo chini ya Wizara zote.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali mliyoipitisha ndiyo itakayotuwezesha kuendesha kazi za Serikali na kutekeleza kikamilifu Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha

Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005. Bajeti hiyo imezingatia utekelezaji wa Malengo ya Dira ya Maendeleo 2025, Malengo ya Milenia 2015 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Serikali itaendelea kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato kwa kutekeleza miradi na mipango mbalimbali ya Maendeleo yenye lengo la kuboresha maisha ya kila Mtanzania. Wizara, Mikoa, Halmashauri na Taasisi za Serikali zimetengewa fedha kulingana na majukumu waliyo nayo ambayo yanalenga kutekeleza MKUKUTA.

Viongozi na Watendaji wote wa Serikali wanao wajibu wa kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mara kwa mara wa kazi zilizopangwa na kutoa taarifa za utekelezaji kwa mamlaka husika. Ufuatiliaji huo, ukishirikisha wananchi, utaongeza uadilifu na uwajibikaji wa watendaji katika utekelezaji wa mipango yetu ya Maendeleo. Natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuwa mstari wa mbele katika kuwaelimisha wananchi kuhusu Bajeti hii na miradi itakayotekelezwa katika maeneo yao.

Mwandishi mmoja Glenn Bland aliandika**:** *"Goals and plans take the worry out of living."* Kama tukiweka malengo, hatua tunazozichukua zitazingatia maisha tunayoyahitaji badala ya kutegemea kila tunapoamka asubuhi tunajisikiaje. Tumepanga, tumekadiria na tunategemea kutumia. Mipango yetu itafanikiwa kama tutatumia fedha zilizotengwa kwa ajili ya kile kilichopangwa.

Mheshimiwa Spika**,** Nchi nyingi Duniani zimekuwa na mafanikio ya uchumi imara kutokana na kujiwekea misingi bora ya hali ya siasa, amani na utulivu.

Aidha, uchumi imara ni matokeo ya juhudi wanazowekeza wananchi katika uzalishaji mali kwenye nchi inayozingatia Utawala wa Sheria na yenye Sera nzuri za Uwekezaji. Ninayo furaha kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, nchi yetu ni miongoni mwa nchi chache duniani ambazo zimepata sifa kubwa katika kudumisha amani na utulivu licha ya tofauti za kiitikadi zilizopo. (*Makofi*)

Napenda kuwapongeza wananchi wote kwa kushiriki katika kudumisha amani na utulivu nchini. Nawahimiza kuzidi kuendelea kuwa mfano wa kuigwa katika Bara letu la Afrika na duniani kote. Nawasihi tusiichezee sifa hii, kwani tukiipoteza madhara yake ni makubwa na siyo rahisi kuirejesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua za kutatua masuala ya Muungano yanayoleta kero kwa wananchi wetu wa pande zote kwa kufanya vikao mbalimbali. Kikao kimojawapo cha ngazi ya juu ni kile kilichoongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kilichofanyika tarehe 15 Mei, 2008, Dar es Salaam.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na baadhi ya Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kikao hicho kilijadili Taarifa za Utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika Vikao viwili vya awali kati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi.

Baadhi ya masuala yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na kufungua Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora huko Unguja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuainisha miradi itakayoombewa ufadhili chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mbali na Kikao cha Makamu wa Rais, vilifanyika pia Vikao vingine 11 vya ushirikiano baina ya Wizara mbalimbali za Tanzania Bara na Zanzibar. Wizara zilizohusika na Vikao hivyo ni pamoja na Mawasiliano, Uchukuzi na Miundombinu; Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Maliasili na Utalii; Viwanda, Biashara na Masoko; Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Sheria, Katiba na Utawala Bora; Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Katika Vikao hivyo, masuala mbalimbali yanayohusu Sekta husika yalijadiliwa kwa maelewano na kufikia muafaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pia zimeridhia uteuzi wa Mshauri Mwelekezi atakayeshauri kuhusu mgawanyo wa mapato yatokanayo na rasilimali ya mafuta.

Kazi hii inatarajiwa kukamilishwa mwezi Agosti, 2008 na kuwasilishwa katika Serikali zote mbili mwezi Septemba, 2008. Vile vile, uandaaji wa Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu utakamilika mwezi Septemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaendelea kutekeleza masuala yafuatayo:-

(a) Kuratibu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano katika Vikao mbalimbali vikiwemo vya Kimataifa;

(b) Kuratibu, kuandaa na kushiriki katika Vikao vya Makamu wa Rais na Mawaziri wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

(c) Kufanya utafiti wa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa lengo la kudumisha Muungano;

(d) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano;

(e) Kuainisha maeneo ya uchumi katika Nchi yetu ambayo yakitekelezwa yataleta faida kwa pande zote mbili; na

(f) Kuratibu mgawanyo wa mapato ya pande zote mbili za Muungano.

Ili kufuatilia utekelezaji wa makubaliano hayo kwa karibu zaidi, Vikao vya pamoja vitafanyika kila baada ya miezi miwili chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Nchi yetu ilifanya Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Kiteto na Chaguzi Ndogo za Madiwani katika Kata 16 Nchini. Katika Uchaguzi Mdogo wa Ubunge Jimbo la Kiteto, Vyama Vinne vya Siasa vilishiriki. Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, alichaguliwa kuwa Mbunge kupitia Chama cha Mapinduzi kwa kupata kura 21,506, sawa na asilimia 61 ya kura zote zilizopigwa ; CHADEMA kilipata kura 12,561 ; SAU kura 300 ; na PPT Maendeleo kura 110.

Kwa mara nyingine, nampongeza Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro aliyeshinda uchaguzi huo. Uchaguzi huo, pamoja na Chaguzi Ndogo mbalimbali za Madiwani, zilifanyika katika mazingira yaliyokuwa huru, amani na yaliyozingatia Misingi Bora ya Demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Agosti, 2007 Mheshimiwa Dr. Christine Gabriel Ishengoma (CCM), aliteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum, kujaza nafasi wazi ya Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia. Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Pangalile Rwakatare (CCM), aliteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum kuanzia tarehe 26 Novemba, 2007 kujaza nafasi ya Marehemu Salome Joseph Mbatia. Aidha, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alimteua Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir kuwa Mbunge wa Viti Maalum, kuanzia tarehe 8 Aprili, 2008. Wote nawapongeza sana kwa kuteuliwa kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanza Awamu ya Kwanza ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kwa kuwaingiza wale waliotimiza sifa za kujiandikisha na kuwaondoa waliopoteza sifa. Hadi sasa, uboreshaji wa Daftari hilo umefanyika katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Mwanza na Kagera. Zoezi hili litaendelea kwa Mikoa ya Mara, Shinyanga, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam na Zanzibar. Awamu ya Pili ya Uboreshaji wa Daftari hilo, itafanyika mwaka 2009/2010, kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Lengo ni kuhakikisha kwamba, kila Mwananchi aliye na sifa za kujiandikisha kuwa Mpiga Kura, anapatiwa nafasi hiyo ili aweze kushiriki katika Uchaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali ilianza kutoa ruzuku kwa Vyama vya Siasa vyenye Madiwani. Vyama vinavyopata ruzuku hiyo ni CCM, TLP, CHADEMA, CUF, UDP na PPT-MAENDELEO. Kiasi cha Shilingi bilioni tatu kilitengwa na Serikali kwa ajili ya ruzuku hiyo. Vilevile, Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa, zilianza kutumika rasmi kupitia Tangazo la Serikali Na. 215 la tarehe 12

Oktoba, 2007. Wadau wote wamefahamishwa na kupatiwa nakala ya Kanuni hizo. Nachukua nafasi hii, kuvishauri Vyama vya Siasa visome kwa makini, viheshimu na kuzifuata Kanuni hizo, ili kuepuka migongano inayotokea kati ya Vyama vyetu. Vilevile, Serikali inafanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992, kwa lengo la kuondoa migongano, migogoro na mahusiano mabaya ndani ya Vyama vya Siasa. Marekebisho hayo, yatawasilishwa hapa Bungeni katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Tatu, mwezi Novemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, usajili wa muda wa Vyama viwili ulifutwa, baada ya kupoteza sifa za usajili wa muda na kushindwa kutimiza masharti ya maombi ya usajili wa kudumu. Vyama hivyo ni *Tanzania Peoples Organisation for Democracy and Development (TAPODD),* ambacho kilifutwa tarehe 31 Julai, 2007 na *National Progressive Democratic Party (NPDP),* kilichofutwa tarehe 16 Aprili, 2008. Vilevile, Serikali ilitoa elimu ya uraia kuhusu faida na majukumu ya kila Taasisi na Mwananchi katika mfumo wa Demokrasia kwa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Bunge lako Tukufu, limeendelea kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba ya kutunga Sheria na kuishauri Serikali. Mabadiliko ya Kanuni za Bunge yalifanyika, ambapo Kamati za Kudumu za Bunge zilizopo sasa zinawawezesha Waheshimiwa Wabunge kuchambua kikamilifu masuala mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa na kusimamia shughuli za utendaji wa Serikali kwa umakini zaidi. Vilevile, Bunge lako Tukufu lilipitisha Miswada ya Sheria 24, liliridhia Maazimio 14 yanayohusu masuala mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa na maswali ya msingi 970 yaliulizwa na kupatiwa majibu. Vilevile, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Waheshimiwa Wabunge, walipata fursa ya kumuuliza Waziri Mkuu Maswali ya Papo kwa Papo Bungeni. Katika mwaka 2008/2009, Ofisi ya Bunge itaendelea kusimamia mipango ya mafunzo kwa Watendaji, kuendeleza mahusiano na Mabunge ya Nchi nyingine na kuboresha huduma mbalimbali za kiutawala na elimu kwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali ilitenga Shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Wabunge. Jumla ya Majimbo 40, yakiwemo 32 ya Tanzania Bara na 8 ya Tanzania Visiwani, yaliteuliwa kupata fedha za ujenzi wa Ofisi hizo katika Awamu ya Kwanza. Hata hivyo, kutokana na ongezeko la gharama, mchanganuo wa kitaalam unaonyesha kuwa, gharama halisi za ujenzi wa Ofisi moja iliongezeka kutoka Shilingi milioni 25 zilizokuwa zimekadiriwa awali hadi shilingi milioni 40.

Katika mwaka 2008/2009, Serikali imetenga Shilingi bilioni moja ili kukamilisha ujenzi wa Ofisi 40 katika Awamu ya Kwanza na kuanza ofisi 10 za Awamu ya Pili. Suala hili litasimamiwa kikamilifu na Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Kiongozi ili kuona lengo hilo linafikiwa.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa hali ya uchumi wetu kwa ujumla unaridhisha. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, katika mwaka 2007 uchumi wetu ulikua kwa asilimia 7.1, licha ya kuwepo kwa misukosuko

mbalimbali ya kiuchumi. Mfumko wa Bei, ambao ulifikia asilimia 9 mwezi Machi, 2008, umeendelea kuwa juu kufuatia kupanda kwa bei ya nafaka, mafuta ya petroli, pamoja na bidhaa nyingine kutoka nje. Wataalam wa uchumi Duniani wanaeleza kuwa, matarajio ya mwenendo wa bei za bidhaa katika Soko la Dunia hususan bei za nishati na nafaka, kwa mwaka ujao zitaendelea kupanda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaweka mazingira mazuri yatakayowezesha Sekta zote kukua kwa kasi inayoridhisha ili kufikia lengo tulilojiwekea la ukuaji halisi wa Pato la Taifa la asilimia 7.8. Changamoto iliyo mbele yetu ni kuhakikisha kuwa, Ukuaji wa Uchumi ni endelevu na wa viwango vikubwa kati ya asilimia 8 hadi 10. Viwango hivyo, ndivyo vitakavyoboresha na kuendeleza huduma za jamii na kiuchumi na hatimaye kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa. Hivyo, sote tuongeze matumizi bora ya rasilimali zilizopo na jitihada zaidi zielekezwe kuongeza tija katika Sekta za Kilimo, Miundombinu, Madini na Huduma za Kijamii. Vilevile, juhudi zielekezwe katika utoaji wa mikopo midogo ili kujenga na kuendeleza ujasiriamali kwa mtu mmoja mmoja au vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali na utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2006/2007, Serikali ilianza kutekeleza Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, kwa lengo la kuwashirikisha Wananchi wengi zaidi katika Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini. Serikali ilitenga Shilingi bilioni 10.5 kwa ajili ya Awamu ya Kwanza ya Mpango huo, ambapo Benki za CRDB na NMB ziliteuliwa kushiriki katika utekelezaji na ziliafiki kutoa mkopo mara tatu ya kiwango cha dhamana kilichokubalika kwa kutumia mitaji yao wenyewe. Katika Awamu ya Kwanza ya Mpango huo, Benki hizo ziliweza kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 32.7 kwa wajasiriamali 44,256.

Kutokana na mafanikio hayo, Awamu ya Pili ya utoaji mikopo kwa wajasiriamali ilizinduliwa mwezi Desemba 2007. Jumla ya Asasi za Kifedha 14 zilijitokeza kushiriki kwenye Mpango huo ili kukopesha shilingi bilioni 10.5 zilizotengwa katika Awamu ya Pili. Hadi sasa jumla ya shilingi bilioni 3.7 zimetolewa kwa Asasi hizo za fedha. Kati ya hizo, shilingi milioni 881.3 zimekopeshwa kwenye Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) mbalimbali Nchini. Vilevile Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ilipatiwa shilingi milioni 600 kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi Wananchi wa Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, umeonyesha mafanikio na changamoto kadhaa. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na kuwepo na ongezeko kubwa la mwamko wa wananchi kutumia Huduma za Kibenki na ari kubwa miongoni mwao kuhusu faida za kujiunga na *SACCOS*. Hii imetokana na jitihada za uhamasishaji kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge na Viongozi mbalimbali wa Kitaifa, Mikoa, Wilaya na Vijiji. Vilevile, Mpango huo umehamasisha na kuendeleza dhana ya wananchi kujiajiri kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo inayobuniwa na mtu mmoja mmoja au Vikundi. Kutokana na uhamasishaji huo, miradi mingi mipya ya kiuchumi imeanzishwa na ile iliyokuwa inalegalega imefufuliwa hivyo kuongeza ajira na kipato kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na wananchi wengi kujitokeza kuomba mikopo, ikilinganishwa na kiasi kidogo cha fedha kilichotengwa. Changamoto nyingine ni wananchi wengi kutokuwa na elimu ya ujasiriamali, inayowawezesha kubuni na kuandaa miradi mizuri inayokopesheka, kuiendesha kwa ufanisi pamoja na kupanga matumizi bora ya mikopo waliyokopeshwa na urejeshaji wake. Aidha, katika Awamu ya Kwanza, ipo Mikoa ambayo ilipata mgao wa fedha za mikopo chini ya kiwango cha shilingi milioni 500. Pia, zipo Wilaya 21 ambazo hazikupata kabisa mikopo katika Awamu ya Kwanza kutokana na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa Matawi ya Benki za CRDB na NMB. Hata hivyo, baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika Awamu ya Kwanza, zimetafutiwa ufumbuzi wakati wa utekelezaji wa Awamu ya Pili. Eneo muhimu lililoshughulikiwa ni lile la kuhakikisha kuwa Mikoa, Wilaya na maeneo ambayo hayakunufaika na Mpango huu katika Awamu ya Kwanza, yanapewa kipaumbele. Katika mwaka 2008/2009, Serikali itaboresha zaidi utekelezaji wa Mpango huu ili uwe na tija kubwa. Napenda kutumia fursa hii, kuwahimiza wananchi kote Nchini, kuendelea kujiunga na *SACCOS* ili waweze kunufaika na Mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada za kutangaza vivutio vyetu zimewezesha kuongezeka kwa miradi inayowekezwa na wawekezaji mbalimbali hapa Nchini. Katika mwaka 2007/2008, Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)*, kilisajili jumla ya miradi 902 yenye thamani ya shilingi bilioni 8.1, ambayo imetoa ajira zipatazo 127,588. Kati ya miradi hiyo, miradi 483 ni ya Watanzania, 196 ni ya wageni na 223 ni ya ubia. Takwimu za Kimkoa zinaonyesha kwamba, Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kusajili miradi 502, Arusha miradi 158, Mwanza 51, Kilimanjaro 32 na Pwani 31.

Mikoa mingine ni Shinyanga 17, Morogoro 16, Mbeya 15, Tanga 14, Iringa 13, Kagera 12, Dodoma 11, Mara 9, Lindi 6, Mtwara 4, Tabora 4, Singida 2, Manyara 3, Rukwa 3, Ruvuma 1 na Kigoma 1. Sekta ya Utalii ndiyo iliyoongoza kupata miradi mingi kwa kusajili miradi 275, ikifuatiwa na Sekta ya Viwanda yenye miradi 236 na Sekta za Nyumba na Biashara ina miradi 125.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, kitaendelea kuitangaza Nchi yetu kwa kutumia mitandao ya Kimataifa; kuwaunganisha wawekezaji wadogo na wakubwa wenye Viwanda Vikubwa hapa Nchini ili waweze kushirikiana kibiashara na kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo ili waweze kukuza biashara zao. Natoa wito kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wa Tanzania, kutumia huduma zinazotolewa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania ili waweze kujiendeleza kibiashara. Kituo hiki hakipo kwa ajili ya kuvutia wawekezaji wa nje tu, bali ni kwa ajili ya kuvutia wawekezaji wote wenye nia ya kuwekeza mitaji yao hapa Nchini. Vilevile Mikoa itangaze vivutio na fursa za uwekezaji zilizopo katika Mikoa hiyo, kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo Tovuti na Mikutano ya wafanyabiashara popote pale itakapofanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi ili kuiwezesha kutoa mchango mkubwa zaidi katika Uchumi. Ili kupunguza vikwazo ambavyo Sekta Binafsi inakumbana navyo, kama vile ukosefu wa fedha za kutosha za

uwekezaji, kutokuwa na taarifa sahihi za masoko ya bidhaa za nje na teknolojia duni, Serikali imetoa udhamini wa Mkopo wa Dola za Marekani milioni 16 kutoka Benki ya Dunia kwa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania. Kati ya fedha hizo, Dola za Marekani milioni 6 zitatumika kuwakopesha wafanyabiashara wadogo na wa kati. Chini ya Mpango huo, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania, itatoa asilimia 50 ya mtaji wa biashara inayokusudiwa kuendeshwa na wafanyabiashara watachangia asilimia 50 iliyobakia.

Sehemu nyingine ya fedha hizo, kiasi cha Dola za Marekani milioni 10, kitatumika kuviongezea uwezo Vyuo na Taasisi zinazotoa mafunzo ya ufundi ili viweze kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuandaa mipango ya biashara inayouzika. Natoa wito kwa wafanyabiashara, kuchangamkia mikopo hii ili iwasaidie kukabiliana na vikwazo vinavyowazuia kufanya shughuli zao kwa ufanisi. Vilevile, Taasisi na Vyuo vya Ufundi vitakavyonufaika na mpango huu, vihakikishe kwamba, mafunzo yatakayotolewa yatawasaidia wajasiriamali kukabiliana na ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Biashara ni chombo kinachounganisha Sekta Binafsi na Sekta ya Umma kwa madhumuni ya kukuza uchumi wa Tanzania. Katika mwaka 2007/2008, Baraza litaendelea kuimarisha majadiliano kati ya Serikali na Sekta Binafsi ili iwe mhimili mkuu wa uchumi. Majadiliano hayo yalilenga kuboresha mazingira ya kuendesha biashara na uwekezaji. Aidha, jumla ya Mabaraza ya Biashara ya Mikoa 21 yameundwa Tanzania Bara na jitihada za kuanzisha Mabaraza ya Biashara ya Wilaya zimeanza. Madhumuni ya Mabaraza haya ni kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji na kuibua fursa za uwezeshaji kiuchumi katika ngazi za chini.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Baraza la Taifa la Biashara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, liliandaa midahalo mbalimbali ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi nchi nzima. Madhumuni ya Midahalo hiyo ilikuwa ni kuainisha maoni na uelewa wa dhana nzima ya uwekezaji toka kwa wananchi na jinsi wanavyoweza kuibua miradi ya kuwaongezea kipato na hivyo kuwa na maisha bora. Midahalo ilifanyika katika ngazi ya Wilaya na Mikoa na hatimaye mdahalo wa Kitaifa utafanyika mara baada ya majadiliano ya Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Matokeo ya mdahalo huo, yatafikishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara kwa madhumuni ya kupanga utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Baraza la Taifa la Biashara, litafanya mkutano wake wa tano utakaohusisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kubadilishana mawazo na uzoefu wa jinsi ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji Nchini. Vilevile, Baraza litasimamia na kuimarisha shughuli za Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya, pamoja na shughuli za Vikundi Kazi Vikuu, vilivyoanzishwa na Baraza vya kuboresha Kilimo, Kukuza Viwanda na Mauzo ya Nje, Ardhi, Utalii, Rasilimali Watu, Huduma za Fedha, Miundombinu na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali kupitia Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilito, imewezesha kuundwa na kuimarishwa kwa Vikundi vya Wazalishaji, Wafanyabiashara na Wasindikaji wadogo

vipatavyo 232 katika Wilaya tisa za Chunya, Ileje, Kyela, Makete, Njombe, Korogwe, Simanjiro, Mwanga na Moshi Vijijini. Vikundi hivyo vimejengewa uwezo kwa njia ya mafunzo ya mbinu mbalimbali za kutafuta masoko na kuviunganisha na masoko ya mazao yao. Aidha, vikundi 1,076 vimepatiwa mafunzo ya ujasiriamali, uongozi, biashara, uchaguzi wa mazao ya biashara, utafiti shirikishi wa masoko, ukokotoaji wa gharama na masuala mtambuka, yakiwemo ya jinsia, UKIMWI na mazingira.

Mheshimiwa Spika, ili kusaidia jitihada za Serikali za kuimarisha upatikanaji wa mikopo kwa wakulima, programu imehamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani. Chini ya Mfumo huu, wakulima huhifadhi mazao ghalani na kupewa stakabadhi ambazo wanaweza kuzitumia kama dhamana kwa mikopo watakayoiomba Benki na kurejesha mkopo huo baada ya kuuza mazao yao wakati bei ikiwa nzuri. Utekelezaji wa mfumo huo, umefanyika katika maghala manane katika Wilaya za Hanang (2), Mbarali (2), Songea, Mbozi, Mufindi na Sumbawanga Vijijini. Wakulima 879 wamepatiwa mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 1.2 kwa kutumia Mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Programu hii, imekarabati barabara za vijijini zenye urefu wa Kilomita 670 ili kuboresha miundombinu inayohusiana na masoko ya mazao ya kilimo na kurahisisha muingiliano baina ya wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara vijijini. Vilevile, jumla ya masoko 14 yamejengwa na yamekamilika. Masoko hayo ni Kikatiti (Arumeru), Kwa Sadala (Hai), Inyala (Mbeya), Gallapo (Babati), Katesh (Hanang), Monduli (Monduli) na Matai (Sumbawanga Vijijini). Masoko mengine yaliyokamilika ni ya Tarakea (Rombo), Kiwira (Rungwe), Soni (Lushoto), Tunduma (Mbozi), Makita (Mbinga), Mlangali (Ludewa) na Mtindiro (Muheza). Masoko ya Hedaru (Same), Kinyanambo (Mufindi) na Dongobesh (Mbulu), yapo katika hatua za mwisho za kukamilishwa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaendelea kuimarisha vikundi vya wazalishaji, wafanyabiashara na wasindikaji wadogo. Aidha, itaanza utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani kwenye maeneo ambayo yameonyesha kuwa na uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula kama vile Kirando (Nkasi), Ipinda (Kyela), Majimoto (Mpanda), Mpitimbi (Songea Vijijini), Monduli (Monduli) na Bashay (Mbulu). Vilevile, jumla ya Kilomita 323.6 za barabara zitakarabatiwa na masoko 7 yatajengwa katika Wilaya za Chunya, Ileje, Kyela, Makete, Njombe, Korogwe na Simanjiro.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali chini ya Programu ya Huduma za Kifedha Vijijini, imefanikiwa kuleta mabadiliko makubwa ya kipato kwa wananchi wanaoishi Vijijini. Kwa kutumia mbinu shirikishi na mafunzo kwa wanachama wa *SACCOS*, kumekuwepo na ongezeko kubwa la Wanachama, Hisa, Amana na Akiba. Vilevile, ushiriki wa wanawake umeongezeka, ikiwa ni pamoja na kushika nyadhifa mbalimbali katika Asasi hizo. Programu pia imeimarisha Benki za Wananchi za Mwanga, Mufindi na Mbinga na Benki ya Ushirika Kilimanjaro, kwa kuzipatia magari, kutoa mafunzo kwa watumishi na kuimarisha usimamizi wa mifumo ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, programu ilitoa mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Mikopo na Maafisa wa Mikopo 1,100 wa *SACCOS* 276. Mafunzo hayo yaliwawezesha kuelewa masuala ya Dhana, Kanuni, Misingi na Taratibu za kutoa mikopo, pamoja na kusimamia na kuhakikisha mikopo inarejeshwa. Vilevile, vikao vya pamoja kati ya Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya za Mikoa ya Mbeya, Iringa, Songea, Dodoma, Singida na Kilimanjaro, viliitishwa kuzungumzia jinsi Wilaya zitakavyochukua hatamu za utekelezaji wa shughuli za kukuza na kuendeleza Asasi za Fedha Vijijini, baada ya Programu kumaliza muda wake. Vilevile, Wahasibu 276 pamoja na viongozi 100, walipewa mafunzo ya *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Programu itaboresha usimamizi na utendaji wa Asasi Ndogo za Kifedha, kuimarisha mifumo ya kifedha Vijijini na kuwajengea uwezo wananchi wa vijijini ili waweze kujiunga na kushiriki katika shughuli za *SACCOS*. Vilevile, Programu itaendelea kuimarisha Benki za Wananchi na kusaidia mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Wananchi Njombe.

Mheshimiwa Spika, Programu hizi zimekuwa zikisaidia juhudi za Serikali za kuondoa umaskini kwa kuwawezesha wananchi wa vijijini kuongeza kipato kwa kupata huduma za mikopo kupitia Asasi za Kifedha na masoko ya uhakika ya mazao yao. Kutokana na utekelezaji wa Programu hizi mbili, uzoefu uliopatikana umebaini kuwepo kwa mafanikio makubwa katika Wilaya ambazo Programu hizi zinatekelezwa. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na ongezeko la Asasi za Kifedha, wanachama na mitaji. Aidha, kwa kuimarisha Benki za Wananchi, *SACCOS* nyingi zimeweza kupata mikopo kutoka katika Benki hizo, ambayo imewekezwa katika miradi mbalimbali ya uzalishaji. Eneo lingine lililoonyesha mafanikio ni lile la kuanzishwa kwa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani.

Kupitia mfumo huu, wananchi wengi wameweza kupata mikopo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Changamoto kubwa zilizo mbele yetu ni kueneza uzoefu huo tulioupata katika Wilaya zote nchini. Nazisihi Halmashauri za Wilaya, hususan zile za jirani, kutembelea Halmashauri ambazo zinatekeleza programu hizo kwa lengo la kuona na kujifunza mafanikio yaliyopatikana na baadaye kuyatekeleza katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote ile, hutegemea sana mtandao mzuri wa barabara. Barabara husaidia shughuli za kiuchumi na kijamii kustawi, kushamiri na kuchangia katika ukuaji wa uchumi na mapato ya watu. Katika mwaka 2007/2008, Serikali ilikamilisha ujenzi wa barabara za Isuna - Singida (Km. 63), Singida - Shelui (Km. 110), Geita - Buzirayombo (Km. 100), Kyamiorwa - Buzirayombo (Km. 120), Nangurukuru - Mbwemkuru (Km. 95), Mbwemkuru - Mingoyo (Km. 95), Mkuranga - Kibiti (Km. 79) na Tarakea - Rongai - Kamwanga (Km. 32). Jumla ya Kilomita 330.4 zilifanyiwa matengenezo ya muda maalum na kilomita 79.0 zilifanyiwa matengenezo katika sehemu korofi. Vilevile, jumla ya madaraja na makalvati yapatayo 492 yamefanyiwa matengenezo ya kawaida katika Barabara Kuu na Barabara za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaendelea na ujenzi wa Barabara Kuu. Baadhi ya Barabara hizo ni Manyoni - Isuna (Km. 54), Mbeya - Lwanjilo (Km. 36), Nelson Mandela (Km. 15.6), Kurasini – Mbagala (Km. 11.6) Masasi - Mangaka (Km. 54), Usagara – Sengerema - Geita (Km. 90) na Mwandiga – Manyovu (Km. 60). Vilevile, kupitia msaada wa Serikali ya Marekani kupitia *Millennium Challenge Corporation (MCC)*, Serikali itajenga kwa kiwango cha lami, barabara za Tunduma – Sumbawanga (Km. 224.5), Songea – Namtumbo (Km. 70), Peramiho – Mbinga (Km. 80), Tanga – Horohoro (Km. 65) na kukarabati Uwanja wa Ndege wa Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara za Vijijini ni muhimu katika kuwasaidia wananchi wanaoishi Vijijini hasa wakulima kusafirisha mazao yao kutoka mashambani hadi kwenye masoko. Ili kufikia azma hiyo, katika mwaka 2007/2008, Serikali za Mitaa zilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 65 kutoka katika Mfuko wa Barabara, kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 37,229. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2008 kiasi cha shilingi bilioni 48.2 kilikuwa kimepelekwa kwenye Halmashauri na kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 7,592 yakiwemo matengenezo ya kawaida kilomita 4,988, matengenezo madogo madogo kilomita 2,099, matengenezo ya muda maalum kilomita 505, pamoja na matengenezo ya madaraja na makalvati.

Mheshimiwa Spika, kupitia Programu ya Usafiri katika Serikali za Mitaa, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 8.2, kwa ajili ya ukarabati wa barabara. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2008, kiasi cha shilingi bilioni 5.8 kilikuwa kimepelekwa kwenye Halmashauri zote nchini, kusaidia kuboresha Kilomita 1,000 za maeneo korofi. Vilevile, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Usafiri na Uchukuzi Vijijini. Programu hii ilitumia jumla ya shilingi bilioni 1.9 kwa Halmashauri 27 ili kufanya matengenezo ya barabara za jamii, ujenzi wa madaraja madogo na kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu matumizi bora ya teknolojia rahisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaendelea kufanya matengenezo ya barabara katika Serikali za Mitaa. Jumla ya shilingi bilioni 65 kutoka kwenye Mfuko wa Barabara, zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Vijijini. Aidha, kupitia Programu ya Usafiri katika Serikali za Mitaa, jumla ya shilingi bilioni 16.8 zitapelekwa katika Halmashauri kwa ajili ya matengenezo ya barabara, maeneo korofi, madaraja na uwekaji wa makalvati. Programu ya Usafiri na Uchukuzi Vijijini, imetengewa shilingi bilioni 1.8 ili kuboresha usafiri vijijini katika Halmashauri 55. Fedha hizi zikisimamiwa vizuri, barabara nyingi za vijijini zitaimarika na kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na tatizo kubwa la usafiri na usafirishaji kutokana na ongezeko la watu na magari. Katika jitihada za kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na maboresho ya barabara zinazoingia na kutoka, Barabara Kuu na kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Usalama Barabarani. Pamoja na hatua hizo, Serikali imekamilisha

maandalizi ya Mpango Kamambe wa Usafirishaji kwa Jiji la Dar es Salaam. Mpango huu umeainisha kwa kina, Mikakati ya Muda wa Kati na Mrefu wa kuondoa kero ya usafiri na msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam. Pamoja na jitihada hizi za Serikali, napenda kusisitiza kuwa, wakati mwingine msongamano wa magari unatokana na uendeshaji wa kibabe. Hivyo, natoa wito kwa madereva wote, kuzingatia Sheria ya Usalama Barabarani na Askari wa Usalama Barabarani waisimamie kikamilifu Sheria hiyo. Aidha, adhabu kali zaidi zitolewe kwa wale watakaokiuka Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi Jijini Dar es Salaam *(Dar es Salaam Rapid Transport - DART)* unaendelea vizuri. Usanifu wa kina utakaowezesha kujengwa kwa miundombinu inayokidhi watumiaji wote wa barabara na matumizi ya mabasi yenye ujazo mkubwa wa kupakia abiria umekamilika. Jumla ya gharama za mradi huu katika Awamu ya Kwanza ni Dola za Marekani milioni 158.2. Kati ya fedha hizo, Serikali ya Tanzania itatoa Dola za Marekani milioni 10, Benki ya Dunia itatoa Dola za Marekani milioni 110 na Sekta Binafsi itawekeza kiasi cha Dola za Marekani Milioni 38.2, kwa kununua mabasi na kujenga mfumo imara wa kukusanya nauli.

Awamu ya Kwanza ina urefu wa kilometa 21 na ina Vituo Vidogo 29, Vituo Vikubwa 5 na maeneo mawili ya maegesho na matengenezo. Fidia kwa Wananchi ambao mali zao zinaathiriwa na ujenzi wa miundombinu ya *DART*, zinaendelea kulipwa na zoezi hilo litakamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2008. Ujenzi wa miundombinu utaanza katika mwaka 2008/2009 na inategemewa utachukua muda wa miezi 24. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha huduma ya Vivuko Nchini, kwa kununua Vivuko vipya na kukarabati vilivyopo. Vivuko vipya vilivyonunuliwa ni vya Kigongo – Busisi chenye uwezo wa kubeba Tani 250, Kivuko cha Kilombero chenye uwezo wa kubeba Tani 50 na Kivuko cha Kigamboni chenye uwezo wa kubeba Tani 500. Aidha, Serikali imenunua Kivuko cha Ruhuhu chenye uwezo wa kubeba Tani 50 kwa ajili ya Wananchi wa Wilaya ya Mbinga na Ludewa. Katika mwaka 2008/2009, Kivuko kipya chenye uwezo wa kubeba Tani 40 kitakachotoa huduma kati ya Nyakalilo na Kisiwa cha Kome kitanunuliwa na Kivuko kipya cha Pangani chenye uwezo wa kubeba uzito wa Tani 50 kinaendelea kuundwa. Vilevile, Vivuko vya M.V. Alina cha Dar es Salaam na Rugezi - Kisorya vimefanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mipango ya usambazaji wa Umeme kwa Wananchi Mijini na Vijijini. Katika mwaka 2007/2008, Serikali imeipatia *TANESCO* fedha za kununua mitambo mipya ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta ya dizeli, yenye uwezo wa kuzalisha *KVA* 1,200 kwa ajili ya Mji wa Mbinga. *TANESCO* pia imekamilisha kazi ya kuweka nyaya za kusambaza umeme katika Mji wa Ludewa. Aidha, kwa kutumia fedha za Mfuko wa Nishati Vijijini, Wakala wa Nishati Vijijini ilifanya upembuzi yakinifu katika maeneo ya Kilolo, Mbinga, Mto wa Mbu, Bahi, Uyui, Mkinga, Simanjiro na Kilindi. Serikali pia imekamilisha upembuzi yakinifu wa Mradi wa *North-West Grid Study* unaojumuisha Mikoa ya Kigoma, Kagera na Rukwa. Vilevile,

shughuli za Mradi wa Uendelezaji Huduma za Nishati Vijijini, unaohamasisha Soko la Umemenuru zimezinduliwa katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Kigoma, Pwani, Rukwa na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nishati pia itafaidika na msaada wa Serikali ya Marekani kupitia *Millennium Challenge Corporation (*MCC*).* Kiasi cha Dola za Marekani milioni 206 kutoka MCC, kitatumika kuboresha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Morogoro, Dodoma na Tanga. Vilevile, kiasi cha Dola za Marekani milioni 63.1 kitatumika katika ujenzi wa njia ya umeme wa chini ya maji kwenda Zanzibar. Aidha, kiasi cha Dola za Marekani milioni 53.7 kitatumika kuzalisha umeme wa Megawati 8 kutokana na nguvu za maji katika Mto Malagarasi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Somanga Fungu. Mradi huu utayanufaisha maeneo ya Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Somanga, Kibiti na maeneo mengine ya jirani. Serikali pia itakamilisha uwekaji umeme katika maeneo ya Kilolo, Mbinga, Mto wa Mbu, Bahi, Uyui, Mkinga, Simanjiro na Kilindi. Aidha, kupitia Wakala wa Nishati Vijijini, Serikali itaongeza kasi ya usambazaji wa Nishati Vijijini, chini ya Mradi wa Uendelezaji na Kupanua Wigo wa Upatikanaji na Usambazaji wa Nishati Nchini.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingi katika Sekta ya Mawasiliano, zinaongozwa na Sekta Binafsi ambazo kwa ujumla zimeonyesha mafanikio makubwa. Kampuni za Simu za Mkononi, zimepanua huduma za mitandao yao hadi Vijijini na hivyo kuwaongezea Watanzania wigo wa mawasiliano. Takwimu zinaonyesha kwamba, wateja wa simu za mkononi wameongezeka kutoka milioni 5.7 mwaka 2006 hadi milioni 8.5 mwaka 2007. Hii ni dalili njema kwani mawasiliano ni kichocheo muhimu cha biashara na hupunguza ulazima wa safari kutoka eneo moja kwenda jingine na hivyo kurahisisha shughuli mbalimbali za kiuchumi. Miundombinu ya huduma za utangazaji pia iliboreshwa na matokeo yake ni kupanuka kwa maeneo yanayofikiwa na huduma za utangazaji zinaotolewa kwa njia za Redio na Luninga na hivyo kuwafikia Wananchi wengi hususan waishio Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliendelea na mchakato wa kuunda Mfuko wa Mawasiliano Vijijini. Mfuko huu utasaidia kufikisha huduma za mawasiliano vijijini kwa kuwapatia ruzuku Wawekezaji walio tayari kupeleka miundombinu na huduma za mawasiliano sehemu zote ambazo hazina mvuto wa kibiashara. Vilevile, Serikali iliendelea kuimarisha vituo vya Mawasiliano Nchini vikiwemo vya Dar es Salaam, Sengerema, Mpwapwa, Kasulu, Mtwara, Kinampanda Mkoani Singida na Wino Mkoani Ruvuma, kwa ajili ya wakulima wa Kahawa. Vituo hivyo vitatumiwa na jamii katika kukuza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa ajili ya biashara, masomo, afya na utawala.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaanza utekelezaji wa awali wa ujenzi na uendelezaji wa Mkongo wa Kitaifa wa Mawasiliano na kuratibu uanzishwaji wa mfumo mpya wa anuani na namba za Posta Nchini ili kurahisisha na

kuboresha huduma zitolewazo na Sekta nyingine. Aidha, Vituo zaidi vya Mawasiliano vitaanzishwa katika Mikoa mingine kwa lengo la kuwafikia Wananchi wengi hususan Makundi ya Wasiojiweza, Wanawake na wengine waishio sehemu za Vijijini. Vituo hivyo vitawawezesha Wananchi kupata habari muhimu za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kwamba, ardhi ni rasilimali ya msingi kwa maendeleo ya Taifa letu na ni tegemeo kubwa la Wananchi wengi kwa kuzalisha mazao ya chakula na biashara. Ardhi ikigawanywa na kutumiwa bila utaratibu unaokubalika na jamii, huwa chanzo kikubwa cha migogoro ya mipaka. Kwa upande mwingine, ardhi ikitumiwa kiholela husababisha uharibufu wa mazingira, mmomonyoko wa ardhi na hivyo kupunguza rutuba ya ardhi na hatimaye Nchi kuwa jangwa. Hivyo, Serikali ina wajibu wa kuhakikisha ardhi yetu, ambayo haiongezeki, inatumiwa kwa busara ili iweze kuendelea kuwa rasilimali endelevu kwa maendeleo ya sasa na ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeshuhudia kuongezeka kwa migogoro ya ardhi, inayosababishwa na jamii za Wakulima na Wafugaji, kugombea maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na maendeleo. Aidha, kumekuwepo na migogoro ya mipaka kati ya Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji. Serikali imebaini kuwa, sababu kuu za migogoro hiyo ni pamoja na kung’olewa au kupotea kwa alama za mipaka na ukuaji holela wa Vijiji, kiasi cha kuingilia maeneo mengine ya kiutawala kama vile maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa au Hifadhi ya Vyanzo vya Maji. Vilevile, kumekuwepo na ufahamu mdogo wa baadhi ya Wananchi na Watendaji juu ya mipaka ya maeneo yao ya kiutawala kutokana na ukweli kwamba, maelezo ya mipaka yaliwekwa miaka mingi iliyopita. Katika maeneo ya Mijini, kumekuwa na ukiukwaji wa Sheria na Taratibu za Mipango Miji, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba bila vibali vya Mamlaka ya Miji husika.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na matatizo hayo ya ardhi, katika mwaka 1995, Serikali iliandaa Sera ya Ardhi, ambayo utekelezaji wake ulianza kwa kutunga Sheria mbalimbali. Maudhui ya Sheria hizo ni kutoa maelekezo ya Taratibu na Kanuni za Umiliki na matumizi endelevu ya ardhi yetu. Maandalizi ya Sera na Sheria hizi yalishirikisha Wadau wengi na yamezingatia mabadiliko ya kiuchumi na mahitaji ya utandawazi. Sheria hizo zimeanza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kuunda Vyombo vya Usimamizi wa utekelezaji wake. Vyombo hivyo ni pamoja na Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na Mabaraza ya Ardhi. Tume ina jukumu la kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi na Mabaraza ya Ardhi yanashughulikia Mashauri ya migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, ikitekeleza majukumu yake ya kupanga matumizi bora ya ardhi ipasavyo katika ngazi ya Taifa, Mikoa, Wilaya, Miji na Vijiji, itazuia kwa kiasi kikubwa, kutokea migogoro ya ardhi Nchini. Vilevile, Mabaraza ya Ardhi yakifanya kazi zake kwa ufanisi, yataharakisha uamuzi wa Mashauri ya Ardhi na hivyo kuendeleza amani Nchini. Hali hii itawavutia Wawekezaji wa ndani na nje, kuwekeza katika mashamba ya biashara, viwanda na hoteli katika maeneo ambayo yametengwa na kupimwa kwa shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, uzoefu uliopatikana katika zoezi la kuwahamisha Wafugaji na mifugo yao kutoka Bonde la Ihefu, umedhihirisha umuhimu wa kuwashirikisha Wadau mbalimbali katika upangaji wa matumizi bora ya ardhi ikiwa ni pamoja na Viongozi wa Mikoa, Wilaya, Serikali za Mitaa na Vijiji. Katika zoezi hilo, Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Serikali za Vijiji, iliweza kuainisha maeneo ya kutosha ya kuhamishia mifugo katika Wilaya za Kisarawe, Rufiji, Lindi, Nachingwea na Kilwa. Maeneo hayo ya malisho, yaliweza kupatikana baada ya Halmashauri hizo kuandaa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika**,** kwa kutambua mafanikio yaliyopatikana katika utaratibu Shirikishi wa kutayarisha Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi chini ya uratibu wa Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi; naelekeza kwamba, kila mwaka Halmashauri zitenge fedha za kutosha kwa ajili ya utayarishaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. Zoezi hili liende sambamba na upimaji wa viwanja Mijini na mashamba makubwa ya kilimo na ufugaji. Aidha, Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi itaimarishwa ili kuiwezesha kuratibu utayarishaji na usimamizi wa utekelezaji wa Mipango hiyo muhimu. Lengo ni kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kila Halmashauri na kila Kijiji na Miji yote. Zoezi hili liende sambamba na uboreshaji wa Kumbukumbu za Ardhi na ujenzi wa Masjala za Ardhi katika ngazi za Wilaya na Vijiji ili kupunguza migogoro ya miliki za viwanja na mashamba.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii, kutoa rai kwa Wananchi na Viongozi wa ngazi zote, kutoa ushirikiano katika utatuzi wa migogoro ya ardhi. Katika kusuluhisha migogoro hiyo, ni vyema tukajenga utamaduni wa kukaa kwa pamoja na kumaliza matatizo kabla hayajawa makubwa na kuleta athari kwa Wananchi. Vilevile, napenda kutoa tahadhari kwa Wananchi ambao wanavamia ardhi iliyokwishapimwa na kuendeleza makazi na kudai fidia pale wanapoondolewa Kisheria. Serikali haitavumilia ukiukwaji huu wa Sheria na Taratibu za Nchi na haitasita kuwachukulia hatua za kinidhamu mara moja, watumishi watakaobainika kutokuwa waadilifu katika utoaji wa huduma za ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali ilipanga kutoa mbolea ya ruzuku kiasi cha Tani 89,820. Hadi kufikia mwezi Mei, 2008 Tani 74,503, sawa na asilimia 83 ya lengo zilikuwa zimesambazwa. Vilevile, jumla ya Tani 3,222 na Lita 133,463 za dawa ya korosho zilisambazwa kwa utaratibu wa ruzuku. Bodi ya Pamba ilinunua na kusambaza dawa za kuulia wadudu aina ya *acrepacks* 500,000, zenye thamani ya shilingi bilioni 1.4. Aidha, jumla ya Makampuni 12 yalisaini Mkataba na Serikali wa kusambaza Tani 1,770 za mbegu za Mazao ya Mahindi, Mtama na Alizeti. Hadi mwezi Aprili, 2008, jumla ya Tani 1,170 za mbegu sawa na asilimia 66 zilifikishwa katika vituo 21 vya usambazaji Mikoani, ambapo Tani 969 zimeuzwa kwa Wakulima. Kwa upande wa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo, hadi kufikia mwezi Mei, 2008, jumla ya shilingi bilioni 3.1 kati ya Shilingi bilioni 3.5 zilizotengwa, zimetolewa kwa ajili ya kutoa mikopo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija katika kilimo, hatua kabambe zitakazowezesha ongezeko la uzalishaji katika Sekta hiyo inabidi zichukuliwe. Hatua ya kwanza itakuwa ni kuhakikisha kwamba, Wakulima wanapata mbolea nyingi kwa msimu ujao wa kilimo ili waweze kuongeza uzalishaji. Ili Wakulima wapate mbolea hiyo kwa wakati na kwa gharama nafuu, katika mwaka 2008/2009, Serikali itatoa dhamana kwa Kampuni ya Mbolea Tanzania ili iweze kununua na kusambaza Tani 150,000 za mbolea ya kupandia itakayozalishwa na Kiwanda cha Minjingu kabla ya msimu wa mvua kuanza. Aidha, itaongeza fedha za ruzuku kwa ajili ya usafirishaji wa mbolea ili kuwezesha Vyombo vitakavyosafirisha mbolea yote inayozalishwa Minjingu, pamoja na ile itakayoagizwa kutoka nje, kusafirishwa na kuwafikia Wakulima kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Juni, 2008 nilitembelea Kiwanda cha Mbolea Minjingu. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kufanya mazungumzo na Uongozi wa Kiwanda hicho ili kubainisha mahitaji ya msingi ya muda mfupi na mrefu, ambayo Serikali inaweza kuyatafutia ufumbuzi ili kukiwezesha kiwanda hicho, kuzalisha mbolea nyingi zaidi. Aidha, nilitaka kujiridhisha kama Kiwanda hiki kina uwezo wa kutengeneza Mbolea ya kutosha, ambayo kwa sasa tunaihitaji sana kutokana na unafuu wa bei ikilinganishwa na mbolea zinazoagizwa kutoka nje. Nimehakikishiwa na Uongozi wa Kiwanda cha Minjingu kwamba, kina uwezo wa kuzalisha mbolea ya *Phosphate* kati ya Tani 150,000 hadi 200,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali itakiwezesha Kiwanda cha Mbolea Minjingu kuagiza nje virutubisho maalum kama *Sulphur, Nitrogen Potassium, Zinc na Copper* ili viongezwe kwenye mbolea ya chengachenga inayozalishwa na Kiwanda hicho. Hatua hii itaongeza ubora wa mbolea hiyo. Vilevile, Serikali itafanya mazungumzo na Makampuni ya nje ambayo yapo tayari kuwekeza Nchini kwa ajili ya kuzalisha mbolea za aina mbalimbali. Lengo ni kuiwezesha Nchi yetu katika kipindi kifupi kijacho, kujitosheleza kwa mahitaji yake ya ndani ya mbolea na ziada kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili, 2008 wakati ninatoa hoja ya kuahirisha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, nilielezea kwa undani, hatari iliyopo mbele yetu kutokana na kupanda kwa bei ya vyakula duniani. Japokuwa takwimu za uzalishaji wa chakula zinaonyesha kwamba, Taifa lingejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 106 kwa msimu wa 2007/2008, bado kulijitokeza uhaba wa nafaka uliosababisha bei za vyakula hivyo kupanda ghafla kuanzia mwezi Desemba, 2007 hadi sasa.

Sisi kama Taifa, hatuna budi tujiandae katika kipindi cha muda mfupi na kujiwekea Mkakati wa Muda Mrefu wa kujitosheleza kwa chakula. Hatua za kuongeza mbolea ya ruzuku na kuhakikisha inamfikia Mkulima kwa wakati ni sehemu ya Mkakati wa kuongeza uzalishaji na kujitosheleza kwa chakula na kuuza ziada nje. Vilevile, katika bajeti ya mwaka 2008/2009, Kitengo cha Hifadhi ya Chakula kimeongezewa uwezo wa kifedha wa Shilingi bilioni 26.3 ili kiweze kununua Tani 100,000 za Mahindi na Tani 5,000 za Mtama na kuhifadhi kwa ajili ya siku zijazo. Naomba kukiagiza Kitengo cha Hifadhi ya Taifa ya Chakula, kinunue nafaka kutoka kwa Wakulima kwa wakati ili kuzuia uwezekano wa Wakulima kuuza chakula kwa Walanguzi na nje ya Nchi na baadaye kukinunua kwa bei kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa sababu za kupanda kwa bei ya chakula duniani ni pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya chakula duniani, ukame na kupanda kwa gharama za uzalishaji kulikosababishwa na kuongezeka kwa bei ya mafuta. Aidha, bei zimepanda kutokana na uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula unaosababishwa na mashamba makubwa yenye ardhi nzuri kutumika kuzalisha mazao yanayotumika kuzalisha nishati mbadala itokanayo na mimea. Hali hii ya mahitaji makubwa ya ardhi nzuri kwa ajili ya uzalishaji wa nishati mbadala, imeanza pia kujitokeza hapa Nchini. Serikali inaandaa Sera na Mwongozo wa kuendeleza kilimo cha mazao ya nishati ili kisiathiri kilimo cha mazao ya chakula hapa Nchini. Vilevile, inaandaa Mkakati wa kutambua maeneo yanayofaa kwa Kilimo Nchini ili kuwavutia Wawekezaji, katika kilimo cha mashamba makubwa. Hatua hizi zitasaidia kwa kiasi kikubwa, kukuza Sekta ya Kilimo kwa ujumla, pamoja na kuzalisha chakula cha kutosha kwa matumizi ya ndani na ziada kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali imeendeleza hekta 11,352 za Umwagiliaji kwa kujenga miundombinu katika Kanda Saba za Umwagiliaji. Ili kuwezesha uendelezaji wa umwagiliaji katika Kanda hizo, upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu 88 za umwagiliaji na mabwawa saba umekamilishwa. Aidha, Wakulima Wadogo waliopo kandokando ya Ziwa Viktoria wamepatiwa vifaa vya umwagiliaji chini ya Mradi wa Kusaidia Wakulima Wadogo, unaotekelezwa kati ya Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na *FAO* na Serikali ya Japan.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itakarabati skimu 20 zilizochakaa pamoja na zilizoharibiwa na mafuriko ili kuendeleza eneo lipatalo hekta 15,000. Aidha, itakarabati mabwawa madogo 10 ili kuendeleza eneo la hekta 3,000 hususan katika maeneo yenye ukame na upimaji na usanifu wa skimu 68 zitakazowezesha kumwagilia hekta 200,000. Serikali pia itakamilisha Sera ya Umwagiliaji na Mkakati wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Nchini. Hatua hizi zitaenda sambamba na kufanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Maendeleo ya Ushirika. Katika mwaka 2007/2008, Vyama 960 vya aina mbalimbali vilikaguliwa na Wananchi walihamasishwa kuanzisha na kujiunga katika *SACCOS* na kufanya idadi ya *SACCOS* Nchini kuongezeka kutoka 3,469 mwezi Mei, 2007 hadi 4,445 mwezi Desemba, 2007. Vilevile, katika kipindi hicho, hisa za Wanachama zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 18.2 hadi bilioni 21.7 na Amana kutoka Shilingi bilioni 59.7 hadi Shilingi bilioni 91.2.

Mheshimiwa Spika, Vyama Vikuu vya Msingi katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Dar es Salaam, vimewezeshwa kufanya biashara ya ununuzi na uuzaji wa korosho kwa kukopeshwa fedha za udhamini wa Serikali, kiasi cha Shilingi bilioni 28.4. Hadi mwezi Februari, 2008, mikopo hiyo imewezesha ununuzi wa Tani 92,000 za korosho. Vyama vyote vimerejesha mikopo ya Benki na Halmashauri katika Mikoa hiyo, zimelipwa jumla ya Shilingi bilioni 2.62 kama ushuru. Napenda niliarifu Bunge lako

Tukufu kwamba, katika mwaka 2007/2008, Serikali imetimiza ahadi yake ya kupunguza mzigo wa madeni wa Vyama vya Ushirika kwa kulipa jumla ya shilingi bilioni 2.5.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaendelea kuviimarisha Vyama vya Ushirika kwa kuwapa mafunzo Maafisa Ushirika na kuwapeleka Maafisa Ushirika katika Halmashauri zisizo na Maafisa hao ili kutoa msukumo na kuimarisha usimamizi. Aidha, Serikali inaandaa utaratibu wa kuwa na Chombo Mahususi kwa ajili kutoa mikopo kwa Wakulima na Wafugaji.

Mheshimiwa Spika**,** mwenendo wa ukuaji wa Sekta ya Madini, umeendelea kuwa mzuri kutokana na kupanuka kwa shughuli za uchimbaji na biashara ya madini hasa dhahabu. Mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2006 na kufikia asilimia 2.7 mwaka 2007. Mchango wa Sekta ya Madini utaendelea kukua zaidi kufuatia mabadiliko ambayo Serikali inaendelea kuyafanya katika kupitia Sera, Sheria na Kanuni za Madini ili itoe mchango mkubwa zaidi katika uchumi wa Taifa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Rais chini ya Jaji Mark Bomani mwaka 2007, imemaliza kazi yake na kutoa mapendekezo yake mazuri ambayo yatazingatiwa katika maboresho ya Sera na Sheria ya Madini na Sekta ya Madini kwa ujumla. Wizara ya Nishati na Madini itatoa ufafanuzi zaidi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali ilitenga maeneo kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo katika sehemu mbalimbali Nchini kama ifuatavyo: Sehemu za Kilindi, Kilosa na Morogoro Vijijini hekta 269,842; sehemu za Maganzo, Kishapu na Ibadakuli Mkoani Shinyanga hekta 14,870; sehemu za Mererani Mkoani Manyara hekta 10,490; sehemu za Rwamagaza na Nyarugusu Wilayani Geita hekta 1,210; maeneo ya Ngasamo Wilayani Magu hekta 229; sehemu za Rwabasi na Nyaserero Wilayani Musoma Vijijini hekta 621; na maeneo ya Matabe Wilayani Chato hekta 880. Aidha, Serikali imewahamasisha Wachimbaji Wadogo katika maeneo mengi Nchini kuanzisha *SACCOS* ili waweze kumiliki maeneo yaliyotengwa na kupimwa viwanja vya uchimbaji. *SACCOS* zipatazo 40 zimeanzishwa katika maeneo ya Rwamgaza na Nyarugusu Wilayani Geita. Njia hii ya kuwaunganisha Wachimbaji Wadogo, itawasaidia sana kupata mitaji mikubwa na kuzalisha kwa kiasi kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwezi Machi na Aprili, 2008, kulitokea maafa makubwa katika Migodi ya Mererani, Mkoani Manyara na Matundasi, Wilaya ya Chunya. Sababu ya msingi ya kutokea maafa haya ni usalama mdogo katika migodi hiyo. Hali hiyo ipo katika migodi mingine mingi, ambayo inamilikiwa na Wachimbaji Wadogo. Suala hili la usalama mdogo katika migodi inabidi sasa lipatiwe ufumbuzi wa kudumu kwa kuhakikisha kwamba, Wamiliki wa Migodi hii wanafuata Kanuni zilizopo za Usalama Migodini ili kuepuka maafa kama haya kutokea tena. Napenda ieleweke kwamba, baadhi ya Wamiliki wa Migodi wanaoitwa Wachimbaji Wadogo, si wadogo kiasi cha kushindwa kuwekeza kwenye miundombinu ya msingi ya usalama wa migodi.

Maafisa wa Madini wahakikishe kwamba, Wachimbaji hao wanazielewa Kanuni za Usalama na kuhakikisha zinafuatwa. Katika mwaka 2008/2009, Sera na Sheria ya

Madini itafanyiwa mapitio kwa kuzingatia mapendekezo na maoni ya Kamati mbalimbali. Vilevile, Serikali itatoa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Usonara na Uboreshaji Thamani ya Madini. Serikali pia itatenga maeneo zaidi kwa Wachimbaji Wadogo ikianzia na eneo lenye hekta 4,000 huko Winza, Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuvutia Wawekezaji katika ufufuaji wa Viwanda vilivyopo na kujenga vipya katika Sekta zilizopewa kipaumbele. Utafiti uliofanyika katika Sekta hii mwaka 2007, ulibaini kuwepo kwa ongezeko la uanzishwaji wa Viwanda Vipya na ufufuaji wa Viwanda vya Umma vilivyobinafsishwa. Utafiti pia umebaini kwamba, asilimia 97.6 ya Viwanda vipo mikononi mwa Sekta Binafsi; utumiaji wa uwezo katika Sekta ya Viwanda umekua kutoka wastani wa asilimia 37 mwaka 2005 hadi asilimia 43 mwaka 2008 na ongezeko la ajira la asilimia 8.7 kati ya mwaka 2006 na 2007. Ili kukuza Sekta ya Viwanda na kuvutia Wawekezaji, Serikali imeanza maandalizi ya Mkakati Unganishi na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda. Mkakati huu unalenga kuendeleza Viwanda vya Msingi, vitakavyoongeza kasi ya kuzalisha malighafi kwa ajili ya Viwanda vingine, jambo litakalosaidia kupunguza uagizaji wa malighafi kutoka nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mamlaka ya Mauzo Nje, Serikali imebainisha maeneo yenye ukubwa wa zaidi ya hekta 2,000 katika Mikoa saba ya Pwani, Kilimanjaro, Arusha, Mara, Kigoma, Mtwara na Morogoro. Maeneo hayo ni kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuuza nje. Zoezi la kubainisha maeneo katika Mikoa mingine linaendelea. Tangu Mamlaka hiyo ianze kazi mwezi Oktoba, 2006 hadi sasa viwanda 16 vimeanzishwa. Uzoefu wa Nchi za China, Indonesia, Malaysia na Thailand ambazo uchumi wake umeendelea kukua kwa kasi kubwa, zimewekeza sana kwenye maeneo ya aina hii. Katika Kongamano kati ya Wafanyabiashara wa China na Afrika lililofanyika Mjini Arusha mwezi Aprili, 2008, Wafanyabiashara kutoka China walionyesha nia ya kuwekeza katika Maeneo Maalum ya Biashara. Tutumie fursa hii kujifunza kutoka kwao ili tusaidiane nao katika kuanzisha na kuendesha maeneo haya. Aidha, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji Tanzania washirikiane na Wafanyabiashara kuchangamkia fursa hii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itakamilisha Mkakati Unganishi na Mpango Kabambe wa kuendeleza Sekta ya Viwanda Nchini. Vilevile, Serikali itaanza kutekeleza Mpango Mkakati wa Kuongeza Uzalishaji na Kukuza Mauzo Nje, kwa kubainisha maeneo yatakayoleta matokeo ya haraka. Serikali pia itaendelea kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa Programu mbalimbali ili kuongeza mchango wa shughuli za viwanda vidogo katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika**,** ukuaji wa Sekta ya Utalii ni muhimu sana katika jitihada zetu za kuongeza mauzo ya nje. Kwa kipindi cha mwaka 2007, mchango wa Sekta hiyo kwenye mauzo ya nje ulifikia Dola za Marekani bilioni 1.04, sawa na asilimia 27.8 ya mauzo yote ya nje. Sekta hii ndiyo iliyotoa mchango mkubwa katika mauzo ya nje ikilinganishwa na Sekta nyingine zote. Mafanikio hayo yametokana na juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali za kuitangaza nje biashara ya Utalii, pamoja na kushirikisha kikamilifu Balozi zetu katika Nchi mbalimbali duniani. Hata hivyo, Sekta hii inayo

nafasi kubwa ya kuongeza zaidi mchango wake katika uchumi. Idadi ya Watalii watakaotembelea Bara la Afrika, inakadiriwa kufikia milioni 77.3 itakapofika mwaka 2020. Hivyo, tuhakikishe kwamba, ongezeko hili la Watalii Barani Afrika, linafaidisha uchumi wetu. Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kushirikiana na Balozi zetu, ziandae Mkakati Maalum wa kutangaza vivutio vyetu hasa katika zile Nchi ambazo Watalii wengi hutokea.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kwamba, zaidi ya asilimia 80 ya Watalii duniani, wanatokea katika Nchi tajiri 20 tu; 17 kati ya hizo zikiwa ni za Ulaya, Marekani, Canada na Japan. Karibu nusu ya matumizi yote ya Utalii hufanywa na Watalii kutoka Marekani, Japan, Ujerumani, Ufaransa na Uingereza. Hii ni changamoto kwetu, itakayotusaidia kutilia mkazo vipaumbele katika kutangaza Utalii wetu. Ni vyema hatua za makusudi kabisa zichukuliwe, kuifanya Tanzania na Vivutio vyake vijulikane katika Nchi hizi. Vilevile, ni muhimu kujitangaza katika Nchi zile ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa kama vile India, Urusi na China na nyinginezo pasipo kusahau kutangaza Vivutio vyetu kwa Nchi za ukanda wetu na Utalii wa ndani.

Pamoja na hili, ni lazima miundombinu mingine inayowezesha Sekta ya Utalii kama vile usafiri, huduma za hoteli, fedha na nyinginezo ziimarishwe ili kusaidia Watalii wawapo hapa Nchini. Aidha, mafunzo katika fani ya Utalii yaimarishwe ili kuweza kuwahudumia Watalii vizuri. Tunaweza kupata Watalii wengi sana lakini tusiweze kuendeleza ujio wao kutokana na huduma mbovu wanazopata wawapo hapa Nchini. Ni vyema sasa tubadilike na tufahamu kwamba, ongezeko la Watalii hapa Nchini litatokana na sisi wenyewe kujitangaza na huduma bora watakazopatiwa wawapo Nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuipa msukumo Sekta ya Mifugo ili itoe mchango mkubwa zaidi katika uchumi. Katika mwaka 2007/2008, uzalishaji wa maziwa uliongezeka na kufikia lita bilioni 1.5 ikilinganishwa na lita bilioni 1.4 mwaka 2006/2007. Uzalishaji wa nyama pia uliongezeka kutoka Tani 370,566 hadi Tani 410,706. Ongezeko hili linatokana na kupanuka kwa wigo wa masoko mapya yanayonunua maziwa na nyama bora inayozalishwa Nchini. Vilevile, jumla ya ng’ombe 2,472 na mbuzi 733 wenye thamani ya Shilingi bilioni 1.3 wameuzwa Nchi za Comoro, Malawi na Burundi. Aidha, nyama ya kondoo, mbuzi na ng’ombe, yenye thamani ya Shilingi milioni 376.6 imeuzwa Nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, Oman na Kuwait.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, jumla ya hekta 930,276 zimepimwa na kutengwa na Halmashauri kwa ajili ya Wafugaji katika Wilaya 24 za Mikoa ya Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Lindi, Mbeya, Morogoro, Pwani, Singida na Tabora. Kuhusu chanjo za mifugo, jumla ya dozi milioni 8.1 zimezalishwa na kusambazwa sehemu mbalimbali Nchini. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali, imeendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti milipuko ya magonjwa Nchini. Mkakati wa kudhibiti ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa umetekelezwa na hadi mwezi Desemba, 2007 jumla ya mifugo milioni 4.3 ilichanjwa. Aidha, jumla ya Wanafunzi 1,007 waliendelea na mafunzo ya Stashahada na Astashahada katika Vyuo sita vya Mifugo na kati ya hao, 393 wamehitimu na wataajiriwa katika Halmashauri. Pia jumla ya

Wafugaji 21,106 walipatiwa mafunzo kuhusu ufugaji bora kwa njia za Mafunzo Vituoni na kupitia Semina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi nayo ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wetu na uwezo wa kuajiri Watanzania wengi. Katika kipindi cha mwaka 2007, mapato yatokanayo na mauzo ya mazao ya Uvuvi nje ya Nchi yalikuwa Shilingi bilioni 7.6, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 6.2, sawa na ongezeko la asilimia 21.7.

Kwa kutambua umuhimu wa Sekta hiyo, Serikali imeandaa Mpango wa Kitaifa wa Kudhibiti Uvuvi Usiozingatia Sheria. Mpango huo umeandaliwa ili kudhibiti uvuvi haramu na kuhakikisha usalama na viwango vya mazao ya uvuvi. Serikali pia imeanzisha mfumo wa kuratibu mwenendo wa meli baharini, ikiwa ni hatua ya kudhibiti meli za nje zinazovua kiholela katika maji mengi kwenye Ukanda wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga mialo 19 ya kupokelea samaki kwenye Ukanda wa Ziwa Viktoria. Vilevile, uchambuzi wa kujenga mialo sita katika Ukanda wa Bahari ya Hindi unafanywa ili kuwezesha Wavuvi Wadogo kushiriki katika uuzaji samaki katika soko la nje. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Nchi yetu imetimiza vigezo vyote vinavyohitajika katika Soko la Jumuiya ya Ulaya na kuruhusiwa kuuza samaki na mazao ya uvuvi katika soko hilo na mengineyo. Aidha, Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi imethibitishwa na *South African National Accreditation Services,* kuweza kuchunguza vimelea kwenye mazao yote ya chakula ikiwa ni pamoja na Samaki. Ithibati hii imeifanya Maabara ya Nyegezi kutambulika kimataifa. Hii ni nafasi nzuri kwa Nchi yetu kutumia ipasavyo Mikataba ya Biashara iliyopo kati ya Nchi za Ulaya na Afrika kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itapitia na kuandaa Mikakati na Sheria zitakazoimarisha Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Lengo ni kuongeza uzalishaji, kuimarisha udhibiti, ubora na usalama, kuwa na masoko ya uhakika na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi. Aidha, Serikali itaboresha na kuongeza huduma za tafiti na ugani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali imeendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II). Idadi ya Shule za Msingi za Serikali imeongezeka kutoka Shule 14,400 mwaka 2006 hadi 15,300 mwaka 2007. Aidha, idadi ya Wanafunzi iliongezeka kutoka 7,959,884 mwaka 2006 hadi 8,316,925 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Vilevile, Serikali iliendelea kujenga na kupanua miundombinu katika Shule za Msingi, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu 1,339, vyumba vya madarasa 2,313, matundu ya vyoo 847 na madawati 18,221. Sambamba na ujenzi wa miundombinu, Serikali iliendelea kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia vikiwemo vitabu vya ziada na kiada, matufe na vivunge vya Sayansi na Hisabati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) na kuufanyia maboresho ili kwenda sambamba na ongezeko la idadi ya Wanafunzi wanaofaulu kutokana na

utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi. Usajili wa Shule za Sekondari umeongezeka kutoka Shule 2,289 mwaka 2006 hadi 3,485 mwaka 2007. Idadi ya Wanafunzi wa kidato cha I - VI, katika Shule za Sekondari iliongezeka kutoka Wanafunzi 675,672 mwaka 2006 hadi 1,020,510 mwaka 2007. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Wananchi na Wadau wengine, iliendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa 777, nyumba za walimu 1,470, maabara 84, maktaba 19, majengo ya utawala 9, ujenzi wa hosteli 12 kwa ajili ya Wasichana kutoka katika Mikoa ya Wafugaji na iliyo nyuma kielimu na ukarabati wa miundombinu katika Shule 8 zenye Wanafunzi wenye mahitaji maalum. Sambamba na ujenzi huo, Serikali iliendelea kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa lengo la kuboresha Elimu ya Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha Wananchi pamoja na Wadau wengine, kugharamia Elimu ya Juu kupitia Mfuko wa Elimu. Katika mwaka 2007/2008, Mfuko wa Elimu ulipokea na kufadhili mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.8 kwa Taasisi 205 katika ngazi zote za elimu. Vilevile, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, imetoa mikopo kwa Wanafunzi 55,584 na imeendelea kukusanya madeni kwa Wanafunzi waliopewa mikopo kuanzia mwaka wa masomo 1994/1995. Hadi sasa kiasi cha Shilingi milioni 665.2 kimekusanywa na hivyo kufanya Bodi ya Mikopo iwe endelevu. Ili kuhakikisha kwamba, idadi kubwa ya Wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita wanapata Elimu ya Juu, Serikali ilifungua rasmi Chuo Kikuu cha Dodoma. Katika mwaka 2007/2008, jumla ya Wanafunzi 1,116 walidahiliwa na katika mwaka 2008/2009, Chuo hicho kinatarajia kudahili Wanafunzi 5,000.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaongeza upatikanaji wa vifaa vya kutosha vya kujifunzia na kufundishia katika Shule za Msingi na Sekondari. Aidha, itainua uwezo wa Vyuo vya Ufundi vya Halmashauri za Wilaya za Korogwe, Karagwe na Mwanga. Vilevile, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Kuinua na Kuendeleza Mpango wa Elimu ya Juu na Ufundi (MMEJU). Serikali pia itaongeza udahili hadi kufikia asilimia 12.5 ya Wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Sita ili wapate nafasi ya kujiunga na Vyuo Vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maji ni miongoni mwa huduma muhimu kwa Wananchi wote. Ili kuwawezesha Wananchi wengi zaidi Mijini na Vijijini, kupata huduma ya maji safi na salama, Serikali iliendelea kukarabati Miradi ya Maji Vijijini, kujenga mabwawa hususan katika maeneo yenye ukame na kuendeleza teknolojia ya uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua. Kufuatia jitihada hizo, upatikanaji wa huduma ya maji safi kwa Wakazi wa Vijijini umeongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2006 hadi asilimia 55.7 mwaka 2007 ikiwa ni ongezeko la asilimia 2.0. Uzalishaji maji mijini uliongezeka kutoka mita za ujazo milioni 99.99 mwaka 2006 hadi milioni 100.2 mwaka 2007. Ongezeko hilo liliwezesha upatikanaji wa maji mijini kufikia asilimia 73.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itakamilisha ujenzi wa matoleo ya maji na mifumo ya kusambaza maji kwa Vijiji 54 na kuwaunganisha wateja kwenye mfumo wa usambazaji maji. Aidha, itatekeleza mradi wa upanuzi wa milango ya maji na kulaza bomba kuu la majisafi lenye urefu wa kilometa 55 kutoka Ruvu Chini hadi Dar es Salaam. Serikali pia itaendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bwawa la

Kidunda na kutambua wingi na ubora wa maji yaliyo chini ya ardhi katika maeneo ya Kimbiji na Mpera kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi wa kusambaza maji Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Afya na kuimarisha kiwango cha utoaji wa huduma za afya. Katika mwaka 2007/2008, Serikali ilianza kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano, unaolenga kupunguza vifo vya Watoto Wachanga na Wanawake vinavyotokana na uzazi. Vilevile, Serikali ilikamilisha mipango ya utoaji wa huduma za upasuaji wa moyo humu Nchini na kazi ya upasuaji ilianza tarehe 21 Mei, 2008 katika Taasisi ya Mifupa ya MOI iliyoko Jijini Dar es Salaam. Hadi kufikia tarehe 13 Juni, 2008 wagonjwa 11 walifanyiwa upasuaji na wanaendelea vizuri. Serikali pia imeendelea kuzipatia dawa, vitendea kazi na vifaa vya kisasa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati za Umma hapa Nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imekamilisha maandalizi ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa malengo ya Sera ya Afya. Lengo kuu la Mpango huo ni kusogeza huduma za afya karibu na Wananchi kwa kuhakikisha kuwa, kila Kijiji kinakuwa na Zahanati, kila Kata inakuwa na Kituo cha Afya na kila Wilaya inakuwa na Hospitali na kuhakikisha kwamba, Wataalamu wenye ujuzi wanaandaliwa kwa kila Kituo cha kutolea Huduma za Afya. Hadi sasa, Serikali imefanikiwa kufungua Zahanati 253 kati ya 652 zilizojengwa na *TASAF* na Zahanati 399 zilizobaki, majengo yake yapo katika hatua za kukamilishwa. Vilevile, Serikali imekarabati Hospitali 11 za Mikoa ya Tabora, Lindi, Dodoma, Kigoma, Shinyanga, Singida, Rukwa, Mara, Iringa, Ruvuma na Tanga. Ukarabati wa Hospitali hizi upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano, unaolenga kupunguza vifo vya Watoto na Wanawake na kuhakikisha kuwa, huduma bora za Afya ya Uzazi na Mtoto zinatolewa bila malipo. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha chanjo zinatolewa katika Vituo vya Mama na Mtoto na kwa sehemu zisizo na Vituo vya Mama na Mtoto, Huduma ya Mkoba itaendelea kutumika. Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 23 kwa ajili ya MMAM ili kuanza ujenzi wa Zahanati na ukarabati wa Hospitali za Wilaya. Halmashauri zitakazoanza kunufaika na Mpango huo zitajulikana baada ya mahitaji kuainishwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya mipaka ya Nchi yetu kwa ujumla ni shwari. Vyombo vyetu vya Ulinzi kwa kushirikiana na Wananchi, vimefanikiwa kudhibiti matukio ya uhalifu na ulinzi wa mipaka yetu. Vilevile, Jeshi letu la Wananchi limeweza kushirikiana na wenzao wa Kimataifa katika ulinzi wa amani kwenye Nchi zenye migogoro kama vile Lebanon, Sudan na Comoro. Nichukue fursa hii tena, kulipongeza kwa dhati, Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kumng’oa madarakani Kiongozi Muasi wa Kisiwa cha Anjuani, Kanali Mohamed Bakari.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Wananchi, liliendelea kufanya operesheni mbalimbali zenye lengo la kukomesha uhalifu. Wananchi wameanza kufahamu umuhimu wa Mpango wa Ulinzi Shirikishi na ninapenda kuchukua fursa hii,

kuwapongeza kwa kushiriki katika Mpango huo ambao umepunguza kwa kiasi kikubwa, vitendo vya uhalifu Nchini. Aidha, nalipongeza Jeshi la Polisi, kwa juhudi wanazofanya za kulinda usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Ulinzi na Usalama wa ndani ya Nchi na katika mipaka yetu na Nchi jirani utaimarishwa. Serikali itakamilisha mchakato wa kuandaa Sera za Usalama wa Raia, Polisi Jamii, Usalama Barabarani na Ulinzi wa Kampuni Binafsi. Aidha, Kitengo cha Intelijensia cha Jeshi la Polisi kitaimarishwa ili kiwe na uwezo mkubwa zaidi wa kubaini mipango ya matukio ya uhalifu. Vilevile, Serikali itavijengea uwezo Vyombo vya Ulinzi ili viwe imara na vyenye utaalam wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali imeendelea na juhudi za Mapambano Dhidi ya Rushwa ndani na nje ya Taasisi zake. Hadi mwezi Machi, 2008, jumla ya tuhuma 754 zilipokelewa. Aidha, tuhuma za Mikataba mikubwa na matumizi mabaya ya fedha za Serikali zilifanyiwa kazi. Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kutoa mafunzo na Semina kwa Watumishi wa Umma na Wananchi kuhusu Mapambano Dhidi ya Rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wananchi wataendelea kuelimishwa kuhusu Sheria mpya ya Kuzuia Rushwa. Ofisi saba ndogo za TAKUKURU zitafunguliwa katika maeneo ya Makambako, Ilula, Isaka, Holili, Mtukula, Kyaka na Tunduma. Uchunguzi wa tuhuma mbalimbali utafanyika na mkazo zaidi utawekwa kwa tuhuma za Mikataba Mikubwa ambayo inaiingizia Serikali hasara. Serikali itaendeleza Mapambano Dhidi ya Rushwa kwa kuwachukulia hatua za Kisheria, Kiutawala na Kinidhamu, wale wote watakaobainika kuhusika na vitendo vya Rushwa. Aidha, itajenga mazingira mazuri zaidi yatakayowapa Wananchi uwezo, ari na ujasiri wa kutoa taarifa na kupambana na Rushwa, wizi na ubadhirifu wa Mali ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa Awamu ya Kwanza, ilitekelezwa kuanzia mwaka 1999 hadi Juni, 2008. Lengo kuu la Programu hii lilikuwa ni kupeleka Madaraka kwa Wananchi. Katika kufikia lengo hilo, Programu ililenga kuweka mgawanyo bora wa majukumu kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na kuimarisha usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, ililenga kuwajengea uwezo wa kitaalam Watumishi wa Serikali za Mitaa, kuboresha miundo ya Serikali za Mitaa na kuwawezesha Wananchi kupanga, kufuatilia na kutekeleza mipango yao kulingana na vipaumbele vyao. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuimarika kwa nidhamu katika matumizi ya rasilimali za Umma na kuongezeka kwa kiwango cha ruzuku kutoka Shilingi bilioni 179.6 mwaka 2000/2001 hadi Shilingi bilioni 719.5 mwaka 2007/2008. Aidha, kumekuwepo na ufanisi katika Sekta za Elimu, Maji na Afya ambapo Wananchi wameshirikishwa na hivyo, utoaji wa Huduma za Jamii umeanza kuimarika.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda mafanikio yaliyopatikana katika Awamu ya Kwanza, Serikali imeandaa Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa, Awamu ya Pili ambayo itatekelezwa katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Juni,

2013. Dira ya Programu hii ni kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kuongoza na kuwajibika katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kutoa huduma bora kwa lengo la kupunguza umaskini katika maeneo yao ya kiutawala. Lengo la Programu hii ni kupeleka Madaraka kwa Wananchi ili waweze kushiriki na kuwajibika katika maamuzi yanayohusu maendeleo yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa zimeendelea kufaidika na Mfuko wa Pamoja wa Serikali za Mitaa, ambao umesaidia kuharakisha mchakato wa maendeleo katika Serikali hizo. Mfuko huu umekuwa ukichangiwa na Wahisani tangu mwaka 2004/2005 na hadi sasa jumla ya Shilingi bilioni 111.4 zimechangwa. Kwa kuwa Mfuko huu utakoma mwaka 2013, Serikali imeanza kutafakari utaratibu endelevu wa kuugharamia kwa kufanya uchambuzi wa kitaalamu, kwa nia ya kuangalia uwezekano wa kuanzisha Mfuko kama huo ili kulinda mafanikio yaliyopatikana. Mfuko huo utasaidia kuhamasisha Wananchi Vijijini, kushiriki kwa hali na mali katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Sekta za Elimu, Afya na Barabara, ambazo kwa sehemu kubwa zinachangia moja kwa moja katika kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zenye sifa ya kupata ruzuku chini ya Mpango wa Kuzipatia Serikali za Mitaa Ruzuku ya Maendeleo na Ruzuku ya Kuzijengea Uwezo, zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kuongezeka kwa ufanisi na nidhamu katika matumizi ya fedha. Katika mwaka 2004/2005, Halmashauri zilizopimwa zilikuwa 47 na zilizofaulu kupata ruzuku zilikuwa 25. Mwaka 2005/2006, Halmashauri zilizopimwa zilikuwa 113 na zilizofaulu kupata ruzuku zilikuwa 66. Mwaka 2006/2007, Halmashauri zilizopimwa zilikuwa 121 na zilizofanikiwa kupata ruzuku zilikuwa 84. Mwaka 2007/2008, Halmashauri zilizopimwa zilikuwa 121 na Halmashauri 109 zilifanikiwa kupata ruzuku. Katika mwaka 2008/2009, jumla ya Halmashauri 127 kati ya 132 zitapata ruzuku baada ya kupimwa na kufaulu kukidhi vigezo vya kupata ruzuku ya maendeleo na kujenga uwezo. Fedha hizi zitawezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo, kuwajengea uwezo wa kitaalamu na kitaaluma Watumishi wa Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kimsingi imekubali kuboresha maslahi ya Madiwani kuhusu posho, matibabu, mazishi na unafuu wa kodi katika vyombo vya usafiri. Katika mwaka 2008/2009, jumla ya Shilingi bilioni 4.8 zimetengwa kwa ajili ya posho za Madiwani. Aidha, Serikali itaandaa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bima ya Afya utakaowawezesha Madiwani kupata matibabu kupitia Bima ya Afya. Vilevile, marekebisho ya Sheria ya Fedha yatafanyika ili Madiwani wafaidike na msamaha wa kodi kwa vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafanyika mwezi Oktoba, 2009 katika Vijiji 10,368, Mitaa 1,785 na Vitongoji 50,832. Ili kufanikisha maandalizi ya Uchaguzi huo, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 4. Shughuli kubwa zitakazofanyika katika maandalizi hayo ni pamoja na kuhakiki mipaka ya Vitongoji, Vijiji na Mitaa; kufanya mapitio ya Kanuni za Uchaguzi na kufanya Mikutano ya Mashauriano na Vyama Vya Siasa. Aidha, shughuli nyingine zitakazofanyika ni kukusanya maoni ya Wadau mbalimbali kuhusu mapendekezo ya kutumia Daftari la

Kudumu la Wapiga Kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuchapisha vitabu vya Kanuni na Fomu za Uchaguzi. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tayari mchakato wa ushirikishwaji wa Wadau umeanza na maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam ni tofauti na Majiji mengine ya Afrika Mashariki. Ndani ya Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam kuna Halmashauri za Manispaa tatu zenye Mamlaka kamili ya kutekeleza majukumu ya Mamlaka za Miji kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Namba 8 ya mwaka 1982. Uzoefu uliopatikana kwa miaka minane ya utekelezaji wa muundo mpya wa Jiji la Dar es Salaam, unaonyesha kuwa, kuna matatizo ya kiuendeshaji na hivyo kutokukidhi matarajio yaliyokusudiwa ya kutoa huduma bora kwa Wananchi. Aidha, matatizo mengine yanayolikabili Jiji la Dar es Salaam ni pamoja na miundombinu ya barabara isiyokidhi mahitaji yanayopanuka kila siku, miundombinu isiyotosheleza ya maji safi na taka na ukuaji wa jiji usioenda sambamba na utoaji huduma kwa Wananchi. Hali hii inalifanya Jiji la Dar es Salaam lisionekane kama kioo cha nchi yetu. Hivyo, kuna haja ya kuliangalia kwa namna ya pekee.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali imeunda Kamati Maalumu ya kuangalia, kuchambua na kutoa mapendekezo ya namna ya kuboresha Muundo wa Halmashauri za Dar es Salaam na uendeshaji wake ili Wananchi wafaidike na huduma bora zinazopaswa kutolewa na Mamlaka hizo za Serikali za Mitaa. Mapendekezo ya Kamati hiyo yataisaidia pia Serikali kufanya maamuzi yenye manufaa na tija kwa maombi ya Halmashauri za Majiji mengine kama vile Jiji la Mwanza ya kutaka kuwa na muundo kama wa Halmashauri za Dar es Salaam. Nazisihi Halmashauri hizo ziwe na subira.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuimarisha Mamlaka za Serikali za Mitaa hapa nchini, Serikali imefanya uamuzi wa kupanua na kuimarisha miundombinu ya Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo ili kuongeza idadi ya Wanachuo kutoka 104 hadi 2000 ifikapo mwaka 2011. Aidha, Serikali itajenga miundombinu kwa ajili ya kuhudumia mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa inayohusiana na Serikali za Mitaa, pamoja na sekta nyingine. Nia ni kukifanya Chuo hiki kiwe cha kisasa na kitovu cha mafunzo, utafiti na ushauri katika masuala yote yanayohusu Serikali za Mitaa ndani na nje ya Bara la Afrika. Upanuzi wa Chuo hiki utatekelezwa na Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa kwa udhamini wa Serikali. Hivi sasa, Mshauri Mwelekezi amepatikana na kazi ya usanifu inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2008. Ujenzi utafanywa katika awamu mbili kuanzia mwaka 2008/2009 hadi 2010/2011. Napenda kuchukua fursa hii, kuzitaka Halmashauri zote kukitumia Chuo hiki ipasavyo ili kujenga uwezo wa rasilimali watu katika Serikali za Mitaa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Shirika la Elimu Kibaha limeimarisha utoaji huduma bora kwa jamii, ikiwemo huduma za tiba na elimu ya kinga. Shirika pia liliendesha Kozi ya Uganga ya miaka mitatu kwa Maofisa Tabibu 100 na kutoa Elimu ya Malezi Bora kwa Wanafunzi 2,482. Katika mwaka 2008/2009, Shirika litaendelea kutoa huduma zake kwa ufanisi zaidi na kufanya ukarabati wa miundombinu

na majengo. Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali Maalum ya Tumbi.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali, ina jukumu la kuchapisha na kudhibiti Nyaraka muhimu za Serikali Kuu na Mitaa. Idara hiyo imekuwepo katika majengo yake ya sasa tangu mwaka 1952 huku baadhi ya mitambo yake ikiwa ni ya zamani. Kutokana na umuhimu wake, majengo ya Idara hiyo yanahitaji kukarabatiwa na baadhi ya mitambo yake kubadilishwa kuwa ya kisasa zaidi. Katika mwaka 2008/2009, Serikali imetenga Shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kuiboresha Idara kwa kuipatia mitambo ya kisasa na kuyafanyia ukarabati majengo yake. Uboreshaji huo utahusu pia Kitengo cha Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali kilichopo Dodoma. Uboreshaji wa Idara hiyo, utaiwezesha kumudu majukumu yake ya kawaida, pamoja na ya uchapishaji wa Nyaraka za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2009 na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Dodoma kama Makao Makuu ya Nchi yetu, inapaswa kuangaliwa kwa namna ya pekee na kuchukua tahadhari ili kuepuka matatizo ya ukuaji wa Mji usioendana na utoaji wa huduma muhimu. Serikali kupitia Programu ya Ustawishaji Makao Makuu, imeendelea kuiongezea Mamlaka uwezo wa kifedha ili kuboresha miundombinu ya Mji wa Dodoma. Hata hivyo, Programu hiyo imekuwa ikitekelezwa kwa takriban kipindi cha miaka 35 sasa. Hali hii inatanabahisha umuhimu wa kupitia upya Programu hii na kufanya marekebisho ya kimfumo, yatakayozingatia mabadiliko katika mazingira ya Nchi yetu kwa hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaendesha Mjadala wa Kitaifa utakaoshirikisha Wadau mbalimbali kuhusu suala la uhamishaji wa Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Baada ya Mjadala huo, Serikali itaandaa mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya kuitambua rasmi Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali. Aidha, Mamlaka itaendelea kutekeleza Programu ya Ustawishaji Makao Makuu kwa kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Mji kwa kuweka miundombinu muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali imeendelea kuweka mazingira yanayoruhusu ukuaji wa Sekta ya Habari na Mawasiliano ya kisasa. Katika kutekeleza jukumu hili, mapendekezo ya uanzishwaji wa tovuti za Mikoa yalikamilika na Tovuti 21 za Sekretarieti za Mikoa zilisajiliwa. Kukamilika kwa Tovuti hizo, kutasaidia kuboresha mawasiliano kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mikoa na Serikali Kuu. Aidha, itarahisisha utoaji huduma kwa Wananchi na kuitangaza Mikoa yetu kiuchumi Duniani. Katika mwaka 2008/2009, Serikali itakamilisha maandalizi ya maelezo ya Mikoa na Halmashauri na kuyaweka kwenye Tovuti za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na juhudi za kuiingiza Lugha ya Kiswahili katika Medani ya Kimataifa. Kiswahili kimeendelea kutumika kuwa mojawapo ya lugha ya kazi katika Umoja wa Afrika. Aidha, mchakato wa kukiwezesha kitumike katika shughuli rasmi za Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki unaendelea vizuri. Mathalan, Jumuiya ya Afrika Mashariki ipo katika

hatua za mwisho za kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, ambapo Makao Makuu ya Kamisheni hiyo yamependekezwa yawe Tanzania. Hivyo, ni vyema sasa tuanze kuitumia Lugha ya Kiswahili kama mkakati wa kuwawezesha Watanzania kupata ajira.

Tunavyozidi kuhamasisha matumizi ya Kiswahili Kimataifa, tujue pia kwamba, wanahitajika Wataalamu wengi wa kufundisha na kutafsiri katika Mikutano na Makongamano mbalimbali ya Kimataifa. Hii ni changamoto kwetu kuhakikisha kwamba, tunafundisha Kiswahili kwa ufasaha na kutumia mwanya wa kukua kwa lugha hii kama fursa ya kiuchumi. Aidha, natoa wito kwa Waandishi wa Vitabu vya Kiswahili, kuandika vitabu vingi zaidi ili waweze kuuza vitabu na kujipatia kipato. Mama wa Kiswahili ni Tanzania, sitegemei Nchi yoyote ituzidi katika kuzalisha Wataalam na vitabu vya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Mazingira kwa kuandaa Kanuni, Miongozo na viwango vya usimamizi wa Mazingira Nchini. Aidha, imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji katika Mikoa mbalimbali Nchini. Serikali pia imefanya tathmini ya Athari za Mazingira kwa miradi zaidi ya 50 na kupatiwa vyeti ili iendelee kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuratibu Mikataba ya Kimataifa kuhusu Hifadhi ya Mazingira ambayo Nchi yetu imeridhia. Uratibu wa Mikataba hiyo umewezesha Taifa letu kupata misaada ya kiufundi na fedha ili kukuza uwezo katika Hifadhi ya Mazingira. Katika mwaka 2008/2009, mkazo utawekwa katika utekelezaji wa Sera na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji na Programu mbalimbali zinazolenga Hifadhi ya Mazingira. Aidha, uratibu wa utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa inayohusu Hifadhi ya Mazingira utaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujenga uwezo wa Taifa katika kudhibiti maafa kwa kutoa mafunzo na kuuelimisha Umma kupitia Vyombo vya Habari na Vikundi vya Jamii. Katika mwaka 2007/2008, Kamati za Maafa za Mikoa mitano ya Tabora, Iringa, Ruvuma, Kilimanjaro na Rukwa, pamoja na Wilaya zake, zimepewa mafunzo ya kukabiliana na maafa. Hatua hii inafanya jumla ya Mikoa iliyopewa mafunzo hayo hadi sasa kufikia 14. Mikoa mingine ambayo tayari Kamati zake zimepewa mafunzo hayo ni Dodoma, Dar es Salaam, Singida, Mwanza, Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, na Tanga.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008/2009, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Kitaifa wa Kuimarisha Uwezo wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa kwa kutoa mafunzo kwa Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya zilizobaki na kuzijengea uwezo wa kupunguza athari za Maafa. Aidha, kazi nyingine zitakazotekelezwa chini ya Mradi huo ni kufanya tathmini ya uwezo wa Taifa kukabiliana na maafa na kujenga uwezo wa kukabiliana na maafa katika Kanda ya Ziwa, Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini, Kati na

Mashariki.  Kazi hii ya kuzijengea uwezo Kamati za Maafa, itatekelezwa kwa ushirikiano na Sekretarieti za Mikoa, Serikali za Mitaa na Asasi Zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali iliteketeza ekari 649 za bangi katika Mikoa mbalimbali Nchini.  Mikoa hiyo ni Morogoro (ekari 625), Mara (ekari 7), Tabora (7), Lindi (5.5), Mwanza (2.6), Iringa (0.75), Pwani (0.75) na Shinyanga (0.25).  Serikali kupitia Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, ilitoa elimu juu ya madhara ya Dawa za Kulevya kwa Umma na kwa makundi maalum katika jamii, wakiwemo Viongozi wa Dini 40 na Vijana walio Shuleni  na walioko nje ya Shule. Vilevile, Tume imeandaa rasimu ya Mpango wa Uelimishaji Jamii juu ya mahusiano ya matumizi ya Dawa za Kulevya na Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa Watumiaji wa Dawa za Kulevya.  Aidha, Mfumo wa Ukusanyaji, Uchambuzi na Utunzaji wa Taarifa za Dawa za Kulevya umeanzishwa ili kupata taarifa za uhakika za Dawa za Kulevya. Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2006 iliandaliwa na kuwasilishwa Bungeni na kusambazwa kwa Wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itakamilisha Sera ya Taifa ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya na kutoa elimu kuhusu athari zitokanazo na matumizi pamoja na biashara haramu ya Dawa za Kulevya. Uteketezaji wa mashamba ya kilimo cha zao haramu la bangi utaendelezwa.  Aidha, Serikali itaimarisha ushirikiano na Wadau mbalimbali wa ndani na nje katika Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Spika, Kampeni za kupambana na UKIMWI zinazoendelea kote Nchini, zinaonyesha matokeo mazuri. Uelewa wa jamii kuhusu janga hili umekuwa ukiongezeka kama inavyoshuhudiwa na kupungua kwa kiwango cha  maambukizi. Matokeo ya utafiti wa pili wa hali ya UKIMWI Nchini yaliyotolewa hivi karibuni yanaonyesha kwamba, kiwango cha maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) kimepungua kutoka wastani wa asilimia saba mwaka 2003/2004 hadi 5.8 mwaka 2007/2008.  Pamoja na mafanikio hayo, Serikali imeendelea kufanya kampeni mbalimbali za Mapambano Dhidi ya UKIMWI.  Mwezi Julai, 2007, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alizindua Kampeni ya Kitaifa ya Kupima VVU kwa hiari kwa yeye mwenyewe kupima VVU hadharani.

Kampeni hii imekuwa ya mafanikio makubwa kwani hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2008, watu wapatao 4,042,055 walijitokeza kupimwa VVU, ukilinganisha na watu 2,000,000 waliowahi kupimwa katika kipindi cha miaka 13 kuanzia mwaka 1995 wakati huduma  hii ilipoanza kutolewa hapa Nchini.  Kati ya watu 4,042,055 waliopimwa, Wanawake walikuwa 2,257,052 na Wanaume walikuwa 1,785,003. Jumla ya watu 194,149 waligunduliwa wameambukizwa Virusi vya UKIMWI wakiwepo Wanaume 76,895 na Wanawake 117,254.  Idadi hii inaonyesha kuwa, asilimia 4.8 ya watu wote waliopima, walikuwa na  maambukizi ya virusi vya UKIMWI.  Napenda kuwakumbusha Watanzania kwamba, kupima afya ni jambo muhimu na hivyo wajitokeze zaidi ili kufahamu hali ya afya zao.  Aidha, Kampeni hii iendelezwe ili iwe ni zoezi la kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2007/2008, fedha zilizotolewa na Serikali na Wahisani kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI ziliongezeka na kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 596.4, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 310.6 zilizotolewa mwaka 2006/2007. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 92. Ongezeko hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na rasilimali kutoka *Global Fund* na Serikali ya Marekani. Vilevile, uboreshaji wa shughuli za UKIMWI kwa kushirikiana na Nchi jirani kama Nchi za Maziwa Makuu, Nchi za *SADC* na Nchi za Afrika ya Mashariki ni moja ya mambo ambayo yameleta mafanikio kwa Nchi yetu kupata uzoefu wa mbinu mbalimbali za kuboresha Programu zetu. Mpango wa Uboreshaji na Ubadilishaji wa Tabia ambao uliandaliwa mwaka huu, umekuwa ni nyenzo kubwa ambayo hutumiwa na watekelezaji mbalimbali Nchini. Vilevile, Serikali imewezesha Sekta mbalimbali kufanya UKIMWI uwe ni sehemu ya shughuli za kila siku kupitia Miongozo mbalimbali inayotolewa kwa shughuli za UKIMWI. Tumeweza pia kuboresha Elimu ya UKIMWI kwa Umma kwa kupitia Maonyesho ya Sinema Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008/2009, Serikali itafanya mapitio ya Sera na Muundo wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Serikali pia itahamasisha Wadau katika ngazi zote Nchini, kuielewa Sheria ya Kudhibiti UKIMWI ya Mwaka 2007. Aidha, itaongeza juhudi za udhibiti wa UKIMWI katika kinga kwa kuwa asilimia 95 ya Wananchi bado hawajaambukizwa. Vilevile, Magari zaidi ya Sinema yatanunuliwa kwa ajili ya maeneo ya Vijijini. Mfuko Maalum wa Fedha wa kuhudumia shughuli za udhibiti wa UKIMWI utaanzishwa kisheria. Aidha, Serikali itaboresha shughuli za udhibiti wa UKIMWI kwa kutumia mfumo shirikishi ili kuifikia jamii kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ilishiriki katika Kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, kilichofanyika Mjini Addis Ababa, Ethiopia kuanzia tarehe 31 Januari hadi tarehe 2 Februari, 2008. Katika Kikao hicho, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alichaguliwa kwa kauli moja kuwa Mwenyekiti wa Umoja huo, kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hili ni tukio la heshima kubwa na kielelezo cha imani na upendo, ambao Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika wanao kwa Uongozi wa Nchi yetu. Heshima hiyo imeongeza wajibu wetu katika kushughulikia changamoto zinazolikabili Bara la Afrika katika nyanja za ushirikiano, kuimarisha uchumi na kuondoa umaskini, pamoja na kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa migogoro inayoendelea katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi, inayolenga kutoa changamoto za kiutendaji katika Balozi zetu, kuhamasisha Utalii, Uwekezaji, Kuvutia Mitaji na Kukuza Mauzo Nje. Ushirikiano wa Kimataifa umeimarishwa kwa Viongozi wa Serikali na Wafanyabiashara wa ndani kufanya ziara na kushiriki katika Makongamano ya Kimataifa kwa lengo la kuitangaza Tanzania na kuwahamasisha Wawekezaji kuwekeza Nchini. Tarehe 2 – 6 Juni, 2008, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nane wa *Leon Sullivan* ulioshirikisha zaidi ya watu 4,000 kutoka Nchi mbalimbali Duniani. Mkutano huo uliwapa nafasi Wageni hao kufahamu fursa mbalimbali za Uwekezaji zilizopo Nchini na vivutio mbalimbali vya utalii. Aidha, waliweza kubadilishana mawazo na Wafanyabiashara wa Tanzania. Nitumie fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanikisha kufanyika kwa

Mkutano huu wa kihistoria. Pia nawapongeza Washiriki wote walioweza kuhudhuria Mkutano huu muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Viongozi wa Kitaifa wametumia ziara za nje kuimarisha mahusiano kati ya Nchi yetu na Nchi marafiki. Ziara hizo zimekuwa na mafanikio makubwa ambapo Nchi hizo zimetoa misaada mbalimbali itakayosaidia katika juhudi zetu za kukuza uchumi. Kwa mfano, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, iliahidi kufuta madeni yote ambayo Nchi hiyo inaidai Tanzania. Aidha, iliahidi kufufua miradi yote iliyoanzishwa miaka ya sitini na sabini, hususan Reli ya Tanzania na Zambia, Kiwanda cha Urafiki kati ya Tanzania na China na Kiwanda cha Zana za Kilimo cha Ubungo. Pia, imeahidi kuisaidia Tanzania katika ujenzi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba hii nimezungumzia mambo mengi ambayo Serikali imefanya kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 na mwelekeo wa kazi zitakazofanyika katika mwaka 2008/2009. Napenda kuhitimisha Hotuba hii kwa kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Tunalo jukumu kubwa mbele yetu la kusimamia utekelezaji wa MKUKUTA. Fedha zinazoombwa katika Bajeti hii ni kwa ajili ya kutekeleza malengo ya MKUKUTA. Tusimamie vizuri matumizi ya fedha hizi ili kutimiza malengo tuliyojiwekea. Naelewa kwamba, fedha zilizotengwa haziwezi kutosheleza mahitaji yetu yote, ila tukitumia fedha za Serikali kwa umakini na kuhakikisha zinazalisha zaidi, miaka ijayo tutakuwa na vianzio vingi zaidi vya mapato. Hiki kidogo tulichonacho, tusikitumie kama yule Mtumwa aliyepewa Talanta moja na tajiri yake na kuifukia. Tuwe Watumwa werevu na tuwekeze ili izae zaidi. *(Makofi)*

(b) Tunayo changamoto ya kulinda ukuaji wa uchumi wetu licha ya athari za kupanda kwa bei ya nafaka, mafuta ya petroli, pamoja na bidhaa nyingine kutoka nje. Sote kwa pamoja, tunao wajibu wa kufanya kazi kwa bidii, tuongeze uzalishaji ili uchumi wetu usitetereke. Kupanda kwa bei ya nafaka iwe ni changamoto kwetu ya kuzalisha zaidi na kuuza ziada nje.

(c) Tumejiwekea utaratibu mzuri wa kuwawezesha Wananchi kujikomboa kiuchumi. Tutumie nafasi hii, kuwahimiza Wananchi kubuni shughuli za uzalishaji na miradi midogo midogo inayokopesheka katika vikundi. Fursa za Wananchi kupata mikopo ni nyingi, tuwahimize kukopa na kurejesha mikopo kwa wakati.

(d) Kilimo bado ni msingi wa Uchumi wa Taifa letu; tuhimize Wananchi hususan Vijana kupenda kilimo. Aidha, tuwahimize kutumia pembejeo zikiwemo mbolea na mbegu bora ili kuongeza tija katika uzalishaji. Mbolea itakayonunuliwa kwa njia ya ruzuku isimamiwe vyema iwafikie Wakulima kwa wakati na kwa bei nafuu. Lengo la kutoa ruzuku si kufaidisha Wafanyabiashara bali Wakulima. Nisingependa kusikia malalamiko kwamba, mbolea ya ruzuku haikuwafikia Wakulima au inafika kwa bei ya juu. Serikali haitamvumilia mtu yeyote atakayezembea katika usimamizi wa mbolea. Narudia tena, mbolea iwafikie wahusika na kwa bei inayolengwa.

(e) Wakati umefika wa kutumia hazina ya ardhi tuliyonayo kwa kuwaelimisha Wananchi kuhusu Matumizi Bora ya Ardhi. Aidha, tuwakumbushe kuepukana na migogoro ya ardhi kwa kufuata Kanuni na Taratibu za Sheria za Ardhi zilizopo. Tujiepushe na dhana ya uvamizi wa maeneo ambayo tayari yametengwa kwa ajili ya maendeleo ya shughuli nyingine kwa manufaa ya Taifa.

(f) Suala la elimu halina mjadala; tuendelee kuhimiza Wananchi kuthamini elimu kwa ajili ya Watoto wetu. Tuongeze juhudi kujenga miundombinu ya kutosha kwa ajili ya elimu kwa wote kuanzia ngazi ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa Bajeti hii ni vyema Watumishi wote wa Serikali wawajibike ipasavyo na wahakikishe kwamba, fedha zilizotengwa kwenye Bajeti ya Serikali zinatumika kwa shughuli zilizopangwa.

Kila Mtumishi anapaswa kupima kazi yake kwa kujiuliza ametoa mchango gani wa majukumu yake katika kuchangia kwenye Bajeti hii. Tusikubali watu wachache watumie fedha hizi kiujanja. Tuwabaini na kuwadhibiti.

Naagiza Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri, kuhakikisha kwamba, Watumishi wote wanafanya kazi kwa malengo, tija na ufanisi. Tukifanya kazi kwa bidii na uadilifu, tutasonga mbele haraka na kuleta maendeleo endelevu Nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza, napenda kuwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wote, kwa ushauri wao ambao umewawezesha Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, kutekeleza majukumu yao ya Kitaifa kwa ufanisi.

Aidha, nawashukuru Wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana Phillemon Luhanjo, pamoja na Vyombo vyote vya Dola kwa kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuiwezesha kukamilisha maandalizi yote ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2008/2009, pamoja na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya kila Wizara, Mikoa na Taasisi zinazojitegemea.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kuwashukuru sana Mheshimiwa Phillip Sang'ka Marmo, Mbunge wa Mbulu, Waziri wa Nchi (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Mbunge wa Ulanga Mashariki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa msaada mkubwa na ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Nawashukuru vilevile Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya Uongozi wa Makatibu Wakuu; Bwana Vincent Mrisho na Bibi Maimuna Tarishi na Naibu Makatibu Wakuu; Bwana Andrew Nyumayo na Bwana Fanuel Mbonde, kwa ushauri wao wa kitaalam ambao wamenipa katika kipindi hiki cha mwanzo katika uongozi wangu. Nawashukuru kwa kukamilisha maandalizi yote ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Nchi yetu imepata misaada na mikopo kutoka kwa Wahisani wetu mbalimbali. Misaada na mikopo hiyo imetoka kwa Nchi rafiki, Nchi Wafadhili, Taasisi za Fedha Duniani, Mashirika ya Umma, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mifuko Mbalimbali Duniani, Madhehebu ya Dini na Mashirika Yasiyo ya Serikali.

Misaada na mikopo hiyo, imechangia sana katika kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

Napenda kuwashukuru wote kwa dhati na kuwahakikishia kuwa, Watanzania tunathamini misaada na mikopo yao na tutaendelea kushirikiana nao katika harakati za maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala Za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mfuko wa Bunge ya Mwaka 2008/2009: Kwa mwaka 2008/2009, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 56,088,806,800, kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo.

Aidha, jumla ya Shilingi 52,911,351,100 zinaombwa kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 10,939,357,000 ni fedha za Ndani na Shilingi 41,971,994,100 ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008/2009, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zake, inaombewa jumla ya Shilingi 93,728,168,000 kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo.

Aidha, jumla ya Shilingi 73,058,705,100 ni kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 32,124,465,000 ni fedha za Ndani na Shilingi 40,934,240,100 ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaombewa jumla ya Shilingi 90,360,780,000 kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo na Shilingi 32,917,762,000 kwa ajili ya Mpango ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 29,947,762,000 ni fedha za Ndani na Shilingi 2,970,000,000 ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji zinaombewa jumla ya Shilingi 908,998,074,000 kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo na Shilingi 356,775,647,000 kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 32,180,000,000 ni fedha za Ndani na Shilingi 324,595,647,000 ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge unaombewa jumla ya Shilingi 48,404,985,000 kwa ajili Mishahara na Matumizi Mengineyo na Shilingi 9,037,505,900 kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 8,670,273,000 ni fedha za Ndani na Shilingi 367,232,900 ni fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2008/2009 ya jumla ya Shilingi 1,664,839,294,000 kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu na jumla ya Shilingi 57,442,490,900 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Hotuba hii, yapo Majedwali mbalimbali ambayo yanafafanua kwa kina zaidi, Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake ikiwemo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Bwana mmoja alipoulizwa: *What is a Budget?* Alijibu: *It is an orderly system for living beyond your means".* Akimaanisha kwamba, Bajeti ni mpangilio wa kuishi nje ya uwezo wako*."* Sisi tunasema *"It is an orderly system for living within our means"* kwamba ni mpangilio mzuri wa kuishi ndani ya uwezo tulionao*."*

Tunaomba tuidhinishiwe fedha hizo ili tuweze kuendeleza yote ambayo tumepanga ndani ya uwezo wetu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakumbushe tu kwamba, Mheshimiwa Waziri ameisoma hotuba yake hiyo aliyodai ni fupi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(6): "Isipokuwa kwa Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, muda wa Waziri anayewasilisha Hotuba ya Makadirio ya Wizara yake, utakuwa ni dakika zisizozidi 60."

Kwa hiyo, yeye ni *exception*. Sasa kwa mantiki hiyo hiyo, kwa sababu mtaona kwamba, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inachanganya zilizokuwa Wizara mbili; yaani Waziri Mkuu *proper* na TAMISEMI na ndiyo maana inakuwa hotuba nzito namna

hii. Kwa hiyo, nilikubaliana na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa sekta hiyo kwamba, kwa kutumia mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni ya pili, yanayonipa uwezo wa kutafsiri kwa busara mambo mbalimbali, sasa nimeitafsiri Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sawa sawa na hotuba mbili kwa maana sasa ya Kanuni ambayo inazuia hao niliowataja wasizidi dakika 30. Kwa hiyo, watazidi hivyo.

Kwa kuzingatia hali ya muda uliopo, itanibidi nitoe tangazo la kusitisha. Kabla sijafanya hivyo, napenda kuwaarifu kwamba, sasa itanibidi nifunge orodha. Walioomba kuchangia hadi sasa ni 102. Inawezekana tukapata nafasi ya 90 kwa kuhesabu kwamba, tuna wastani wa 22 kwa siku na hata hiyo itakuwa ngumu, labda 80.

Kwa hiyo, nikiendelea kupokea maombi ya kuchangia itakuwa si sahihi na pia mkumbuke kuna majedwali ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nilidhani basi kwa kuzingatia hoja zote hizo ni sahihi, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 06.31 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 - Ofisi ya Waziri Mkuu

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama alivyotangaza Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ina wachangiaji wengi sana. Mpaka sasa wamefikia wachangiaji 105, wamezidi hata ile hotuba nyingine, mara mbili ya ile hotuba ya kwanza. Kama mnavyofahamu, siku ya tano katika hotuba hii, tutaingia kwenye kifungu baada ya kifungu. Kwa hiyo, inabidi muda uwe mrefu sana kuingia kwenye vifungu kwa sababu ana Fungu la Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu la *TAMISEMI*, Fungu la Tume ya Uchaguzi na Tume zingine. Kwa hiyo, siku ni chache zaidi kuliko zile za bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tunapoingia katika kufanya kazi hii, tutatumia Kanuni ya 60(5) ambayo inasema:-

*“Endapo maombi ya kuchangia hoja fulani yatakuwa mengi zaidi ya muda kwa hoja hiyo, Spika atatoa nafasi ya kwanza kwa Wabunge ambao:-*

*(a) hawajachangia katika hoja zilizotangulia kujadiliwa katika Mkutano unaoendelea, kwa sasa ni bajeti ya Fedha au;*

*(b) wamechangia mara chache.”*

Waheshimiwa Wabunge, ukiendelea Kifungu 60(6) kinasema:-

*“Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya (5) ya Kanuni hii, Spika atahakikisha kuwa, nafasi za kuchangia zinatolewa kwa uwiano unaofaa baina ya aina zote za Wabunge walioomba kuchangia hoja hiyo”.*

Kwa maana hiyo ni kwamba kutakuwepo na nafasi kwa akina mama, kutoka Zanzibar, kutoka Upinzani na hata Chama Tawala. Kwa hiyo, kama wewe unakuta mpangilio wako hauendi sawasawa, sababu ni hizo nilizozisema hapo juu.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi tulikuwa hatujasikiliza msemaji wa Kamati inayohusika pia Kambi ya Upinzani na kila kundi litapewa saa moja moja. Tunaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Katiba, Mheshimiwa Lubeleje.

Waheshimiwa Wabunge, naona siku hizi, Kamati wanachapisha vitabu vyao, haya ni maendeleo, hongera sana Kamati zote. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7), Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa mwaka wa Fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009: Fungu 25 - Waziri Mkuu, Fungu 27 - Msajili wa Vyama vya Siasa, Fungu 37- Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 42 - Mfuko wa Bunge, Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu 91 - Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Fungu 92-Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawasilisha taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (*TAMISEMI*), kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, kwa Fungu 56 Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI* na Mafungu 70-89 na 95 kwa ajili ya Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Utaratibu na Bunge, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi. Baada ya kuiletea Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kazi ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2008/2009, tarehe 5 Juni, 2008, Kamati ilikutana katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam na kupokea maelezo ya muhtasari

wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa mwaka wa Fedha 2008/2009. Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo na mafungu yake kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa Fedha 2007/2008, Fungu 25 – Waziri Mkuu na 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2007/2008, Kamati ilielezwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ilitekeleza shughuli mbalimbali. Baadhi ya shughuli ambazo zilifanyika ni pamoja na kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo mikoani, kukutana na wananchi na kutoa maelekezo kwa watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, baadhi ya shughuli zilizofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37 ni pamoja na kuzijengea uwezo Kamati za Maafa za Mikoa ya Tabora, Iringa, Ruvuma na Rukwa, kwa kutoa mafunzo kukabiliana na maafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu litakumbuka kuwa katika mwaka wa fedha 2006/2007, baadhi ya Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, yakiwemo Mafungu 37 na 61, yalipunguzwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu iliyoharibiwa na mvua. Kwa hiyo, suala la kuzijengea uwezo Kamati za Maafa kwa ujumla ni muhimu sana hasa tukizingatia kuwa nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na majanga ya ukame, njaa, mafuriko na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 42 - Mfuko wa Bunge, katika kipindi kilichopita, ilielezwa kuwa Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya Sh.42,406,423,000/= zilizowezesha kufanyika kwa mikutano minne ya Bunge ambayo ilichambua kikamilifu masuala ya Kitaifa na kusimamia utendaji wa Serikali. Aidha, ilielezwa kwamba Kamati za Bunge zilikutana kama ilivyopangwa na kufanya ziara maeneo mbalimbali kwa nia ya kufuatilia utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kusimamia Serikali ni la kikatiba ambalo limeainishwa katika Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa kwa pamoja na Ibara za 89 na 96 za Katiba zinazolipa mamlaka Bunge kutunga Kanuni na kuunda Kamati zake ambazo hufanya kazi kwa niaba ya Bunge. Kwa mantiki hiyo, ziara za Kamati kukagua miradi ya maendeleo Mikoani au katika taasisi inazozisimamia, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, sinabudi nikiri kuwa si Kamati zote zilizopata fursa hiyo kwa kutumia Fungu 42. Hili ni mojawapo kati ya maeneo ambayo Kamati za Bunge zimekuwa zikipigania kila mara ili ziweze kufuatilia utendaji wa vyombo vinavyohusika kujionea hali halisi kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kuwa tangu Kamati yangu iundwe mwaka 2003, ukiacha ziara fupi ilizowahi kufanya katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, haijawahi kufanya ziara ndefu Mikoani, kukagua miradi inayotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu hususan katika Mikoa ambayo katika

muda mfupi ujao Bunge lako Tukufu litaidhinisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Mafungu mengineyo, katika kipindi kilichopita, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ilitekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo chaguzi ndogo za Madiwani na Mbunge. Nyingine, uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura na kutoa elimu kwa wanachi kuhusu daftari hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa Fungu 91 – Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, iletekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa Sera ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, kutoa mafunzo na taarifa kwa umma kuhusu athari za dawa za kulevya na kufanya utafiti kuhusu rushwa katika mchakato mzima wa udhibiti wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zilizotekelezwa na Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI ni pamoja na kuanda miongozo kuhusu UKIMWI na maandalizi ya Mkakati wa Kudhibiti UKIMWI 2008 – 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha uliopita, Kamati ilipokea maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, yakiwemo matarajio ya mapato na Mpango wa Maendeleo. Aidha, Kamati ilifahamishwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka huo.

Mwisho, Kamati iliombwa kupitisha jumla ya shilingi 167,003,291,830, kati ya fedha hizo shilingi 62,509,500,030 ni fedha za maendeleo na shilingi 104,493,791,800, matumizi ya kawaida, mishahara na ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Mwaka 2008/2009, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Kamati ilitoa ushauri na maoni juu ya Maafa, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)*, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Kudhibiti Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupokea maombi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati ilijadili kwa kina shughuli mbalimbali zilizopangwa kufanyika kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa sasa hivi kumekuwepo na ongezeko la ghafla la bei ya mafuta ambalo licha ya kuwa linatokana na ongezeko la biashara hiyo katika soko la dunia, lakini bado wapo wafanyabiashara wachache wanaotumia fursa hiyo kupandisha bei ya bidhaa hiyo kiholela na hivyo kusababisha gharama za maisha kupanda.

Kwa mantiki hiyo, mbali ya kuwepo kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (*EWURA*), Ofisi ya Waziri Mkuu iangalie namna itakavyoweza kuingilia kati kudhibiti ongezeko la mara kwa mara la mafuta linalosababisha kupanda maradufu kwa mahitaji muhimu ya wananchi kama vile vyakula, vifaa vya ujenzi na kadhalika ili kuwaondolea mzigo wananchi.

Aidha, kwa kuwa Bunge lilipitisha Sheria inayoiruhusu Tanzania *Petroleum Development Company (TPDC)* kuagiza mafuta, Serikali isimamie utekelezaji wa Sheria hiyo ili wananchi wengi waweze kupata fursa ya kutumia mafuta yatakayoagizwa na *TPDC.*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majanga ya Kitaifa na Maafa mengine ni kwamba kama tunavyofahamu, nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na majanga mbalimbali ya kitaifa yanayowasabishia wananchi madhara mbalimbali yakiwemo magonjwa, vifo, mafuriko, njaa na kadhalika.

Kamati yangu inafahamu kazi nzuri inayofanywa na Kitengo cha Maafa. Pamoja na hayo, Kamati inashauri kuwa wigo wa kushughulikia maafa upanuliwe zaidi na kuhusisha majanga mengine kama vile ajali barabarani, majini na kadhalika kwa kutafuta njia za kuzuia majanga hayo yasitokee badala ya kungojea yatokee kwani kinga ni bora kuliko tiba.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la hali ya chakula nchini ni kwamba, katika vipindi vilivyopita, tumeona jinsi Taifa lilivyokuwa likitumia rasilimali nyingi kukabiliana na tatizo la njaa baada ya nchi yetu kukumbwa na ukame. Ukame ambao siyo tu ulisababisha upungufu wa chakula bali ulisababisha Taifa likumbwe na tatizo la umeme baada ya vyanzo vya maji kupungua na hivyo kusababisha gharama za maisha kupanda maradufu.

Kutokana na uzoefu ambao tumeupata, Kamati inashauri kuwa Serikali itathmini hali halisi ya chakula nchini na kuangalia maeneo yote yenye upungufu ili juhudi za kukabiliana na upungufu huo zifanyike mapema. Kamati inatoa ushauri huo kwa kuzingatia ukubwa wa Tanzania na matatizo ya miundombinu ya mawasiliano na barabara ambayo wakati mwingine huifanya Serikali ichelewe kupata taarifa za vijiji vinavyokumbwa na balaa la njaa kwa wakati muafaka.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la vijana kujihusisha na madawa ya kulevya ni kwamba, katika Miji mingi nchini hususan Dar es Salaam na Zanzibar, kuna ongezeko kubwa la vijana, wanaojulikana kwa jina la ‘*Mateja’* wakijihusisha na madawa ya kulevya. Vijana hawa ambao huwa na *vijiwe* vyao, siyo tu wanahatarisha maisha yao binafsi, bali pia wanahatarisha mustakabali wa Taifa na kuangamiza nguvu kazi ya kesho ikizingatiwa kuwa madawa hayo huwasababishia madhara mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupoteza uwezo wao wa kufikiri na kusababisha maambukizo ya Ukimwi.

Kutokana na hoja hizo, Kamati inashauri kuwa elimu ya madawa ya kulevya iwekwe kwenye silabasi za shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kuwaelimisha vijana wetu madhara ya madawa hayo. Kwa kufanya hivyo, Kamati inaamini kuwa tutawaokoa vijana wetu kujiingiza katika vitendo hivyo viovu.

Pamoja na hayo, Serikali iendelee kudhibiti biashara ya madawa ya kulevya na kuhakikisha kuwa inasimamia kikamilifu utekelezaji wa sheria zinazohusiana na madawa hayo.

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa kasi ya kuhamia Dodoma imepungua kutokana na ufinyu wa bajeti, sote tutakiri kuwa Manispaa ya Dodoma kwa hivi sasa inapanuka. Ongezeko kubwa la ujenzi wa nyumba, vyuo vikuu, kikiwemo Chuo Kikuu cha Dodoma, kumeifanya manispaa hiyo kuvutia wawekezaji wadogo na wa kati kuwekeza katika manispaa hiyo.

Pamoja na hayo, zipo dalili zilizoanza kujitokeza kuwa panapokuwepo mikutano ya Kitaifa kama vile ya Bunge na mikutano mikuu ya Vyama vya siasa, hujitokeza misongamano ya ghafla ya magari kwenye baadhi ya barabara za Manispaa hususan barabara ya Dar es Salaam na barabara ya mtaa wa Kuu.

Kutokana na dalili hizo, Kamati inashauri kuwa Serikali iimarishe na kupanua miundombinu iliyopo kumudu ongezeko la watu na magari kwa siku za usoni kuepukana na adha ya msongamano wa magari na watu kama inayojitokeza hivi sasa katika jiji la Dar es Salaam. Tusipofanya hivyo, kuna wakati Manispaa hiyo inaweza ikajikuta ikifuata utaratibu wa njia tatu.

(f) Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(Constituency Development Fund),* itakumbukwa Bunge hili kupitia vyombo mbalimbali na Waheshimiwa Wabunge wenyewe wametoa mapendekezo ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*Consituency Development Fund),* kwa lengo la kuwawezesha Wabunge kuwa na Mfuko Maalumu wa Maendeleo katika maeneo yao. Hii ni kufuatia matatizo mbalimbali yanayowakabili katika kutekeleza majukumu yao ya uwakilishi. Pamoja na mchakato unaoendelea kuhusu Mfuko huo, Kamati inasisitiza kuwa juhudi za kuushughulikia ziendelee na kama imeshindikana Bunge hili lifahamishwe ili liweze kufikiria njia mbadala.

(g) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *The National Assembly (Adminstration) Bill*, 2008, itakumbukwa pia katika Mkutano huu, pamoja na mambo mengine, Bunge litashughulikia pia Muswada wa Sheria ya "*The National Assembly (Administration) Bill"* wa Mwaka 2008. Muswada huo uliahidiwa kuwa ungeletwa kwa hati ya dharura. Kwa kuwa hadi sasa haujaletwa, Kamati inaikumbusha Serikali kuuleta na kama kuna tatizo basi Bunge hili lifahamishwe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa niruhusu nizungumzie maoni ya Kamati yangu, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kama nilivyodokeza hapo mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kazi ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilifanyika tarehe 3 - 4 Juni, 2008 katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam.

Kama ilivyo ada, tarehe 3 Juni, 2008, Kamati ilipokea maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2008/2009. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, akisaidiwa na Mheshimiwa Aggrey Mwanri (Mb), Naibu Waziri.

Aidha, baada ya maelezo hayo, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa kwa Mikoa kwa mwaka wa fedha uliopita na makadirio ya mapato na matumizi ya Mikoa kwa mwaka 2008/2009 kwa Mafungu 70 - 89 na 95 yaliyowasilishwa na Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitengewa jumla ya Sh.89,362,431,000/= kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo, ruzuku za Taasisi na Mfuko wa Barabara.

Aidha, Ofisi hiyo ilitengewa jumla ya Sh.27,903,399,000/= kwa ajili ya kugharimia programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI* na Sh.58,452,260,500/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipokea taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na mafanikio na changamoto mbalimbali zilizojitokeza. Lakini kabla sijataja maeneo machache ya shughuli zilizotekelezwa, napenda nitumie fursa hii kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI*, kwa kufanikisha majukumu yaliyopangwa licha ya ufinyu wa bajeti ambao umejitokeza katika Mafungu 56, 70 - 89 na 95.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika usimamizi na utunzaji wa fedha za Halmashauri, itakumbukwa kuwa kati ya maeneo ambayo yamekuwa yakisimamiwa na Bunge lako Tukufu na kutolewa ushauri wa kina kupitia Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati hii, ni utunzaji wa hesabu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka kadhaa, utunzaji wa hesabu katika Halmashauri ulikuwa wa kiwango cha chini na matokeo yake kwa mujibu wa taarifa mbalimbali za Ukaguzi, Halmashauri nyingi zilikuwa zikipata hati chafu. Hii ilitokana, pamoja na mambo mengine, baadhi ya watendaji kutozingatia Kanuni na Sheria za matumizi ya fedha za umma, kwa upande mmoja na kwa upande mwingine, baadhi ya Wahasibu katika Halmashauri hizo kukosa sifa zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kazi nzuri zinazofanywa na Kamati za Bunge na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Serikali ilijitahidi kuziba upungufu wa watumishi kwa kuajiri watumishi wapya katika Mikoa na Halmashauri na kuwapeleka wataalamu wa fani mbalimbali kwenye Halmashauri kwa ajili ya kuleta ufanisi.

Aidha, katika kipindi hicho, Halmashauri nyingi ziliboresha usimamizi na utunzaji wa hesabu zao na kupunguza hoja za ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kwako, naomba nichukue fursa hii kuipongeza Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa kazi nzuri inayofanya katika kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kwa mujibu wa sheria za nchi.

Pia napenda nimpongeze Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kutekeleza wajibu wake.

Aidha, naipongeza Serikali na Halmashauri zote kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na vyombo vinavyohusika na kuboresha usimamizi na utunzaji wa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kilichopita, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pia iliendelea na ukarabati na ujenzi wa nyumba na Ofisi za Wakuu wa Wilaya, vituo vya kutolea huduma za afya, majengo ya shule za msingi na sekondari na ukarabati wa hospitali za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nawasilisha Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Mwaka 2006, pamoja na mambo mengine, nilieleza kuwa Kamati yangu kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), ilikagua miradi ya *TASAF* katika Visiwa vya Unguja na Pemba na Mkoa wa Tanga kati ya tarehe 23-26 Mei, 2006.

Aidha, tarehe 18-26 Januari, 2007 ilikagua miradi ya aina hiyo katika Mikoa ya Iringa na Ruvuma na tarehe 3 – 10 Oktoba, 2007, Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara hizo, Kamati ilijionea na kufurahishwa na miradi iliyohusisha nguvu za wananchi ikiwemo miradi ya ujenzi wa shule za msingi, sekondari na zahanati. Kwa kuzingatia kuwepo kwa shughuli mbalimbali zilizofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI* katika eneo hili na kwa kuzingatia kazi nzuri iliyofanywa na *TASAF*, Kamati inashauri kuwa *TAMISEMI* ishirikiane na *TASAF* na kujifunza mbinu inazotumia katika uhamasishaji wa miradi ya wananchi ili iweze kuzitumia katika ujenzi wa shule, zahanati na miradi mingineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mbinu hizo ni kuzishirikisha Halmashauri zenyewe na wananchi kuibua miradi kwa kutumia fedha za ndani *(own source).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha uliopita, Mikoa nayo ilitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Mkoa wa Manyara (Fungu 95), ulitenga jumla ya Sh.885,000,000/= kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuweka umeme na maji.

Aidha, kwa mwaka 2008/2009, umeomba jumla ya Sh.176,000,000/= kwa ajili ya kukamilisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, kufanya *landscaping* pamoja na kukamilisha kazi nyingine ndogo. Taarifa ambazo Kamati hii imezipata zinaonyesha kuwa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, pamoja na kwamba halijakamilika, ni jengo la kisasa na linalovutia.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Mkoa wa Kagera – Fungu 87, pamoja na shughuli nyingine za maendeleo, ulitekeleza ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa. Kwa mwaka wa Fedha 2008/2009, Mkoa umeomba Sh.22,946,136,000/= kwa ajili ya fedha za maendeleo. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambayo kwa taarifa tambazo Kamati imezipata, jengo la ofisi hiyo lilijengwa mwaka 1950.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2007/2008, Mkoa wa Dodoma uliidhinishiwa jumla ya Sh.1,971,100,000/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, ukiwemo ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Wilaya, ukarabati wa nyumba ya Katibu Tawala wa Mkoa, ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya na kadhalika.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Mkoa wa Pwani, Fungu 71, uliidhinishwa jumla ya Sh.16,484,366,500/= kwa ajili ya fedha za maendeleo. Fedha hizo zilitumika, pamoja na shughuli nyingine, kukarabati jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, kazi ambayo ilianza kufanyika tangu mwaka wa fedha 2000/2001. Kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, kiasi kilichotolewa kilikuwa ni Sh.88,300,000/= ambazo zilizitumika kuimarisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Mwaka 2008/2009 Sh.78,000,000/= zinaombwa kukamilisha ujenzi wa uzio wa tofali na grili katika jengo la Mkuu wa Mkoa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ambazo Kamati hii imepokea, zinaonyesha kuwa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, lilikuwa katika hali mbaya na hivyo kuhitaji matengenezo makubwa.

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, shughuli ambazo zilifanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Fungu 86, ni pamoja na ukarabati wa majengo likiwemo jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambalo ukarabati wake ulianza tangu mwaka wa fedha 2002/2003. Kwa mujibu wa taarifa ambazo Kamati imezipata, jengo hilo lilikuwa mali ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC*).

Katika mwaka wa fedha 2008/2009, fedha zinazoombwa kwa ajili ya miradi ya Mkoa ni Sh.20,518,262,000/= zikiwemo Sh.100,000,000/= kwa ajili ya kuimarisha jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Shughuli nyingine ni ukarabati wa majengo ya Serikali, ukarabati wa hospitali ya Mkoa (Bombo), ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo Mikoa mingine, Mkoa wa Mara, nao ulitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ukiwemo mradi wa ukarabati wa nyumba za Serikali. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2006/2007, jumla ya Sh.59,800,000/= zilipangwa kutumika katika kukarabati Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Aidha, kwa mwaka 2007/2008, jumla ya Sh.90,000,000/= zilitumika kati ya Sh.140,000,000/= zilizotolewa. Tathmini ya jumla ya bajeti kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeelezea kwa muhtasari mafanikio na changamoto ambazo Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilikabiliana nazo katika kipindi kilichopita kwa kutoa mifano michache ya miradi iliyotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Mikoa ya Pwani, Manyara, Kagera, Tanga, Dodoma na Mara. Hata hivyo, tathminini ya jumla ya Mikoa yote ambayo Kamati hii imepata fursa ya kuipitia, inaonyesha kuwa takriban kila Mkoa uliomba na kuidhinishiwa fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Serikali, zikiwemo Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya, nyumba za watumishi wa Serikali, Hospitali za Mikoa na Wilaya na kadhalika.

Aidha, Kamati imebaini kuwa majengo mengi ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa yalirithiwa kutoka ofisi za taasisi nyingine na kusababisha yafanyiwe ukarabati wa mara kwa mara. Pamoja na hayo, tatizo la ufinyu wa bajeti ni moja kati ya changamoto kubwa inayokwamisha utekelezaji wa miradi iliyopo katika Mafungu 56, 70 - 89 na 95.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009, mbali ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2007/2008, pia Kamati ilifahamishwa juu ya kazi mbalimbali zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mikoa na Halmashauri.

Mwisho Kamati iliombwa ipitishe jumla ya Sh.1,555,839,136,100.00, kati ya fedha hizo Sh.743,303,552,000/= ni mishahara, Sh.349,783,470,000/=, Matumizi Mengineyo na Sh.462,752,114,100/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maombi hayo ambayo hatimaye Kamati iliyapitisha, naomba niwasilishe Maoni na Ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na 2008/2009. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo tisa. Maoni hayo yalihusu ruzuku ya pembejeo ya kilimo, Mpango wa Elimu ya Sekondari (MMES), Manispaa ya Dodoma, Manispaa ya Temeke,

Ilala, Kinondoni na Jiji la Dar es Salaam, uendeshaji wa Shirika la Masoko la Kariakoo, mgawanyo wa rasilimali za maendeleo katika Mikoa, upunguzaji wa msongamano wa magari Dar es Salaam, ujenzi na ukarabati wa barabara za Manyoni-Singida, Iringa – Dodoma - Babati na Babati-Singida.

Maelezo ya kina ya maoni na ushauri wa Kamati kwa ujumla yamo katika Taarifa ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mwaka wa Fedha 2007/2008 yaliyowasilishwa katika Mkutano wa Bunge la Bajeti lililopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2008/2009, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, semina kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu maboresho ya Serikali za Mitaa. Eneo la kwanza linahusu maboresho ya Serikali za Mitaa, Awamu ya I na II. Katika eneo hili, Kamati ilitafakari kwa makini kuhusu uelewa wa Waheshimiwa Wabunge juu ya maboresho hayo na kuona umuhimu wa kuwaandalia semina.

Kamati inaamini kuwa, Waheshimiwa Wabunge ni wadau wakubwa na muhimu wa maendeleo ya Taifa hili. Kutokana na kuwa karibu na wananchi, wakielimishwa vya kutosha juu ya maboresho hayo, wanaweza kutumia fursa hiyo vizuri kwa ajili ya kusukuma maendeleo haraka. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iandae semina ya maboresho ya Serikali za Mitaa, Awamu ya I na II kwa Wabunge wote kwa ajili ya kuwaelimisha kwa kina maboresho yanayoendelea katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza bajeti ya maendeleo Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kama nilivyoeleza hapo mwanzo, changamoto kubwa inayoikabili Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Mikoa kwa ujumla, ni ufinyu wa bajeti. Ufinyu huo umesababisha baadhi ya shughuli hususan miradi ya maendeleo kutokamilika ipasavyo. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), itenge fedha za kutosha kwenye bajeti yake ya maendeleo kwa miaka ya fedha ijayo. Kamati inaamini kuwa iwapo bajeti ya maendeleo itaongezwa itasaidia sana kusukuma maendeleo katika Mikoa na Halmashauri ambako ndiko kwenye kitovu cha maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwasilisha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Wilaya na Mikoa kwa wakati pamoja na ufinyu wa bajeti, Kamati imebaini kuwa lipo tatizo la ucheleweshaji wa fedha kutoka Hazina kwenda TAMISEMI, Mikoani na Wilayani kwa ujumla. Ucheleweshaji huu husababisha shughuli ambazo zimepangwa kutekelezwa zisikamilike kwa wakati.

Kamati inashauri kuwa jitihada za kutosha zifanyike kuhakikisha kuwa fedha zinazopelekwa katika maeneo yanayohusika hususan Mikoani na Wilayani zinafika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udhibiti wa watumishi wasiowajibika katika Halmashauri, eneo lingine ambalo linagusa sana hisia za wananchi ni kutowajibika ipasavyo kwa baadhi ya watumishi katika maeneo yao ya kazi hususan katika sekta za afya na elimu. Yapo malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kuwa wanapokwenda kupata huduma za tiba katika baadhi ya hospitali, zahanati au Vituo vya Afya, wamekuwa wakijibiwa vibaya na baadhi ya Wauguzi na wakati mwingine wanakosa huduma kabisa kutokana na Madaktari wanaohusika kutokuwepo kazini hususan nyakati za usiku. Vivyo hivyo yapo malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa baadhi ya Walimu hawatimizi wajibu wao ipasavyo katika maeneo yao ya kazi.

Kwa kutambua kuwa afya na elimu ni haki ya msingi ya kila mwananchi, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ishirikiane na Wizara nyingine kuwadhibiti watumishi wasiowajibika katika Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji hususan kwenye sekta za Afya na Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Ofisi/nyumba mpya za Serikali badala ya ukarabati, kama nilivyoeleza hapo mwanzo, katika tathmini iliyofanywa na Kamati yangu, kiasi fulani cha fedha zilizoombwa na Mikoa katika bajeti zilizopita na bajeti ya mwaka 2008/2009, zilitumika au zitatumika kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambayo mengine yamejengwa tangu ukoloni na mengine yanatumia majengo ya zilizokuwa taasisi za umma kama ilivyoelezwa katika Mkoa wa Kagera na Tanga. Aidha, yapo majengo mengine kama jengo la Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, halistahili kuwa katika hali linavyoonekana kulingana na hadhi ya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi.

Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa Mikoa iangalie uwezekano wa kujenga ofisi au nyumba mpya pale ambapo gharama za kukarabati nyumba au ofisi zinazohusika zitalingana na ujenzi wa nyumba/ofisi mpya.

Pamoja na hayo, Serikali iangalie uwezekano wa kujenga jengo jipya la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani ambalo linaonekana limejengwa mahali ambapo udongo wake unatitia na hivyo kusababisha ukarabati wa mara kwa mara.

Kwa mantiki hiyo hiyo, katika bajeti zijazo, Serikali iangalie uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma linalolingana na hadhi ya Dodoma kama nilivyoeleza awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za vitabu vya bajeti vya Mikoa kuonyesha maelezo ya kina za shughuli zilizopangwa katika kupitia vitabu vya bajeti vya Mikoa kwa mwaka wa fedha 2008/2009, moja kati ya upungufu uliojitokeza katika vitabu hivyo ni kukosekana kwa maelezo ya kina na ya kutosha kuhusu mafanikio na matatizo yaliyopo Mikoani na kwenye miradi ya maendeleo ya baadhi ya Mikoa.

Kutokana na dosari hiyo, Kamati inashauri kuwa katika bajeti zijazo, taarifa za bajeti za Mikoa, ziainishe kwa kina mafanikio na matatizo yaliyopo Mikoani pamoja na kutoa maelezo ya kutosheleza kuhusu miradi ya maendeleo inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya barabara katika zoezi zima la kuimarisha miundombinu ya barabara hasa zile zinazogusa mikoa, Kamati imebaini kuwa zipo barabara ambazo zinapita kwenye rasilimali nyingi ambazo kama zikitumiwa vema zinaweza kuongeza uchumi wa Taifa.

Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa miundombinu ya barabara za Dodoma - Manyoni, Manyoni - Isuna, Manyoni – Itigi – Tabora - Kigoma, Iringa -Dodoma, Dodoma - Babati na Somanga - Ndundu iimarishwe na kufanyiwa matengenezo makubwa ikiwezekana kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kwanza, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati.

Pili, napenda nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Mizengo Pinda, (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushirikiano mkubwa alioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Tatu, natumia fursa hii kuwashukuru, Mheshimiwa Philip S. Marmo, (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Celina O. Kombani, (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, (Mb.), Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo na Maafisa wote, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano walioutoa kwa Kamati na kuiwezesha kuwasilisha maoni yaliyoboresha makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mwisho kabisa, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mafungu yake yote. Umahiri na uzoefu wao wa muda mrefu katika nyanja mbalimbali za sekta za utumishi wa umma, Mikoa na Halmashauri, ndio ulifanikisha kazi hii. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Yusuf R. Makamba, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Rajab H. Juma, Mheshimiwa Abdubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangaro.

Aidha, napenda kumshukuru, Dkt. Thomas D. Kashililah, Kaimu Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa. Bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Charles Mloka, Ramadhani Abdallah, Elihaika Mtui, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha kuwa maoni ya Kamati yanakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, jumla ya Sh.1,664,839,294,000/= na Mfuko wa Bunge, jumla ya Sh.57,442,490,900/= kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Katiba kwa mawasilisho ya Maoni ya Kamati yako.

Kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ana masahihisho kidogo katika jedwali lao la maombi ya fedha. Maana alivyosoma Waziri Mkuu na ilivyokuwa kwenye machapisho kidogo kuna hitilafu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kuwa baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhitimisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009, baadaye tumepata rai kuwa kumekuwa na tofauti kati ya tarakimu ambazo zilikuwa zikisomwa na zile ambazo zilikuwa kwenye kitabu ambacho tumegawiwa.

Sasa tumethibitisha kwamba tarakimu zote ilivyo katika vitabu tulivyogawiwa yaani zilizoko katika kifungu cha 131 – 134, ukurasa wa 91 na ukurasa wa 92 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, zote ni sahihi. Tarakimu hizo ni sahihi jinsi ilivyo kwenye vitabu vyenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza tarakimu hizo ni sahihi isipokuwa kuna kosa dogo la kuchapa katika fungu la Mfuko wa Bunge pale kwenye kifungu cha 134, ukurasa wa 92, katika sentensi ya mwisho, Waziri Mkuu alisoma ifuatavyo:-

*"…Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 8,670,273,000 ni fedha za ndani na shilingi 367,232,900 ni fedha za nje."*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale mwisho kuna 900. Ndiyo maana jumla yote ya Mfuko wa Bunge ni shilingi bilioni 9,037,505,900.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa hii izingatiwe. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mmeelewa au turudie?

**WABUNGE:** Tumeelewana.
**NAIBU SPIKA:** Nashukuru. Kwa hiyo tatizo ni dogo kuliko tulivyofikiria.

Sasa nitamwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, nafikiri ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha, 2008/2009, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 96(6), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunifikisha kwenye haki na ukweli, baada ya kuishinda tena CCM kwenye Kesi ya Uchaguzi, Na.20/2005 ambapo Mahakama Kuu, Kanda ya Arusha, ilinitangaza kama Mbunge halali wa Karatu na kutupilia mbali malalamiko yaliyowasilishwa na waliojiita wakereketwa wa CCM.

Nawashukuru sana wananchi wa Karatu ambao waliendelea kuniunga mkono wakati wote wa kesi hiyo ya Uchaguzi. Nawapa pole kwa usumbufu wote waliopata kipindi chote cha kesi.

Nachukua fursa hii, kuwahakikishia kuwa nitawatumika kwa akili, moyo na uwezo wangu wote katika kufanya yale yote tuliyocheleweshewa kwa kipindi chote cha kesi.

Nachukua fursa hii pia kuwashukuru Watanzania wote kutoka kona zote za Tanzania, wenye mapenzi mema ambao kwa maelfu waliniletea salamu za pongezi baada ya Mahakama Kuu kutangaza ushindi huo tarehe 15/5/2005. Ahsanteni sana. Salamu zenu zilinifariji sana. Mwenyezi Mungu awarudishie mara mia kwa upendo wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa nimekosa fadhila, iwapo sitatoa shukrani kwa Chama changu CHADEMA, vyama vya *CUF, TLP, NCCR* - Mageuzi, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Kambi ya Upinzani, wakiongozwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Wabunge wenzangu wa Chama Tawala ambao wote kwa ujumla wao wakati wote wa kesi, walikuwa wakinitakia kheri na ushindi, huo ndio ni ukomavu wa siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, haki inaweza kucheleweshwa tu lakini haiwezi kamwe kupotea na wala ukweli hauwezi kufunikwa kwa mbinu na hila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Wakili wangu, Ndugu Tundu Lissu, kwa kufanya kazi yake kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, tumepata ushahidi wa dhahiri kwani kila tulipokuwa tukisema kuwa baadhi ya watu wa CCM huwa wanaiba kura, watu wengi walikuwa hawaamini na wengine hutuzomea. Kwa uamuzi wa Mahakama Kuu katika Kesi namba 20/2005, hasa kwa wakereketwa husika kuingiza nyaraka za kugushi na za udanganyifu Mahakamani, ushahidi wa wazi umepatikana na mbinu moja ya wazi ya wizi wa kura, nayo imebainika hadharani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana wahusika wakereketwa waliotufungua macho kwa njia ya kesi hiyo kwani itatusaidia sana katika kupanga mikakati bora zaidi katika kuthibiti wizi wa kura katika chaguzi zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kesi si jambo jema, lakini hakuna baya lisilo na jema, kwani bila kesi hiyo tusingeweza kufahamu siri kubwa inayotumika katika kuiba kura. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE – SENDEKA:** Kanuni ya 63(1).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, naomba ukae, Kanuni gani?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE – SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 63(1), kwa ruhusa yako, naomba kuendelea.

**NAIBU SPIKA:** Unaweza kuendelea.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE – SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Wilbrod Slaa, akiwasilisha taarifa yake hapo, alikitaja Chama cha Mapinduzi kana kwamba katika hukumu iliyotolewa, Chama cha Mapinduzi kilimwibia kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaweza kuwepo watu waliofanya makosa lakini Chama kama Chama hakikuwa na nafasi yoyote ya kuiba kura na si jadi ya Chama cha Mapinduzi kuiba kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, ningependa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, namheshimu sana kaka yangu lakini kwa kukitamka Chama cha Mapinduzi na kuthibitisha kwamba Chama cha Mapinduzi ni wezi wa kura, alithibitishie Bunge hili Tukufu kwamba Chama kama Chama kimeiba kura, yanaweza kuwepo matatizo ya mtu

binafsi lakini ni mtu siyo Chama na kama akashindwa kuthibitisha afute kauli hiyo. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kawaida kufuatana na Kanuni zetu, hatuwezi kuwa na hoja mbili wakati mmoja. Kwa hiyo, uamuzi wa hoja ya kwanza unafanyika halafu utakuja na ya pili. Sasa Mheshimiwa Dr. Slaa, una maelezo?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwamba Mheshimiwa Mbunge amezungumza hivyo lakini nasikitika kwamba hajui Kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 63(4), inamtaka Mheshimiwa anayetaka uthibitisho, yeye ndiye athibitishe kuwa ninachosema siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimezungumzia hukumu ya Mahakama na hukumu ya Mahakama, ni *public document,* wala kwa hukumu hiyo, sitakiwi kuleta Bungeni ushahidi kwa sababu tayari ni *public document*. Ndiyo utaratibu wa kesi ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani kwa bahati mbaya hakuelewa. Naomba mwenzangu atuthibitishie, amenipotezea muda wangu, naomba ulinde muda wangu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkipenda hapa kuwa ni uwanja kupigana vitimbi, mnaweza.

Kusema kwamba CCM imeiba kura, si kweli, ni kwamba kuna mtu aliyesimamia pale aliiba kura. *(Makofi)*

Pia kusema kwamba CHADEMA ilishtakiwa, si kweli, alishitakiwa Dr. Slaa. *(Makofi)*

Naomba labda nisikilize hoja ya pili ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto inasema nini.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 63(1), inazungumzia suala la kusema uongo. Kwa mujibu wa marekebisho ya Kanuni zetu za Bunge ambayo nasikitika sana Wabunge wengi hawajaisoma na ku-*internalize*, kwa mujibu wa marekebisho ya Kanuni za Bunge…

**NAIBU SPIKA:** Kabla ya kutumia Kanuni, soma Kanuni hiyo inasemaje?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Naomba Wabunge wa CCM, wakae kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa marekebisho ya Kanuni za Bunge...

**NAIBU SPIKA:** *Order please*!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wabunge wa CCM wakae kimya, umenipa nafasi ya kuzungumza. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini, matusi hayo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kila mtu Kanuni inamdai am-*address* Spika, hakuna mtu anayetakiwa kum-*address* mwingine. Sasa nimempa nafasi Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa hiyo, naomba msikilize. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ambao nataka kueleza ni kwamba kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kanuni ya 63 (1) (2) (3) (4) (5) (6) (7) (8) (9) (10), zinaelezea utaratibu wa Mbunge kusema uongo na uthibitisho wa uongo. Inamtaka Mbunge anayetoa hoja ya Mbunge mwenzake kusema uongo, anapaswa yeye athibitishe huo uongo unaosemwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba utoe maelekezo hayo kwa Wabunge badala ya kupoteza muda wa hoja ambazo zinazungumzwa kwa kuanza kuwasimamisha Wabunge wengine kuzungumza, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kama hoja ni hiyo, nimeshatoa uamuzi. Sasa naomba Mheshimiwa Dr. Slaa, uendelee. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani dakika zangu zimelindwa, mimi sitazijua tena.

**NAIBU SPIKA:** Watakulipa. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Ahsante.

Kwanza niseme tu kwamba kwa bahati mbaya Wabunge, inawezekana hawakusikiliza vizuri, mimi sikusema CCM…

**NAIBU SPIKA:** Tumeshafanya uamuzi, endelea.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Naweka rekodi sahihi kwa sababu iko kwenye *Hansard*.

**NAIBU SPIKA:** Ulishaweka!

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mizengo K.P. Pinda, (Mb), Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Waziri Mkuu na hatimaye kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu.

Ninampongeza pia Mheshimiwa Celina O. Kombani, (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Pia Mheshimiwa Aggrey Mwandri, kwa uteuzi huo, lakini pia kwa kuandaa bajeti yao hii ya kwanza, wakisaidiana na Makatibu wao Wakuu na wataalamu wao wote. Aidha, napenda kumpongeza kwa dhati kwa hotuba yake nzuri na ya kina pamoja na kwamba hakutoa ufafanuzi wa kina katika maeneo kadhaa muhimu kama nitakavyoeleza baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mtovu wa shukrani, iwapo sitakushukuru wewe binafsi na Wenyeviti wa Bunge na Mheshimiwa Spika, japo nilikuwa nimegeuza kutokana na utaratibu, kwa kazi nzuri mnayofanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Ninamwomba Mwenyezi Mungu awajalie hekima na busara na kuwapatia nguvu na afya mnazohitaji katika kuliendesha vizuri Bunge letu hasa katika kipindi hiki kigumu katika historia ya nchi na Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni bajeti ya tatu tangu Serikali ya Awamu ya Nne iliposhika uongozi wa nchi yetu. Kambi ya Upinzani inatoa maoni yake kwa kufanya tathmini ya malengo na mwelekeo wa kazi za Serikali katika vipindi mbalimbali vya nyuma ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa malengo ya Serikali ya Awamu ya Nne kwa kipindi cha tangu waliposhika madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Waziri Mkuu ni msimamizi wa Shughuli za Serikali Bungeni na mjadala wa Waziri Mkuu unaihusu Serikali yote, tunapenda Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe majibu ya kuridhisha katika maeno yote ambayo Waziri wa Fedha, hakutoa majibu ya kuridhisha siku alipokuwa anafunga hotuba yake hasa kwa vile Waziri Mkuu ndiye mwenye kauli kuhusu shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kupanga bajeti ni hatua moja muhimu lakini usimamizi wa fedha hizo ni muhimu zaidi, mchango wa Kambi ya Upinzani, safari hii utajikita zaidi kwenye maeneo mengi yenye utata ili Bunge na wananchi kwa ujumla wapate majibu ya kuridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Waziri Mkuu katika hotuba yake, amegusia kwa kifupi sana suala la rushwa, katika *para* ya 96 na 97. Ikizingatiwa kuwa kwa muda mrefu sasa Taifa letu, ndani ya Bunge hili Tukufu, kwenye mikutano ya hadhara na kwenye Vyombo vya Habari, limegubikwa na taarifa za kusikitisha kuhusu tuhuma za uvunjifu

wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Na.13 ya mwaka 1995, zinazomhusisha Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kuhusiana au kupitia makampuni anayomiliki ya *Tanpower Resources Ltd* na *ANBEM*. Tuhuma hizo pia zimemhusisha aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini wa kipindi hicho hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaona si vema kujadili masuala ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu tu, bila kupata ufafanuzi wa kina wa maswala haya muhimu kwani imani ya Watanzania wengi imeguswa na tuhuma hizi na hivyo kuwa na mashaka na fedha nyingi zinazoidhinishwa na Bunge kama kweli zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na wananchi wote wanaopenda kujua ukweli, mchango wetu unajikita katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu/rushwa na ufisadi. Bajeti inatumika na Serikali kupanga matumizi ya fedha kidogo zilizopo katika maeneo na sekta muhimu zinazohitaji kipaumbele katika kuleta maendeleo kwa Taifa na wananchi wote kwa ujumla. Hivyo, ni kweli kuwa bajeti ni silaha na chombo muhimu sana katika kutoa dira ya utendaji kazi katika Serikali na katika Taifa. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani, ina maoni kuwa kupanga ni kitu kimoja na kutumia kilichoidhinishwa na Bunge ni kitu kingine. Tatizo kubwa zaidi ni katika nidhamu ya matumizi na uadilifu wa kutumia kilichoidhinishwa na Bunge kwa malengo yaliyopitishwa katika bajeti. Ni kwa msingi huo, haiwezekani kutenganisha masuala ya bajeti na masuala ya udhibiti wa matumizi na nidhamu ya matumizi na uadilifu wa wanaopewa majukumu ya kusimamia utekelezaji wa bajeti husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, iliamini kuwa hotuba ya Waziri Mkuu, itaingia kwa undani kuondoa mashaka katika hali hii ya hewa iliyochafuliwa na mjadala wa ufisadi, kwa bahati mbaya haikufafanuliwa kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba yetu, Ibara 63(2), Bunge ndiyo chombo kikuu katika Jamhuri ya Muungano na majukumu yake ya kikatiba tukiacha ya kutunga Sheria, ni kuisimamia na kuishauri Serikali.

Kambi ya Upinzani, ina maoni kuwa kwa vile viko vyombo vingi na watu wenye sifa mbalimbali wanaofanya kazi ya kuishauri Serikali, Bunge ndiyo chombo pekee cha kuisimamia Serikali. Hivyo, ni lazima Bunge lifanye kazi hii kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lisipotimiza wajibu wake huu vizuri na mambo yakaharibika katika nchi, Bunge halitakuwa na maelezo yoyote kwani hakuna chombo kingine chochote kwa mujibu wa Katiba yetu chenye uwezo wa kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema Serikali ni pamoja na kusimamia matendo na maamuzi ya Rais. Jambo ambalo watu wengi hawalielewi kwa kudhani kuwa Rais yuko juu ya Sheria ya nchi.

Kambi ya upinzani imependa kuweka wazi suala hili kutokana na mawazo mbalimbali yanayojitokeza mara kwa mara katika mijadala mbalimbali, kama yalivyoripotiwa na vyombo mbalimbali vya habari. Huu ni msingi mkubwa katika nchi ya kidemokrasia na hasa inayofuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka yaani *separation of powers.* Bunge basi linajukumu pekee la kuisimamia Serikali na vyombo vyake vyote bila kuingilia utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kusimamia ni pamoja na kupata taarifa zote zinazohitajika kutekeleza jukumu la usimamizi, kufanya maamuzi na kusimamia maamuzi hayo muhimu pale inapohitajika kama chombo cha usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubadhirifu kupitia *EPA* na *Richmond*, mwaka uliopita, wakati nawasilisha hoja ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu, nilitoa hoja mbalimbali kuhusu ubadhirifu mkubwa ndani ya Benki Kuu ya Tanzania, *(BOT)*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kanuni ya 68(7). Naomba mwongozo wako Mheshimiwa Naibu Spika kuhusu suala la *Richmond.* Bunge lako Tukufu, liliarifiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba wakati wowote atatoa taarifa ya mapendekezo yote ya Tume ya Mwakyembe, wakati wowote ambapo Spika atamruhusu katika Mkutano huu. Sasa itafaa jambo hili tulijadili kabla ya Mheshimiwa Spika hajaliweka katika orodha ya Shughuli za Bunge?

Pili, suala la *EPA* liliundiwa Tume na Mheshimiwa Rais na Tume hiyo wakati wowote itamkabidhi Rais taarifa yake. Je, itakuwa ni sahihi sasa kujadili shughuli ambayo sasa hivi inafanyiwa kazi na Tume ya Rais? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu haya ni maoni ya Kambi ya Upinzani, sasa kama itaamuliwa chochote kile ndipo hapo uamuzi hautafikiwa kwa sababu kuna Kamati hizo lakini maoni ya Kambi ya Upinzani yaendelee. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kwamba nakatishwakatishwa, sasa sijui niliachia wapi, halafu naanza wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka uliopita wakati nawasilisha hoja ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu, nilitoa hoja mbalimbali kuhusu ubadhirifu mkubwa ndani ya Benki ya Tanzania, kama ilivyonukuliwa na kumbukumbu ya Bunge, "*Hansard*" ya Kikao cha Tisa, Tarehe 25 June, 2007. Pamoja na kwamba hoja hiyo

ilipingwa sana na baadhi ya Wabunge wenzangu, nashukuru kuwa sasa suala la ubadhirifu katika vyombo vyetu mbalimbali na ndani ya Serikali, siyo tena suala la mjadala kwani mengi zaidi yamejitokeza. Jamii nayo sasa imezoea neno 'Ufisadi' na ufisadi unajadiliwa kwa uwazi bila woga tofauti na ilivyokuwa hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya habari, navyo vimefanya kazi nzuri sana kufanya uchunguzi wa kina na kuwapa habari Watanzania kuhusu hali ya ufisadi katika nchi yetu. Kambi ya Upinzani inavipongeza sana vyombo vyote vya habari kwa kazi nzuri waliyoifanya na waendelee na moyo huo huo wa kuwaelimisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,, Kambi ya Upinzani, imefarijika sana kwamba sasa pazia kubwa lililofunika masuala ya ubadhirifu, limeondoka na masuala haya yanajadiliwa siyo tu ndani ya Bunge lako Tukufu bali na Watanzania ambao kimsingi ndiyo wadau wakubwa na wamiliki wa mali na rasilimali za Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala wa ubadhirifu na ufisadi, ndani ya *BOT* kuhusu Kasma ya *EPA*, ulishafika ndani ya Bunge kama chombo cha usimamizi. Bunge kama wawakilishi wa wananchi, limestushwa na kiwango kikubwa cha ubadhirifu huu, tena wakati wananchi wanajifunga mikanda, wanakabiliwa na hali ngumu ya maisha kutokana na gharama ya maisha ambayo imepanda sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuwa gharama ya maisha imepanda kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wetu, hazikubaliki kwa sababu haiwezekani hali hiyo iwe hivyo kwa wananchi wa kawaida tu, wakati kundi dogo la watu, kama ilivyoainishwa kwenye ufisadi wa *EPA,* linaneemeka na limeachiwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wa Tanzania, wameacha kunywa chai kwa vile sukari sasa imekuwa bidhaa ya anasa. Mikate iliyokuwa kimbilio la walala hoi hasa mijini, imekuwa haishikiki tena kwa vile bei ya mkate inakimbilia Sh.1,000. Nyama inazidi kuwa hadithi ya kusadikika kwa Watanzania wengi kwani bei ya kilo inakimbilia zaidi ya Sh.2,500. Mchele ukiacha mahindi ambao ni chakula cha Watanzania wengi, unakimbilia Tsh. 1,500 kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Bunge kama mwakilishi wa wananchi, lichukue nafasi yake kusimamia maslahi ya Watanzania na kulinda haki yao kwa kusimamia vizuri fedha, mali na rasilimali za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 8(1)(a) inatamka kuwa:-

*"wananchi ndio msingi wa mamlaka yote…"*

Ibara ya 8(1)(d), inataka wananchi washirikishwe katika shughuli za Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo haielekei kabisa kama Serikali inawajibika kwa wananchi. Wananchi wamebaki kuwa watazamaji katika shughuli za Serikali tofauti na matakwa ya Katiba kwani kama Bunge hili ambalo linawawakilisha wananchi, linashindwa kushirikishwa hata kwa mambo ya msingi, ni kwa namna gani Serikali itajitetea kuwa wananchi wanashirikishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni haya yanatokana na mambo yafuatayo:-

Moja, hadi sasa, takriban miezi sita, tangu taarifa ya ukaguzi wa *EPA* kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais, taarifa hiyo imebaki kuwa siri. Ninalisema hili kwa sababu nimeeleza mwanzo kazi yetu ni kusimamia vitu vinavyofanywa na Serikali inayoongozwa na Rais. Usiri huu ndio unaosababisha minong'ono mingi na mashaka kuwa Serikali haiko makini na vita dhidi ya ufisadi. Ufisadi ulihojiwa ndani ya Bunge na ilikuwa muhimu kwa Serikali kutoa taarifa ya kina kwa Bunge na kwa umma wa Watanzania. *(Makofi)*

Pili, Kambi ya Upinzani, imestushwa sana na Taarifa ya Mheshimiwa Mkulo, Waziri wa Fedha, alizotoa Bungeni Ijumaa wakati anahitimisha hoja yake kuwa "Fedha za *EPA* si za Serikali bali za wafanyabiashara walizolipa kwa ajili ya kununua bidhaa nje".

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa hiyo ambayo dhahiri ni ya kupotosha, Kambi ya Upinzani imefanya utafiti wa kina na kugundua kuwa Fedha hizo kimsingi zinatokana na programu inayoitwa *"Debt Buy Back Program"*. Hata hivyo, ukaguzi uliofanywa na *Deloitte and Touche* 2006 na baadaye kuthibitishwa na Ernest and Young, 2007, ulithibitishwa kuwa Kampuni 22 zilifanya biashara na makampuni yanayodhaniwa "hewa".

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kati ya wafanyabiashara hao 13, si wao, wala principles wao nje ya nchi, hawakuweka fedha zozote *BOT* kwa ajili ya kutimiza masharti ya *Debt Buy Back Program k*ama alivyotaka kueleza Waziri wa Fedha. Badala yake walitumia nyaraka za kugushi, kama inavyoonekana katika vielelezo mbalimbali vya ukaguzi ambavyo tunavyo. Kwa msingi huo, fedha zilizoibiwa ni za Serikali ya Tanzania na Kambi ya Upinzani inasisitiza fedha zote za EPA kama zilivyoainishwa na Wakaguzi, zirejeshwe Serikali kwa manufaa ya Taifa zima. *(Makofi)*

Aidha, Waziri Mkuu pia kama Msimamizi wa Shughuli za Serikali Bungeni, atoe tamko la Serikali kuhusu kauli hiyo ya Waziri wake ambayo imeleta mfadhaiko zaidi katika jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya ukaguzi wa *EPA* ambayo nakala yake tunayo katika kifungu cha 3.20, 3.23, na 3.24, kinatamka wazi uwepo wa *"fraudulent supporting documents submitted in to support claims"* yaani ufisadi uliotumika ni pamoja na kutumia hati za kugushi katika kutoa fedha kutoka *BOT* (tafsiri haikuwa moja kwa moja). Malipo ya viwango visivyo sahihi au kutumia viwango visivyo sahihi vya kubadilisha fedha (yaani *incorrect amounts and incorrect exchange rate)*. Ukaguzi ulionyesha kuwa kati ya Tsh.133 bilioni zaidi ya Sh.90.3 bilioni yalifanyika kwa kutumia

hati za kugushi *(invalid and fraudulent supporting documents)*, nyaraka hizi zimeonyeshwa katika kiambatanisho “C” ikionyesha na majina ya makampuni husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, katika kifungu cha 3.25, ukaguzi huo ulishauri kuwa kwa malipo ya zaidi ya 42.6 bilioni uchunguzi wa kina zaidi ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ufisadi unaotisha zaidi ni ule uliofanyika kupitia Kampuni ya *Kagoda Agriculture Ltd*, iliyosajiliwa nchini chini ya Sheria ya Makampuni, Sura ya 212, tarehe 29 September, 2005 na kupata Hati Na.54040. Wakurugenzi waliosajiliwa wa Kagoda, ni watu wawili wenye anuani za *Kipawa Industrial Area, Plot no 87* Temeke Dar-es-Salaam, P.O. Box 80154, Dar-es-Salaam, kinyume na utaratibu wa usajili BRELA ambapo unahitaji Wakurugenzi wa Makampuni kujisajili kwa kuonyesha anuani ya mahali anapoishi na siyo Sanduku la Posta.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe, kwenye fomu za usajili, ambapo Bwana mmoja anayeitwa John Kyomuhendo, amejionyesha kuwa *“Promoter”*, hawakuonyesha kama ni Wakurugenzi mahali pengine kwenye kampuni nyingine yeyote. Cha kushangaza ni kuwa Kampuni hiyo ambayo Wakurugenzi wake dhahiri wanaonekana wapya kabisa katika uwanja wa biashara isipokuwa kama walidanganya kwa sababu wanazofahamu wenyewe, ndani ya wiki nane, walikuwa wamekwishachotewa zaidi ya dola za Marekani 30.8 milioni yaani karibu zaidi ya Sh.40bil.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya makampuni ambayo yamefanya biashara na kampuni hiyo kama inavyoonekana kwenye kifungu cha 3.27; yanadhaniwa kwamba ni makampuni hewa. Baadhi ya makampuni hayo ama hayajulikani yaliko au hayako kabisa au yamekwishakubadilisha jina yanaonekaana kwenye kifungu cha 3.27. Makampuni hayo ambayo yako Marekani, Japan, Ujerumani, Italia, Ufaransa, mengine hata anuani zake hazikujulikana kabisa. Katika hali hii inayoonyesha wazi kuwa kulikuwa na kugushi.

Kinachotisha zaidi hata kampuni ya ukaguzi ya *Deloitte*, kwa barua yao kwa Gavana wa Benki Kuu ya tarehe 6 September 2006 na kwa Wakurugenzi wote wa *BOT* ya tarehe 10 October, 2006 kati yao akiwemo Katibu Mkuu wa Hazina, Bwana Gray Mgonja, kuwa kuna utata kuhusu Kampuni ya Kagoda, ambayo japo ilisajiliwa 29 September, 2005 tarehe 10 September 2005 yaani siku 19 kabla ya kusajiliwa, tayari ilikuwa na mkataba wa kiasi cha fedha za Japan (Japan Yen), JPY 956,110.986 na Kampuni ya Nishizawa Ltd na mkataba mwingine wa Dola za Marekani 9,057,463.90, wa Tarehe 12 September, 2005 zaidi ya siku 15 nadhani na Kampuni ya Textima Ltd na mikataba hii yote inatamka kuwa “Kampuni hii imesajiliwa Tanzania kwa mujibu wa Sheria” jambo ambalo dhahiri ni udanganyifu na ni uvunjifu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, isitoshe Kampuni ya *Deloitte* ilionyesha katika Barua walizomwandikia Gavana na Wajumbe wa Bodi, dosari zifuatazo katika Mikataba *(Deeds of Assignments)*, kuwa na maneno na mfumo unaofanana jambo linaloashiria kuna kugushi, kwani makampuni kwa kawaida yanapenda kuwa na vipengele visivyofanana. Kati ya hati zote hizo, hakuna hata moja iliyowekwa kwenye *“Letter*

*Head"* ya Kampuni zao, mikataba yote imesainiwa ukurasa wa mwisho tu tofauti na kawaida ya kusaini mikataba. Makampuni 12 yana muhuri *(seal)* unaofanana na ule wa Kampuni ya Kagoda, Mikataba ya Makampuni ya *Fiat Veicoli Industriali ya Italia, Valmet (USA) Adriano Gardella S.P.A (Italy),* yote haikuwa na mihuri japo mkataba unaonyesha kuwa muhuri umewekwa, Kampuni ya Valmet yenye mkataba wa dola za Marekani 2,398,439.96 umewekewa saini na mtu anayeitwa Patrick Kevin, Mhasibu *(Accountant),* jambo ambalo si kawaida kwa mkataba wa kiwango kikubwa kiasi hicho. Mambo haya yote yalipaswa kutoa ishara kwa Benki Kuu kuwa mikataba yote imegushiwa lakini wala siyo Benki Kuu wala Wakurugenzi waliostuka na kuchukua hatua pamoja na barua hiyo ya *Deloitte.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, fedha hizi zililipwa kupitia Benki zetu wenyewe yaani Benki ya Kitanzania ambayo ni *CRDB* Benki. Hii ni Benki ambayo ilipaswa kuonyesha uzalendo kwani pamoja na ukweli kuwa mabenki ya kigeni kama vile *Kenya Commercial Bank* na *Barclays Bank,* walikataa kulipa fedha hizo baada ya kuona kuwa zina harufu ya kifisadi na hata ikafikia mahali wakafunga *Account* za mteja mmojawapo baada ya kutilia shaka malipo hayo na kuwaandikia *BOT* pamoja na kuwarudishia hundi zao, ila Benki yetu wenyewe ya *CRDB* haionekani ikichukua hatua zozote zile hata pale ambapo malipo hayo yalipofanyika kwa mkupuo kwa siku moja kwenye matawi tofauti ya Benki hiyo Jijini Dar es salaam kama vile matawi ya Kijitonyama, Azikiwe, Vijana, Lumumba na Holland. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, badala ya Gavana au Wakurugenzi ambao walijulishwa rasmi kuchukua hatua yeyote ya kisheria, hawakuchukua sheria stahiki badala yake Gavana wa Benki Kuu alimjulisha Bwana Samuel Sithole, Mkurugenzi wa Kampuni ya Deloitte ambaye alisafiri toka Afrika Kusini kuokoa hali hiyo, kuwa Waziri wa Fedha (wa wakati huo), anafahamu malipo *(Transactions)* hiyo na angeweza kuwapatia Wakaguzi nyaraka zote husika kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Wakaguzi walikutana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wa wakati huo, tarehe 11 September 2006 na kuelezwa kuwa malipo hayo yanahusu "masuala ya usalama wa Taifa" *(State Secrets)* na kwamba Wakaguzi hawatapewa nyaraka zozote kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 14 September, 2006, Wakaguzi wa Deloitte walipewa '*Draft Confirmation Letters"* lakini bila nyaraka zozote *(supporting documents).* Ndipo Wakaguzi walipomweleza *Governor*, tarehe 14 kuwa kutokana na hali hiyo wanatoa kwa *BOT* "Hati ya Mashaka *(Qualified Opinion)* ya Ukaguzi. Sababu ya msingi ni kuwa Wakaguzi waliamini kuwa nyaraka zilizotumika katika malipo hayo 'ni za kugushi' na kuwa kulikuwepo na uwezekano mkubwa wa ufisadi mkubwa katika malipo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya kuchukua hatua, kwa mshangao mkubwa, tarehe 21 September 2006, Wakaguzi wa *Deloitte* walifukuzwa kazi kwa kusema ukweli kwa barua kutoka *BOT*. Hii ni hali ya kutisha. Ni dhahiri kabisa kuwa Uongozi wa Benki Kuu, Wakurugenzi wa Benki Kuu akiwemo, Gray Mgonja, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Waziri wa Fedha, wote walihusika au kuficha au kwa uzembe katika njama za

kuficha au kutaka kuficha ukweli huu uliowekwa bayana na Wakaguzi wa Kampuni ya Kimataifa ya Deloitte ambayo kwa hakika walionekana wazi kufanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe kitendo hicho cha kufuta mkataba wa Wakaguzi wakati kazi ya ukaguzi imekamilika na Wakaguzi wameonyesha dosari kubwa katika mahesabu *(irregularity),* ni kukiukwa kwa taratibu za Kimataifa za ukaguzi (Tazama Barua ya Deloitte ya 10 October, 2006 iliyopelekwa kwa Mheshimiwa Zakia Meghji).

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu Kampuni ya *Richmond* iliyoingiza nchini majenereta kwa ajili ya umeme wa dharura, haujatolewa taarifa. Kimsingi Kambi ya Upinzani inashangazwa na hali ilivyo, kwani tulitegemea Serikali itatoa taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na si majibu ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maazimio kuhusu watu waliotakiwa kuchukuliwa hatua za kinidhamu hayajatekelezwa. Watu hao bado wako kazini kama desturi. Mikataba iliyotakiwa kusitishwa, haikusitishwa miezi kadhaa tangu Maazimio hayo kupita. Kambi ya Upinzani, inashangazwa na hali hii na haitegemei kuwa Maazimio ya Bunge, ambayo ndio msimamizi wa shughuli za Serikali, hayatekelezwi bali yanatafutiwa "maelezo". Hii ni hali ya hatari katika mustakabali wa uendeshaji wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, pamoja na taarifa ya ufisadi ndani ya *BOT*, pia hakuna hatua yeyote iliyochukuliwa kuhusu maeneo mengine tuliyoyaibua mathalani ufisadi kupitia Kampuni ya Meremeta na Tangold. Waziri wa Fedha ambaye ndiye mwenye dhamana na makampuni hayo katika majibu yake siku ya Ijumaa amerusha masuala hayo kwa Mawaziri wa kisekta. Inawezekana Serikali inasubiri Bunge liunde tena Kamati Teule nyingine kwa lengo la kupitia makampuni haya ambayo umiliki wake umegubikwa na utata mkubwa kutokana na Meremeta kuandikishwa Uingereza ikiwa na Hati ya Usajili Na.3424504 ya tarehe 19 August, 1997 na kupata Hati ya Kutimiza Masharti *(Certificate of Compliance)* nchini Tanzania kama Tawi la Kampuni ya Kigeni yenye Na.32755 ya tarehe 3 Oktoba, 1997. Hii haieleweki kwa sababu Meremeta tuliambiwa ni kampuni itakayoshughulika kusaidia Jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoshangaza katika Kampuni hii ni kuwa wenye hisa wake tofauti na Bunge lilivyoelezwa mara nyingi, ni *Triennex (PTY) Ltd* ya Afrika Kusini yenye hisa asilimia 50%, Msajili wa Hazina mwenye hisa asilimia 50% kwa niaba ya Serikali ya Tanzania na Kampuni mbili za *London Law Services* Ltd wa Temple Avenue, wenye hisa 1% na *London Law Secretarial Services* Ltd ambao anuani yao ni sawa na hao wenzao, nao pia wana hisa 1%. Hii Meremeta hasa ni ya nani na hawa *London Law Services* na *London Secretarial Services* kwenye kampuni yetu ni akina nani hasa? Haya ni majibu ambayo Watanzania lazima wapate. Kampuni ya Meremeta ina hisa asilimia ngapi? Hivi Serikali inaogopa nini kuweka mambo haya wazi, hadharani angalau kwa Kamati husika ya Bunge basi ili kama kuna sababu ya msingi wawakilishi wa wananchi waweze kufahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi, hivyo hivyo kwa Kampuni ya *Tangold* ambayo ilisajiliwa katika kisiwa cha Mauritius tarehe 5 Aprili, 2005 ikiwa na Hati ya Usajili Na. 553334 na kupata *Global Business Licence* (C2/GBL) tarehe 8 Aprili, 2005 na kupata Hati ya Kutimiza Masharti hapa nchini tarehe 20 February 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, taarifa zilizoko ni kuwa *Tangold* imekuwa na akaunti *NBC Corporate Branch, No*. 0lll03024840 iliyofunguliwa tarehe 1 Januari, 2003 yaani miaka miwili kabla Kampuni hiyo haiijasajiliwa Mauritius na takriban miaka minne tangu imepata Hati ya 'Kutimiza Masharti' Tanzania. Ni kwa vipi, kampuni hii kufanya kazi wakati Bunge lilijulishwa na Mheshimiwa Waziri Karamagi kuwa ndiyo iliyorithi Meremeta baada ya Meremeta kufilisika? Meremeta ilifilisika mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali haya yanahitaji kujibiwa kinagaubaga ili kuwarudishia Watanzania imani kuhusu kinachojiri na usalama wa rasilimali na fedha zao. Waziri Mkuu ndiye mtu stahiki wa kurudisha imani hii kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, baada ya Waziri wa Fedha kushindwa kutoa majibu ya kuridhisha juzi. Isitoshe, Makampuni haya tangu yaliposajiliwa nchi za nje na hata hapa Tanzania japo yamekuwa na akaunti katika benki za nje na za ndani, hesabu zao hazijakaguliwa na chombo chochote hadi leo (hatujui kama itakuwa imekaguliwa na *CAG* katika Taarifa ya *BOT* ya 2007/2008 ambayo haijawasilishwa Bungeni bado). Wahusika wa *Tangold* na Bodi ya Wakurugenzi ni viongozi au waliokuwa viongozi waandamizi katika Serikali. Wakurugenzi hao ni pamoja na hayati Daudi Balali aliyekuwa *Governor* wa Benki Kuu *(BOT),* Andrew Chenge aliyekuwa Waziri wa Miundombinu, Gray Mgonja, Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Patrick Rutabanzibwa, Katibu Mkuu, Maji na Vincent Mrisho, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana kupata majibu ya maswali haya kwa mustakabali wa nchi yetu. Kupitisha bajeti, ni kitu kimoja na kuziba mianya ya ubadhirifu ni kitu kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hayo yote yanayohusu ufisadi ndani ya *BOT*, Kambi ya Upinzani, inastushwa kuwa wajumbe wa Bodi ya *BOT* waliokuwepo wakati wote wa sakata hilo bado wamebaki katika Bodi mpya akiwemo Katibu Mkuu wa Hazina Gray Mgonja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Rais, amwondoe haraka iwezekanavyo, Gray Mgonja katika nafasi yake ya Ukatibu Mkuu wa Hazina. Gray Mgonja, amekuwa mjumbe kwa kofia yake ya Katibu Mkuu wa Hazina. Vivyo hivyo, Rais wa Zanzibar naye amwondoe Ndugu K.M. Omar, Katibu Mkuu wa Hazina (Z), ambaye naye anaingia kwa kofia yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii, itaruhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Wakaguzi (kif.4.3) nanukuu hapa:-

*"Wakurugenzi wote wa BOT waliokuwepo kati ya Septemba 2005 na Oktoba 2006, waondolewe wote na wengine wapya kuteuliwa"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inawezekana ndiyo sababu kwa nini Serikali haileti taarifa hizi. Ni kwa njia hii tu, Serikali itarudisha imani ya Watanzania kwa chombo hicho kikubwa katika nchi kusimamia hazina, mali na rasilimali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliambie Bunge hili, ni lini uchunguzi wa kina utafanyika kuhusu ubadhirifu katika maeneo mengine yanayohusu Meremeta, Tangold, Mwananchi *Gold Co. ltd* na *Deep Green Finance Company Ltd*? Kambi ya Upinzani haikuona uchunguzi wowote katika Taarifa ya Uchunguzi wa *EPA* kuhusu makampuni haya na Kamati ya Bomani nayo kwa Taarifa tuliyonayo imependekeza uchunguzi wa haraka ufanyike kunusuru rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inahitaji maelezo ya kina siyo tu jinsi fedha zilivyokuwa zinahamishwa, bali pia nani wamiliki wa makampuni hayo binafsi yaliyolipwa fedha za walipa kodi wa Tanzania? Kwa nini Kampuni kama ya *Deep Green Finance* ilikuwa inafanya kazi wakati haikuandikishwa hata *BOT* kama *financial institution* kama utaratibu unavyotaka? Kwa nini *Tangold* imefanya kazi nchini miaka minne kabla haijasajiliwa? Kwa nini Msajili wa Hazina ambaye ndiye mmiliki wa mali za Taifa, kwa niaba ya Serikali, hajaorodheshwa mahali popote katika Hati ya Usajili ya *Tangold*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwasilishe mara moja, Muswada wa Sheria Bungeni ili kuondoa utata unaosababishwa na mgongano wa nafasi za Mwenyekiti wa Bodi na *Governor* wa Benki Kuu, nafasi ambazo kwa sasa zote zimeshikiliwa na mtu mmoja. Pia kuweka kisheria nafasi ya *Independent Audit Committee* ambapo kwa sasa Kamati hii inatoka ndani ya Bodi yenyewe na kupitia upya Sheria nzima kama ilivyopendekezwa na Wakaguzi (Kif.4.4). Haya ni maneno ya Wakaguzi siyo ya kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali, bila kuchelewa, kuwachukulia hatua za kinidhamu na za kisheria, Maofisa wote waliotajwa katika Taarifa ya Ukaguzi ya *Ernest and Young* na kukubaliwa na *CAG* mathalan, Mkurugenzi wa Fedha wa *BOT*, Katibu wa Benki Kuu *(SB)*, Mkurugenzi wa Sera za Uchumi *(DEP)*, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Madeni *(DDDD)*, Kaimu Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani *(IA)*, Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Shughuli za Benki *(Director of Bank Supervision)*. Kama hatua zimekwisha kuchukuliwa, basi Waziri Mkuu alijulishe Bunge hili na Taifa kwa ujumla juu ya hatua zilizochokuliwa ili Bunge liweze kutimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hotuba hii iko kamili, basi naomba inukuliwe jinsi ilivyo, siyo kama ninavyoisoma, kwa sababu ya kukatishwakatishwa, sasa sijui muda wangu tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wakaguzi walivyopendekeza, Kifungu cha 4.1, Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu, ni kwa nini Serikali hadi sasa imeshindwa kutekeleza pendekezo la kufungua upelelezi rasmi wa kijinai *(formal criminal*

*investigation)* na badala yake kumekuwa na utata wa kinachoendelea kwani kumetolewa taarifa zinazogongana mara kwa mara na Kamati ya Mwanyika, Waziri wa Fedha na wakati mwingine hata na Wasemaji wa CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizo zimedai kurudisha au kukusanya mapato zaidi. Watanzania wamechanganyikiwa na kinachoendelea. Wanataka kujua mapendekezo ya Wakaguzi yanatekelezwa vipi, hatua gani imefikiwa, fedha ngapi zimerejeshwa, akaunti ngapi za wahusika zimefungwa *(freeze)* na wahusika wangapi wamekwisha kufikishwa Mahakamani kati ya makampuni 13 yanayohusika na tuhuma za ufisadi wa zaidi ya Sh.90,359,078,804.13. Hizi ni fedha nyingi sana, Bunge haliwezi kukaa kimya kwa kusubiri Serikali kwamba inafanya kazi halafu Serikali haileti hata baada ya muda mrefu namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna fedha zimerejeshwa, ni kiasi gani kimerejeshwa, nani amezirejesha na zimewekwa wapi? Haya ni maswali muhimu, ni vema Serikali ikayajibu na kama kwa sababu yoyote ile, itakuwa si vema kuyajibu ndani ya Ukumbi wa Bunge zima, basi majibu yatolewe kwa Kamati ya Bunge ya Kudumu inayohusika na masuala hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge kama msimamizi kwa niaba ya wananchi, itafanya makosa kuachia majukumu yake ya "kusimamia" kwa Serikali ambayo katika hatua ya awali ndiyo imetufikisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaelekea, Serikali inafanya utani kwa kutotoa tamko kuhusu kifo cha Dr. Balali aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu. Watanzania tunashindwa kuielewa Serikali kwa kukaa kimya angalau kungekuwa na hata sentensi moja katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu Balali, hakuwa mtu wa kawaida tu, Ndugu Balali alikuwa msimamizi wa taasisi kubwa na nyeti sana katika nchi yetu. Ndugu Balali, anahusishwa na tuhuma zote zinazohusiana na ufisadi mkubwa ndani ya *BOT*. Ndugu Balali, ndiye mtu pekee aliyekuwa na ufahamu wa kina kuhusu kilichojiri katika hayo yote yanayotuhumiwa. Serikali haikumhoji japo ilifahamu kwamba Ndugu Balali alikuwa mgonjwa jambo linalohitaji maelezo ya kina! Serikali ilikuwa na hofu gani kumhoji Ndugu Balali?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitengua uteuzi wa Ndugu Balali bila hata kumpa haki yake ya kusikilizwa, jambo linaloleta utata mkubwa sana, hata baada ya yeye Ndugu Balali kutoa Barua yake ya kujiuzulu mwezi December, 2007!

Mheshimiwa Naibu Spika, hatimaye kitendo cha Ndugu Balali, Mtanzania, kuweka wosia wa kuzikwa Marekani, nayo imeacha utata na maswali mengi sana vichwani mwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua Ndugu Balali amefariki, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, lakini kwa vile kuna taarifa kuwa Ndugu Balali

ameacha wosia kuhusu nafasi yake katika tuhuma hizi, ukweli hautapatikana isipokuwa kwa Tume au Kamati Maalum ya Uchunguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wakati muafaka Serikali isiachie majungu na umbea kutembea kwa usalama na uhai wa Taifa letu. Itoe mara moja taarifa ya kina kuhusu kifo cha Ndugu Balali, ikiwa ni pamoja na alivyohusika na tuhuma hizi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe, Kambi ya Upinzani, inataka uanzishwe mara moja mchakato wa uchunguzi ili Taifa liweze kufahamu kinagaubaga ni nini nafasi hasa ya Ndugu Balali katika tuhuma zote zilizomkabili, ikiwemo ya *EPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua Ndugu Balali amefariki, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, lakini kwa vile kuna taarifa kuwa Ndugu Balali ameacha wosia kuhusu nafasi yake katika tuhuma hizi, ukweli hautapatikana isipokuwa kwa Tume/Kamati Maalum ya Uchunguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, haiamini kuwa Serikali kwa kila kitu itatufikisha mahali pa kuunda *Select Committee* ya Bunge. Tamko la Waziri Mkuu, kuwa Serikali isipotenda vizuri na kwa uwazi, Bunge litaunda Kamati Teule nyingi, tunamtaka sasa Waziri Mkuu kusimamia kauli yake hiyo aliyotoa ndani ya Bunge lako Tukufu, iundwe Kamati huru ya Serikali na taarifa yake iwasilishwe Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utata kati ya *Tangold/Meremeta* na *Deep Green*, kuna utata mkubwa sana kuhusu matumizi ya fedha katika akaunti za *Tangold*, *Meremeta* na *Deep Green Finance Co. Ltd*. Ili kuwapa picha kamili ya sura hii ya ufisadi, ni vema Waheshimiwa Wabunge, wakaona kwa macho yao kilichotokea na kinachoifanya Kambi ya Upinzani kusisitiza kupata taarifa ya kina kuhusu mambo haya. Taarifa hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *Deep Green Finance Ltd*, ilianzishwa mnamo tarehe 18 Machi 2004. Kwa mujibu wa Taarifa za Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Wakurugenzi wa *Deep Green Finance*, walikuwa ni mabwana Mark Ross Weston wa New Zealand; Anton Taljaard wa Afrika Kusini na Rudolph Van Schalkwyk pia wa Afrika Kusini. Wote watatu ni wakazi wa Afrika Kusini na wanaelekea kuwa ni maafisa na/au wafanyakazi wa *Nedbank Ltd*. ya Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na taarifa za BRELA, wanahisa wa *Deep Green Finance*, ni Mawakili Protase R.G. Ishengoma na Stella Ndikimi wa IMMMA *Advocates; Nedbank Ltd., Nedbank Africa Investments Ltd.* na *SBM Nedcor Holdings Ltd.* Tarehe 15 Aprili 2005, Mawakili Ishengoma na Ndikimi walihamisha hisa zao kwa Nedbank Ltd. na *Nedbank Africa Investments Ltd.*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za kibenki tulizonazo, zinaonyesha kwamba tarehe 1 Mei 2004, *Deep Green Finance* ilifungua Akaunti Na. 011103024840 katika tawi la *Corporate* la Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC),* Dar es Salaam. Kitu cha kushangaza ni kwamba, kampuni hii iliruhusiwa kufungua na kuendesha akaunti hiyo

bila ya kuingiza hata senti moja kwa zaidi ya mwaka mmoja kuanzia tarehe 1 Mei, 2004 hadi tarehe 31 Julai 2005. *(Makofi)*

Hata hivyo, kwa kipindi kifupi cha miezi minne kati ya Agosti 1 na Desemba 2005, kampuni hii ilipokea jumla ya shilingi 10,484,005,815.39 kutoka Wizara ya Fedha na/au *BOT* bila kuonyesha wazi ni biashara gani kampuni hii imefanya na Wizara ya Fedha au *BOT*. *(Makofi)*

Fedha hizo zilitolewa kwa utaratibu ufuatao:-

(a) Tarehe 1 Agosti 2005, *BOT*, kwa kutumia hundi Na.241740, ilihamisha dola za Marekani 1,354,167.26 au shilingi za Tanzania 1,546,778,770.92 kwenda kwenye akaunti ya *Deep Green Finance.* Siku hiyo hiyo, fedha hizo zote zilitolewa kwenye akaunti ya *Deep Green Finance* kwa utaratibu maalum wa haraka *(special clearance)* na katika *cash*, kwa fedha za Tanzania japo zilipelekwa katika Dola za Marekani, jambo linalotia shaka kuhusu malengo ya fedha hizi, hasa ikizingatiwa kuwa waliochukua ni wageni;

(b) Tarehe 1 Septemba 2005, *BOT*, kwa kutumia hundi Na.015558, ilihamisha dola za Marekani 1,827,137.44 au shilingi za Tanzania 2,083,255,881.60 kwenda kwenye akaunti ya *Deep Green Finance*. Siku hiyo hiyo, jumla ya shilingi 2,083,333,333.33 zilitolewa kwa mara nyingine tena kwa kutumia utaratibu maalum wa haraka tena kwa *cash*;

(c) Tarehe 8 Septemba 2005, *Tangold Ltd*. ilihamisha dola za Marekani 100,256.62 au shilingi za Tanzania 114,611,746.80 kwenda kwenye akaunti ya *Deep Green Finance.* Itakumbukwa kwamba *Tangold Ltd.* ni kampuni ya kigeni iliyoandikishwa nchini Mauritius tarehe 5 Aprili 2005 na kupewa Cheti cha Kutimiza masharti ya Tanzania tarehe 20 Februari 2006. Wakurugenzi wa *Tangold Ltd*. ni wale ambao tulikwisha kuwataja hapo kabla.

Kufuatana na barua ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa *BOT* ya tarehe 21 Desemba 2006, *Tangold Ltd.* ililipwa na *BOT* dola za Marekani 13,736,628.73 kwa kupitia akaunti isiyojulikana ya Nedbank Ltd. ya Afrika Kusini na kwa madhumuni yasiyojulikana;

(d) Tarehe 16 Septemba 2005 jumla ya shilingi 129,000,000.00 zilitolewa kutoka kwenye akaunti ya *Deep Green Finance* na kuwekwa kwenye akaunti ya muda maalum *(FDR)*;

(e) Tarehe 3 Oktoba 2005, hundi ya *BOT* Na. 16596 yenye jumla ya shilingi 2,083,333,333.33 za Wizara ya Fedha, ililipwa kwa utaratibu maalum wa haraka kutoka kwenye akaunti ya *Deep Green Finance*. Inaelekea hundi hiyo ililipwa kabla fedha hazijaingizwa kwenye akaunti ya *Deep Green Finance* kwa vile tarehe 4 Oktoba 2005,

*BOT* ilihamisha dola za Marekani 1,789,075.89 au shilingi 2,083,891,765.35 kwenda kwenye akaunti ya *Deep Green Finance;*

(f) Tarehe 8 Oktoba 2005, jumla ya shilingi 39,761,397.98 zilihamishwa kutoka kwenye akaunti ya *Deep Green Finance* kwenda *Tangold Ltd*.;

(g) Tarehe 31 Oktoba 2005, jumla ya shilingi za Tanzania 2,083,333,333.33, fedha za Wizara ya Fedha zilihamishiwa kwenye akaunti ya *Deep Green Finance* kwenda kusikojulikana;

(h) Tarehe 2 Novemba 2005, dola za Marekani 1,821,095.57 au shilingi za Tanzania 2,083,653,279.68 zilihamishwa kutoka kwenye akaunti ya *Deep Green Finance* kwenda kusikojulikana;

(i) Tarehe 30 Novemba 2005, *BOT* ilihamisha shilingi za Tanzania 2,083,333,333.33, fedha za Wizara ya Fedha, kwenda kwenye akaunti ya *Deep Green Finance*. Siku moja baadaye, dola za Marekani 1,817,199.52 au shilingi za Tanzania 2,184,610,383.04, zilihamishwa kutoka kwenye akaunti ya *Deep Green Finance* kwenda kusikojulikana;

(j) Tarehe 10 Desemba 2005, shilingi 100,940,489.71 zilihamishwa kutoka *Tangold Ltd.* kwenda kwenye akaunti ya *Deep Green Finance*. Hii ilikuwa ni siku nne tu kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Desemba 14, 2005 kufanyika nchini kote;

(k) Tarehe 19 Desemba 2005, siku tano baada ya Uchaguzi Mkuu kufanyika, dola za Marekani 88,722.17 au shilingi za Tanzania 104,755,554.09, zilihamishwa kutoka kwenye akaunti ya *Deep Green Finance* kwenda kusikojulikana;

(l) Tarehe 9 Februari 2006, shilingi 3,836,800.00 zilihamishwa kwenda akaunti ya Mawakili wa *Deep Green Finance*, *IMMMA Advocates*, iliyoko benki ya *Standard Chartered.* Haijulikani kama fedha hizi zilikuwa ni kwa ajili ya malipo ya Mawakili hao au la; na

(m) Malipo ya mwisho kutoka kwenye akaunti ya *Deep Green Finance* yalifanywa tarehe 22 Novemba 2006 ambapo jumla ya shilingi 14,465,000.00 zilihamishiwa katika akaunti isiyojulikana ya benki ya *Standard Chartered* na kwa matumizi yasiyojulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na rekodi za kibenki zilizoonyeshwa hapo juu, jumla ya shilingi 10,484,005,815.39 ziliingizwa katika akaunti ya *Deep Green Finance* katika kipindi cha miezi minne tu kati ya tarehe 1 Agosti na 10 Desemba 2005. Hiki kilikuwa ni kipindi cha mchakato na/au kampeni za Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 14 Desemba 2005.

Aidha, kuanzia tarehe 11 Desemba 2005, hakuna fedha yoyote iliyoingizwa katika akaunti hiyo hadi tarehe 27 Februari 2007, kampuni hiyo ilipovunjwa ‘kwa hiari’ ya wanahisa wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kurudia kwamba, kwa ushahidi huu wa nyaraka za kibenki, kampuni ya *Deep Green Finance,* haikuwa na hata senti moja kabla ya tarehe 1 Agosti 2005 na wala haikupokea hata senti tano baada ya tarehe 10 Desemba 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtu yeyote makini, ni lazima kupata tafsiri sahihi ya mchakato huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa za sasa hivi, inafahamika kwamba faili la *Deep Green Finance* lililotakiwa kuwa *BRELA* limetoweka, isipokuwa Hati ya Kufunga Kampuni *(Winding Up)*. Tuna kila sababu ya kuamini kwamba hii ilikuwa ni kampuni hewa *(shell company)* iliyoundwa kwa ajili tu ya kupitishia fedha za umma kutoka Benki Kuu kwenda kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2005. Ndio maana kampuni hiyo haikuwa na fedha zozote benki kutokea tarehe 1 Mei 2004 hadi tarehe 1 Agosti 2005, wiki tatu kabla ya kuanza kwa kampeni za Uchaguzi Mkuu na ndio maana mabilioni yaliyolipwa na Benki Kuu na *Tangold Ltd*. yalilipwa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu na mara baada ya Uchaguzi Mkuu kupita malipo hayo ya fedha za umma yalikoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe ufafanuzi wa kina katika jambo hili. Bunge linapaswa kuelezwa pia ni vipi kampuni ya *Deep Green Finance Co.Ltd.* imekuwa ikifanya kazi kwa kipindi chote hicho bila usajili wa Benki Kuu kama *Financial Institution* kama inavyotakiwa na Sheria ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Tangold Limited*, ni kampuni ya kigeni inayomilikiwa na baadhi ya watu tuliowataja hapo juu. Kuna utata mkubwa zaidi ambao umeigubika kampuni ya *Tangold Ltd.* Kwanza, licha ya nyaraka kuonyesha kwamba kampuni hiyo ilipewa Hati ya Kutimiza Masharti ya Tanzania, tarehe 20 Februari 2006, nyaraka za kibenki tulizonazo, zinaonyesha kwamba *Tangold Ltd.* ilifungua akaunti Na. 011103024852, *NBC Corporate Branch*, tarehe 1 Januari 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyokuwa kwa *Deep Green Finance*, siku ya *Tangold* kufungua akaunti yake ilikuwa ni siku ya mwaka mpya na hiyo ni siku ya mapumziko dunia nzima.

Aidha, taratibu za kibenki za ufunguaji wa makampuni, zinalazimu kampuni husika kuwasilisha benki nakala ya usajili, nakala ya Katiba kabla ya kuruhusiwa kufungua akaunti na Hati ya Mlipa Kodi *(Registration Certificate)*. Taratibu za kibenki

za ufunguaji wa akaunti za makampuni zinalazimu kampuni husika kuwasilisha benki nakala ya usajili wa kampuni na Katiba yake kabla ya kuruhusiwa kufungua akaunti.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kujibiwa na *NBC* pamoja na watawala wa nchi hii ni je, ilikuwaje *Tangold Ltd.* waliruhusiwa kufungua na kuendesha akaunti ya benki kabla hawajaandikishwa nchini Mauritius achilia mbali kupata Hati ya Kutimiza Masharti ya Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 7, cha *Memorandum and Articles of Association*, kinataja wazi kuwa wenye hisa wanaweza kuhamisha hisa zao kwa baba, mke, mtoto na mpwa. Kambi ya Upinzani, inataka Bunge hili lielezwe kama kweli *Tangold*, ni mali ya Serikali kwa asilimia mia moja, baba, mke, mtoto na mpwa wa Serikali ni nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *Tangold Ltd*, iliendesha akaunti hiyo bila kuweka au kutoa fedha yoyote ile kati ya tarehe 1 Januari 2003 hadi tarehe 1 Agosti 2005, ilipoanza kunyeshewa mvua ya neema ya mabilioni ya fedha za walipa kodi wa Tanzania kutoka *BOT*! Mvua hiyo, ni nje ya mvua ya dola za Marekani 13,340,168.37 iliyohojiwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali na iliinyeshea *Tangold Ltd*. kama ifuatavyo:-

(a) Tarehe 1 Agosti 2005, *BOT* ilihamisha shilingi za Tanzania 4,703,221,229.08 kwenda kwenye akaunti ya *Tangold Ltd*. Tarehe hii ni muhimu sana kwani ndiyo siku ambayo *BOT* ilifanya pia malipo ya kwanza kwa *Deep Green Finance* kama ilivyoelezwa katika taarifa hii. Ukijumlisha kiasi hiki na kile kilichohamishwa kwenye akaunti ya *Deep Green*, ni jumla ya Tshs 6.2 billion.

Fedha zote hizi zilichukuliwa kwa *'cash'*. Inashangaza waliozichukua fedha hizi walizebebaje kwani wataalam wanakisia kuwa ni sawa na tani 50 zinazoweza kubebwa tu na lori tano za tani 10 kila moja! Hili linabaki kuwa fumbo;

(b) Tarehe 2 Septemba 2005, *Tangold Ltd*. ilihamisha shilingi za Tanzania 244,428,386.15 kutoka akaunti yake hiyo kwenda kwenye akaunti ya *Deep Green Finance.* Kama tulivyoelezea katika taarifa hii, *Deep Green Finance* ililipwa tarehe 1 Agosti, 2005, Tshs 2,083,255,881.60 na *BOT*;

(c) Tarehe 8 Oktoba 2005, shilingi za Tanzania 39,761,397.98 zilihamishiwa kwenye akaunti ya *Tangold Limited* kutoka kwenye akaunti ya *Deep Green Finance*;

(d) Tarehe 12 Oktoba 2005, *Tangold Ltd.* ilihamisha shilingi za Tanzania 1,690,500,000.00 kwenda Meremeta Limited;

(e) Tarehe 23 Novemba 2005, Tangold Ltd. ilihamisha shilingi za Tanzania 555,300,048.00 kwenda *Meremeta Ltd.;*

(f) Tarehe 10 Desemba 2005, *Tangold Ltd.* ilihamisha shilingi za Tanzania 100,940,489.71 kwenda kwenye akaunti ya *Deep Green Finance;* na

(g) Tarehe 12 Desemba 2005, siku mbili kabla ya Uchaguzi Mkuu, *Tangold Ltd.* ilihamisha shilingi za Tanzania 551,060,000.00 kwenda kwenye akaunti ya Meremeta Ltd.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, *Tangold Ltd.*, haikupokea wala kuingiza fedha zozote kwenye akaunti yake hadi tarehe 6 Juni 2006. Tangu tarehe hiyo hadi leo hii, *Tangold Ltd.*, haijaweka wala kutoa fedha nyingine yoyote katika akaunti hiyo. Kwa maana hiyo, katika kipindi cha miezi minne, *Tangold Ltd.*, iliingiziwa na *BOT* jumla ya shilingi za Tanzania 4,742,982,627.06 na ilifanya malipo kwa *Deep Green Finance* na *Meremeta Ltd.* ya jumla ya shilingi za Tanzania 3,363,531,259.67.

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali muhimu ya kujiuliza kuhusiana na *Tangold Ltd.*, ni haya yafuatayo. Kwanza, ilikuwaje kampuni ambayo haikuwa hata imeandikishwa kisheria ikalipwa mabilioni ya fedha za walipa kodi na/au ya umma na bila maelezo yoyote?

Pili, ilikuwaje Serikali, kupitia kwa aliyekuwa Waziri Karamagi, itoe taarifa ya uongo Bungeni kwamba Ta*ngold Ltd.*, ni kampuni mpya na imeanzishwa ili kurithi mali na madeni ya *Meremeta Ltd.*, wakati makampuni yote mawili yalikuwa yakipeana mabilioni ya fedha za umma wakati wa mchakato wa Uchaguzi Mkuu katika mazingira ya kutatanisha? *(Makofi)*

Tatu, kwa nini malipo ya mabilioni haya yalikoma mara baada ya Uchaguzi Mkuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhuma hizi nzito zinaihusisha moja kwa moja Serikali na watendaji wake wakuu kutokana na mfumo huu wa kuhamisha fedha za umma *(transaction)* bila maelezo ya kutosha.

Aidha, tunawaomba wananchi wa Tanzania wenye mapenzi mema na Taifa letu, waidai Serikali, iwaeleze mabilioni haya yalilipwa kwa ajili gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri Mkuu, kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu mambo yafuatayo:-

(a) Makampuni haya ya *TANGOLD*, Meremeta na *Deep Green* ni ya nani na wanahisa wake ni kina nani?

(b) Serikali inatoa kauli gani kuhusu uwezekano wa uvunjifu wa Sheria ulio dhahiri kutokana na jinsi makampuni haya yalivyosajiliwa, yalivyoanza kazi nchini bila usajili rasmi jambo ambalo ni kinyume na Sheria na kufungua Akaunti Benki siku za Sikukuu jambo linaloashiria kuna udanganyifu, hila za uwizi yaani *'fraud and forgery"*.

(c) Serikali inaeleza nini juu ya fedha nyingi za umma kuchukuliwa kwa *cash*, tena na watu ambao sio raia? Fedha hizo zilihamishwa na *BOT* kwa Dola za Marekani: Je, ni sababu zipi ziliwafanya wageni hao kuzitoa Benki kwa *cash* na walizipeleka wapi? Uzito wa fedha zilizohamishwa tarehe 1 Agust, kwa fedha taslimu ni sawa na tani 50, yaani uzito sawa na lori tano za tani kumi kumi: Je, ni utaratibu fedha za umma kuchukuliwa kwa mtindo huo?

(d) Je, Serikali iko tayari kufanya uchunguzi wa kina kwa kutumia Makampuni yenye sifa na kutoa Taarifa kwa Bunge hili Tukufu au ni hadi Bunge litakapounda Kamati Teule ili kupata ukweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kampuni za *TANPOWER Resources Ltd* na *ANBEM, Kiwira Coal Mines Ltd* ilikuwa mali ya Serikali kwa asilimia mia moja. Kuna utata mkubwa umezuka kuhusu utaratibu uliotumika kubinafsisha Kampuni hiyo na hisa zake kuuzwa kwa Makampuni binafsi kati ya mwaka 2004 na 2005. Kwa taarifa iliyoko, Serikali imebakiziwa hisa zisizozidi asilimia 15 tu kati ya 100 kutokana na ubinafsishaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *ANBEM* ilisajiliwa tarehe 21 June, 1999 na wanahisa waanzilishi wakiwa ni Anna Mkapa wa *S.L.P.* 7652 Dar es Salaam, Mjasiriamali *(Entrepreneur)* na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa wa *S.L.P* 7652 Mjasiriamali kama ilivyo kwa Anna Mkapa. *Memorandum and Articles of Association* ya Kampuni ya *ANBEM* iliandaliwa na Wakili maarufu, (sasa ni Marehemu) *Kapinga & Company Advocates* wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, japo haikuelezwa wazi, inaeleweka wazi kuwa Mama Anna Mkapa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ni Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu hasa pale inapoelezwa kwenye nyaraka hizo hizo za *Brella* kuwa wanakaa *Plot No. 15 Luthuli Road*, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam ambayo inadhaniwa kuwa ni anuani ya Ikulu, Makao ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kampuni ya *ANBEM* pamoja na Kampuni ya *TANPOWER Resources Ltd* iliyosajiliwa tarehe 29 Desemba, 2004 na kupewa Hati ya Usajili Namba 51080, Wakurugenzi wa Kampuni ya *Tanpower Resources Ltd* ni Mama Anna Mkapa, Mheshimiwa Daniel Yona, *Mr.* Evans Mapundi, *Mr.* Joe Mbuna na *Mr.* Nicholas Mkapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Tanpower Resources Ltd* pamoja na *Share holder* wake *ANBEM* akiwemo Benjamin William Mkapa na makampuni binafsi mengine ya *DevConsult International Ltd, Universal Technologies Ltd, Choice Industries Ltd* na *Forsnik Enterprises Ltd* ndizo zinazoonyeshwa kununua hisa kwanza 70 na baadaye kuongezeka kuwa 85 za kilichokuwa *Kiwira Coal Mines Ltd* ambayo hadi wakati huo ilikuwa asilimia 100 mali ya Serikali ya Tanzania kwa niaba ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Tanpower Resources Ltd* ndiyo inayosemekana imewekeana na *TANESCO* mkataba wa muda mrefu ambao inasemekana watauzia umeme Kampuni ya *TANESCO* kwa kiwango cha Dola za Marekani millioni 271, yaani *TANESCO* itakuwa inalipa kiasi cha Shilingi milioni 300 kwa *capacity Charge*, Kampuni binafsi ya *Tanapower Resources Ltd*, nje ya malipo ya matumizi ya Umeme. Kiwango hiki ni kikubwa kuliko hata malipo yanayolipwa na *TANESCO* kwa *Richmond/Dowans* kama inavyoonyeshwa kwenye Mkataba wa tarehe 8 Juni, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo kadhaa hapa yanayotia wasiwasi. Wakati mikataba hii inawekwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, mjasiriamali alikuwa pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa, Daniel Yona, Mkurugenzi mmojawapo wa *Tanpower Resources Ltd* alikuwa ndiye Waziri wa Nishati na Madini. Yeye ndiye aliyekuwa anafanya mawasiliano na Kampuni ya *Kiwira Coal Mines Ltd* wakati wa ubinafsishaji wa *Kiwira Coal Mines Ltd*, kama inavyoonyeshwa na nyaraka mbalimbali mathalan barua toka kwa bwana Evans Mapunda wa *Tanpower Resources Ltd* yenye *Kumb na TPRCL/GEN/2005/06* ya tarehe 4 Januari, 2005/2006 kwenda kwa Mheshimiwa Daniel Yona - Waziri wa Nishati na Madini na kutoka kwa Mheshimiwa Daniel Yona yenye *Kumb.CDA 48/171/01 ya* tarehe 24 Machi, 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna maswali mazito yanahitaji kujibiwa na Serikali:-

(a) Wahusika wakubwa, yaani Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, japo kajiandika Mjasiriamali na Mheshimiwa Daniel Yona - Waziri, japo kwenye barua hakujionyesha kama Mkurugenzi wa *TPRCL*, hapa kuna suala la wazi la *conflict of interest.* Waziri huyo huyo anayekuwa na dhamana ndio huyo huyo anawasiliana na Kampuni ambayo anataka kuiuzia mali ya Taifa. Serikali tunataka itueleze hili, suala la *"conflict of interest"* kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ilizingatiwa vipi?

(b) Kwa vile hakuna ushahidi wowote wa utaratibu ulioonyeshwa wa kubinafsisha *Kiwira Coal Mines Ltd* na hata *tender* haikuonekana, tunaomba Serikali ituambie, Kampuni hii ilibinafsishwa baada ya sheria ya manunuzi ya Taifa: Je, Serikali ilileta hapa kwa utani *Procurement Act* pamoja na *Public Finance Act?* Ni kitu gani kinawazuia Watanzania wasiamini kuwa hapa kulikuwa na suala la matumizi mabaya ya nafasi zao kushawishi *Kiwira Coal Mines Ltd* kuwauzia Kampuni ya *Tanpower* asilimia 85 ya mali ya Watanzania?

(c) Kwa kuingia Mkataba huo wa kuiuzia *TANESCO* umeme unaolipiwa *Capacity charge*, yaani utalipiwa hata bila kutumika, ni vigezo gani vya kiushindani

vilitumika, jambo ambalo ni dhahiri litawagharimu Watanzania ambao hata kabla ya hapo wamekwisha kulemewa na bei ya Umeme? Kama kweli ni Kampuni ya Kiwira kuwa na matatizo ya kifedha, ni kwanini hatua ya awali isiwe ni Waziri wa Nishati kufanya kila jitihada kuikoa Kampuni hiyo na badala yake kuinunua yeye mwenyewe kwa kutumia Kampuni anayomiliki yeye na Mheshimiwa Rais aliyeko madarakani, ambaye wajibu wake wa kwanza ni kulinda na kutunza kwa uadilifu rasilimali aliyokabidhiwa na Watanzania azitunze kama mdhamini?

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili Kambi ya Upinzani inahitaji majibu ya kina sana, kwanza kama haya tuliyoeleza ni ya kweli, Serikali inalielezaje hili la mgongano wa maslahi na kukiukwa kwa sheria ya Maadili ambayo Rais ndiye mlinzi wake? Lakini badala yake yeye ndiye dhahiri anaonekana kuikiuka na hatimaye kubinafsishwa kwa *Kiwira Coal Mines Ltd* bila *Tender?* Kambi ya Upinzani kama haitapata majibu ya kuridhisha, nitaomba iundwe Kamati Teule ya Bunge kutazama mchakato mzima wa kuuza *Kiwira Coal Mines Ltd* kwa Kampuni ya *Tanpower Resources Ltd.* Kambi ya Upinzani pia inaitaka Serikali, ifute mara mmoja mkataba kati ya *Tanpower Resources Ltd* na *TANESCO* ili Watanzania wasije wakaumizwa na gharama kubwa ya *capacity Charge* ya umeme huo utakaotokana na *Tanpower Resources Ltd.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumekuwepo na mjadala mkubwa kuhusu kama Rais mstaafu anaweza kushtakiwa au la kutokana na kinga zinazoelezwa na Katiba Ibara ya 46(1) na (2). Ninapenda kusema kuwa kwa maoni ya wanasheria wengi, Katiba Ibara ya 46(3) iko wazi, kwani inatamka wazi kuwa Rais mstaafu ana kinga na nina nukuu: *"Jambo alilofanya kama Rais wakati alipokuwa anashika madaraka ya Rais kwa mujibu wa Katiba..."*

Hivyo kwa tafsiri iliyoko, Rais mstaafu hana kinga kwa jambo alilofanya yeye kama raia binafsi wakati alipokuwa madarakani. Isitoshe, Katiba Ibara ya 46(2) inaeleza wazi kuwa:

*"Haitaruhusiwa kufungua Mahakamani shauri kuhusu jambo lolote alilotenda au alilolikosa kulitenda yeye binafsi kama raia wa kawaida ama kabla au baada ya kushika madaraka ya Rais, ila tu kama angalau siku thelathini kabla ya shauri kufunguliwa Mahakamani, Rais atapewa au atakuwa ametumiwa kwanza taarifa ya madai…."* Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa kinga ya Rais mstaafu siyo *absolute.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliambia Bunge hili ni hatua gani itachukua dhidi ya Rais Mstaafu na Waziri wake wa Nishati wa Wakati ule ili kuwarudishia imani Watanzania kuwa tuliowaweka madarakani hawatatumia tena nafasi zao kujibinafsishia mali ya Watanzania wote?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *SPM*–Mgololo, Kambi ya Upinzani inasikitishwa na hali ya Serikali kutokuchukua hatua ya kujisafisha kabla ya kuchokonolewa. Ndiyo kusema, Serikali haiyajui haya yote yanayoandikwa na kusemwa na watu mbalimbali?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Mgololo ilibinafsishwa kwa Kampuni ya *RAI Group Ltd* ya Kenya tarehe 16 Januari, 2004 kama inavyoonekana kwenye *Assets Sale Agreement* kati ya *United Republic of Tanzania* na *RAI Group Ltd* (kama nilivyopokea kutoka Ofisini kwako kwa Barua yenye Kumb Na. CEB/147/155/03/09 ya tarehe 19 Juni, 2008) inayomilikiwa na Wakenya wawili Bwana Jaswant Singh Rai na Bwana Sarbjit Singh Rai kila mmoja akiwa na hisa 0.0006% kwa bei ya Dola za Marekani milioni 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo mkataba huu wa mauziano unatisha sana na Kambi ya Upinzani inataka ufafanuzi wa kina katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kifungu cha 3.1 cha Mkataba wa Mauziano unatamka kuwa Bei ya mauzo ni Dola za Marekani milioni 26. Cha kushangaza ni kuwa, mkataba huo huo unaeleza italipwa Dola za Marekani milioni moja siku ya kuwekeana saini na Dola za Marekani milioni tatu zitawekwa kwenye *Escrow Account* ambazo Mwekezaji atazichukua atakapokuwa anatimiza masharti fulani fulani kwa ukarabati wa kiwanda *"chake."*

Fedha nyingine Dola za Marekani milioni 22 atazitumia Mwekezaji kwa kufanyia kiwanda ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi anadanganywa nani? Kama Bei ni Dola milioni moja, kwanini isielezwe hivyo wazi wazi? Hili fumbo maana yake ni nini? Isitoshe, hata kodi ya Serikali imewekwa, kwani mkataba unasema dhahiri kuwa kwa kutimiza matakwa ya ushuru wa *Stamp Duty* kiwango kitakachotumika ni Dola za Marekani milioni moja? Hii maana yake ni nini kama sio kutoa sadaka Rasilimali za Watanzania?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ilikuwa inajiuliza, hivi hawa wawekezaji wenye hisa 0.006% kila mmoja ni kweli wawekezaji na wanaweza kukifufua kiwanda kama kweli kiko kwenye hali mbaya kama Serikali inavyosema?

Utafiti wetu umeonyesha kuwa, kumbe mwenye mali halisi wala siyo *Rai Brothers* kama walivyo kwenye *Sale agreement*, bali ni *Angel Hurst Industries* ya Uingereza yenye hisa 99.988% kama ilivyosajiliwa kwenye Kituo cha Uwekezaji kama inavyoonekana kwenye *Certificate of Incentives No. 00021049* iliyotolewa *TIC* tarehe 19 Aprili, 2004 kwa *Mufindi Paper Mills Ltd* ambayo ndiyo Kampuni iliyosajiliwa baada ya kununua Kampuni ya *Southern Paper Mills (SPM)* ambayo ilikuwa asilimia 100 mali ya Serikali na hivyo mali ya Watanzania wote na kusimamiwa na *NDC* ikiwa na Hati ya *Industrial Licence No. 0907.* Isitoshe, kiwango cha fedha kilichotajwa kwa *TIC* ni Dola za Marekani milioni 52 *(Foreign)* na Shilingi bilioni *9*.251 fedha za ndani yenye jumla ya Dola za Marekani 61.251 na siyo milioni 25 walioyotaja kwenye nyaraka mbalimbali za *Sale Agreement.* Kwanini kuwe na udanganyifu huu mkubwa?

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Kazi katika hukumu yake ya Uchunguzi wa Mgogoro wa Kazi Na. 80/2006 ya *TUICO vs PSRC* na wenzake ilitamka wazi kuwa, sio rahisi kuamini kuwa mali zote za *Southern Paper Mills Ltd* za thamani ya soko la mabilioni, sio chini ya bilioni 500, kwa makisio yangu na si ile thamani ya

Shilingi bilioni 85 iliyotumika kuuzia, ambayo nionavyo ni *token/book price value* tu ambayo mathalan *flat rate ya Trailer Scania* linalofanya kazi lilithaminiwa kwa Sh. 300,000/= kwa kila *Traillor* ambayo ni chini ya bei halisi hata ya tairi lake moja tu.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hali ya kutisha, kwani hata kama tatizo ni kwamba hapakuwa na mnunuzi wa *SPM Ltd,* basi wangeliuza vifaa hivyo kimoja kimoja wangelipata mara kadhaa ya bei waliyopata. Rasilimali zilizouzwa ni pamoja na nyumba zikiwemo za *Grade A,* Kijiji kizima cha Wafanyakazi kama ilivyorikodiwa kwenye Mkutano wa Mashauriano ya Kamati ya *Fast Track* ya Baraza la Mawaziri la tarehe 4 Agosti, 2003. Misiniulize nimepataje, hizi ni *documents* za Mahakamani, wakati wa mgogoro na ni *Public documents*) inayosomeka: “kinachouzwa ni kiwanda, kijiji na eneo la ardhi ambalo bado kuendelezwa la hekta 28,000.”

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu imekuwa sio makini katika ubinafsishaji huu, kama ilivyo kwa mengine mengi. Watumishi zaidi ya 760 bado wanadai haki zao pamoja na hukumu iliyotolewa na Mahakama wanadai zaidi ya Tsh. 2,647,255,816/=. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali isimamie utaratibu unaoeleweka wa kulipwa Watanzania hawa maskini ambao wamejikuta wao na familia zao katika maisha magumu kutokana na maamuzi yasiyo makini ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hayo yote, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali yafuatayo:-

(i) Bunge hili lielezwe *Angel Hurst Industries* ni ya nani hasa na kwanini hawako popote kwenye Mkataba rasmi ?

(ii) Mkataba kati ya Serikali na *RAI Group* utazamwe upya kuondoa utata huu wa Mali ya Watanzania, ikiwemo vifaa vya kiwanda, nyumba, kijiji cha Wananchi na eneo la hekta 28,000 ambazo hazikulipiwa kitu kabisa, ikiwa lazima tathmini ifanyike upya kuangalia bei halisi ya yote hayo na/au Mkataba uvunjwe.

Serikali iangalie ni kwanini Watendaji wetu Serikalini hawakulinda maslahi ya nchi yetu, badala yake waliegemea kwa mwekezaji ikiwa ni pamoja na kuweka Jeshi la Polisi kulinda kiwanda hicho kwa miaka yote kwa kodi ya Watanzania, wakati polisi hao wangeliweza kufanya kazi ya ulinzi na usalama wa Raia? Kuegemea huku kunaonekana hasa katika barua ya Waziri wa wakati huo wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Juma Ngasongwa, yenye Kumb CCD/111/450/01 ya tarehe 14 Agosti, 2005 na tena barua yanye Kumb. Na CCD/111/450/01/33 ya tarehe 8 Septemba, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishawahi kusema ndani ya Bunge hili, kuwa kuna ufisadi mkubwa kupitia mpango wa *Commodity Import Support.* Huu ni mpango wa kuipa Serikali uwezo wa kuimarisha uchumi wake kwa kuzipatia taasisi, makampuni, viwanda na biashara mbalimbali katika kipindi cha miaka ya 1980 hadi 2004.

Katika mpango huo, Wahisani mbalimbali wakiwemo Serikali ya Japan ilitoa fedha nyingi za kigeni kwa mpango huu na *BOT*/Hazina kusimamia fedha hizo na wajasiriamali kuruhusiwa kuagiza bidhaa au huduma kutoka nje ya nchi na Serikali kupitia *BOT/*Hazina kulipia kwa fedha za kigeni. Wajasiriamali walitakiwa kukopa bila riba, ila iwapo atashindwa kulipia atatakiwa kulipia asilimia 17 kama riba ya thamani ya mali au huduma walizokuwa wanaagiza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizokuwa zinalipwa na wajasiriamali zilitakiwa kuingia kuimarisha Bajeti ya Serikali, pamoja na miradi maalum ya maendeleo kama ilivyokubaliwa katika mkataba kati ya Serikali na Wafadhili waliochangia mpango huo. Matatizo ya Mpango huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, mimi sina tatizo na waliokopa fedha kupitia mpango huu. Kukopa ni deni na mkopaji anatakiwa kulipa, kama sio leo, kesho kwa utaratibu wowote wa kisheria kama ni lazima. Hivyo sina tatizo kuwa hizi fedha ni za mkopo hivyo Serikali itaendelea kuwadai wahusika.

(ii) Tatizo langu la msingi ni taarifa kuwa kuna utapeli na ufisadi mkubwa jinsi fedha hizi zilivyokopeshwa na au kuidhinishwa na/au kutolewa. Nyaraka nilizonazo zinaoonyesha kuwa:-

(a) Kati ya makampuni 980, mengi yalianzishwa tu kama chambo cha kupatia fedha hizo na mengi ya kampuni hizo au yamekwishafungwa na hayako tena, au yamefilisika na/au yalikuwa hewa jambo ambalo linaonyesha kuwa kulikuwa na uzembe mkubwa sana katika Serikali, kwani mikopo hiyo au ilitolewa bila uchambuzi wa kutosha, au kulikuwa na ushirikiano kati ya viongozi wa Serikali hasa Hazina na *BOT* walioidhinisha ukopaji huo na au uwizi wa moja kwa moja, kupitia kampuni moja ya ushauri.

(b) Taarifa zinaonyesha maajabu kuwa, kwa mfano Kampuni moja ilipata mikopo kupitia makampuni hewa 35. Fedha za umma zilichukuliwa kupitia makampuni haya hewa na hivyo kufanya fedha hizo zisilipike kabisa au kuwa ngumu kabisa kulipika.

(c) Majina mengine yakiwemo ya Wabunge, au walioanzisha makampuni au walipata vibali na kuviuza vibali vyao kwa wajasiriamali wajanja na wao kulipwa kiasi fulani tu cha fedha, au kwa kuelewana, au kwa kudanganywa na kuhujumiwa.

(iii) Matokeo ya haya yote, ni fedha za umma zaidi ya shilingi bilioni 900 zilichukuliwa kwa njia hii na waroho hawa wachache kwa njia hii ya ufisadi. Taifa limepata hasara kubwa kwa vile fedha hazikufanya kazi zilizokusudiwa, hazilipiki kwa vile makampuni mengi ni hewa na/au utaratibu haukuwa makini kwa makusudi au kwa uzembe. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutoa Taarifa ya kina kuhusu hatima ya fedha hizi zilizochotwa kupitia utaratibu huu, ikitenganisha zilizokopwa kwa utaratibu halali na zile zilizokopwa kupitia makampuni hewa, ambayo inasemekana makampuni zaidi ya 400 kati ya 980 yalikuwa hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inastushwa na usiri ulioko Serikalini na hasa usiri unaohusiana na Taarifa mbalimbali za Kamati zinazoundwa na Serikali (Waziri Mkuu) na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ilipotoa jukumu la kusimamia Serikali kwa Bunge, haikuweka mpaka wowote. Hii ni kwa sababu kazi zote anazofanya Mheshimiwa Rais zinafanyika kwa kutumia fedha za wananchi kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, yaani *Consolidated Fund.* Hivyo, Bunge linapaswa kujua matokeo ya Tume na Kamati hizo ili kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika miaka sita iliyopita zimeundwa Kamati tano kuchunguza madini. Hadidu rejea za Kamati hizo karibu zote zinafanana. Kwa mfano Kamati ya Kipokola, Kamati ya Masha, Kamati ya Generali Mboma na sasa Kamati ya Bomani. Ripoti ya Kamati zote zimewasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na hakuna Taarifa kwa umma wa Tanzania, wala kwa Bunge. Taarifa zote hizo hazijafanyiwa kazi na hakuna anayejua kama ziko kwenye *Shelf* za Rais, au zimejaa buibui mahali fulani kwenye kona ya Ikulu *(Makofi).*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu!

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(d) pamoja na (g), nikianza na hii Kanuni ya 64 inasema: *"Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge."* Kipengele (d) kinasema: *"Hatotumia jina la Rais, kwa dhihaka katika mjadala au madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge, kuamua jambo lolote kwa namna fulani"*. kifungu (g) kinasema ifuatavyo, *"Hatotumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine."*

Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji katika taarifa yake aliyoiwasilisha sasa hivi, amelitumia jina la Rais, kwa namna ya kutaka kulishawishi Bunge na pia imekuwa ni namna ya kudhalilisha, pale aliposema taarifa zote hizo hazijafanyiwa kazi na hakuna anayejua kama ziko kwenye *shelf* za Rais, au zimejaa buibui mahali fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hiyo ni kauli ambayo sio kauli ya kistaarabu na hasa kwa kutumia jina la Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, naomba muwasilishaji afute kauli hii au athibitishe ukweli wa kauli yake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda tumalize hii *discussion* iliyopo hapa. Majibu yatatolewa. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, nilimalizia hapo, naomba nirudi tena. Ninauliza swali na Serikali inatakiwa kujibu. Taarifa zote hizi hazijafanyiwa kazi na hakuna anayejua kama ziko kwenye *Shelf*

za Rais, au zimejaa buibui mahali fulani kwenye kona ya Ikulu. Kwa kawaida *documents* huwa zinakaa kwenye kona fulani na hii haihitaji kuthibitishwa.

Mheshimiwa Spika, ataarifa ya Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Lowassa kuchunguza ujenzi wa maghorofa *Dar es Salaam*, baada ya *Hotel ya Chang'ombe Village* kuanguka, nayo haijatolewa Taarifa. Taarifa hii haijulikani nini mapendekezo yake. Hakuna utekelezaji uliofanyika wa mapendekezo ya Kamati hizo, huku majengo mengine yakiendelea kuporomoka kama ilivyotokea Kisutu juzi tarehe 21 Juni, 2008 Jijini Dar es Salaam. Kambi ya Upinzani inaona haya ni matumizi mabaya ya kodi za umma na hakuna Kamati inayofanya kazi bila kutumia mabilioni ya fedha. Huu ni ulaji mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile hakuna taarifa rasmi, tunawajibika kufanya makisio tu. Kamati ya Bomani imekwenda Zambia, Australia, Canada, Ghana kwa taarifa tulizopata kwenye vyombo vya Habari. Kamati imezunguka karibu nchi nzima, mathalan maeneo yote yenye madini. Kwa tafsiri rahisi, haya ni mabilioni ya fedha ambayo yangeweza kutumika kujenga shule, zahanati, mabweni na/au kutoa chakula kwa watoto wetu ambao sasa wengi wamefunga shule kwa kukosa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema basi, Waziri Mkuu akaliarifu Bunge lako Tukufu, baada ya kuwa Waziri wa Fedha hakugusia chochote, Kamati ya Bomani imetumia shilingi ngapi na Wakaguzi wa *EPA* wamelipwa kiasi gani? Hizi ni fedha za wananchi, ni lazima zitolewe taarifa kwa chombo chao ambacho ni Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imetishwa zaidi na taarifa iliyosambaa katika mtandao inayoonyesha kuwa Taarifa hizo za Kamati ya Rais, ambayo ni siri kubwa kwa Wabunge na kwa Watanzania, tayari inajulikana na watu wa nje wakiwemo wawekezaji. Kambi ya Upinzani imefadhaishwa sana na taarifa aliyoitoa *CEO* wa Kampuni ya *Tanzanian Royalty Exploration Corporation* - Bwana James E. Sinclair Mwenyekiti na *CEO* ya tarehe 30 Mei, 2008 yenye kichwa cha habari, naomba kunukuu:-

*"Changes to Tanzanian Mining Law Certain to benefit Mineral Exploration."* Na pia ya tarehe 11 Juni, 2008 yenye kichwa cha Habari:"*A Special Note to Shareholders.*" Taarifa ya Bwana Sinclair ya tarehe 30 Mei, 2008 inatamka wazi kuwa: "*I have had the privilege of reviewing the Committees Recommendations-along with comments from the Chamber of Mines –and have no serious issues with them… What is important to know, however is that the man who will make the final decision on the recommendation is the President not the Committee."*(na) *"As one might expect, any legislation involving such an important segment …has generated heated debate. In my opinion, a small percentage of this rhetoric is instigated by special interest groups in the west whose commentary reads like … a standard play book*".

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani hizi ni dharau kubwa kwa Watanzania, matusi kwa Wabunge na pia inajenga picha kuwa Wabunge wanaopiga

kelele kuhusu mali na rasilimali zao sio watu wanaoweza kufikiri wenyewe bali wanatumika na watu wa Magharibi. Matusi haya hayawezi kuvumilika. Hivyo basi, tunamtaka Bwana Sinclair aombe radhi kwa Bunge hili na Watanzania wote kwa ujumla, kwa kuwa anawekeza hapa Tanzania, ni vyema akawasiliana na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiburi hiki amekipata baada ya Bunge lako Tukufu kudharauliwa kwa kunyimwa Taarifa muhimu kama hii. Hivyo Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuacha mara moja tabia ya kuthamini vyombo na watu wa nje na Wabunge wawe wa kwanza kupata taarifa muhimu za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwasilishe mara moja Bungeni katika kipindi hiki cha Bunge Taarifa ya Kamati ya Bomani, pamoja na Taarifa zote za Kamati za awali ili Wabunge waweze kutimiza majukumu yao ya kuisimamia Serikali. Tumekwishasema mara nyingi, Wabunge ni watu wazima, waliokula kiapo, wanajua kutunza siri kwa vile na wao ni Wazalendo, hivyo suala la siri haliwezi kuwepo kwa Wabunge vinginevyo kiapo wanachokula hakina maana yeyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtu yeyote mnyoofu, mkweli na anayefanya upembuzi yakinifu wa hali ya siasa ya Tanzania atakubali leo kuwa hali ya siasa ni tete. Tusijidanganye kwa kusema kila mara kuwa hali ya kisiasa nchini ni shwari. Tusipojiangalia na kuwa makini tutakuwa tunacheza mchezo wa mbuni wa kuficha kichwa kwenye mchanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kukicha kuna taarifa ya mgomo kwenye shirika hili au lile kutokana na wafanyakazi au kunyanyasika au kunyimwa haki zao au kubaguliwa kama ilivyo kwa hoteli ya *Wildlife Lodge* kule Ngorongoro ambako wafanyakazi wanatengwa na mwajiri kwa msingi wa kwamba kama aliyeajiriwa ni baba, basi mama na watoto hawatambuliwi na hivyo hawatakiwi katika kambi ya hoteli. Huu ni ubaguzi, haikuwepo katika ofisi yetu na ipigwe marufuku mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka maeneo mbalimbali ya nchi, kuna taarifa ya wananchi kuvamia vituo vya Polisi na wakati mwingine kuondoka na Wahalifu, au kuwapiga hadi kufa. Pamoja na kuwa Kambi ya Upinzani haikubaliani na hali hii ya jamii kujichukulia sheria mikononi na inaikemea, lakini hii ni kielelezo cha wazi kuwa hali sio shwari nchini kama tulivyozoea. Watanzania walio wengi, takriban asilimia 18 hawana uhakika wa mlo wao wa siku. Baba na Mama Lishe kila kona ya nchi wananyanyasika kwa vyakula vyao kumwagwa kinyume na utaratibu na/au watu kubomolewa makazi yao bila utaratibu makini.

Mahakamani, Polisi na hospitalini kuna taarifa za haki kununuliwa kama karanga kutokana na matendo ya rushwa yaliyokithiri. Matukio ya wanafunzi kugoma au kupiga waalimu na kufanya uharibifu kwa mali za shule yanazidi kuongozeka mambo ambayo tulikuwa tukiyasikia kwa nchi jirani. Haya yote, kwa vyovyote hayafanyi hali ya siasa kuwa shwari. Kila kukicha matabaka yanazidi kujengeka au ya walio nazo na wasio nazo;

watu wanazungumza zaidi na zaidi kwa misingi ya kikanda au ya kiudini, hii sio hali tuliyozoea Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikio la kufa huwa halisikii dawa. Serikali inaelekea kufanya mzaha na hali ya mpasuko wa kisiasa Zanzibar. Kidole kikiumwa, mwili mzima huathirika. Mpasuko wa Zanzibar kwa vyovyote vile una athari kubwa kwa jamii nzima ya Watanzania. Kwa Mheshimiwa Rais kutokuchukua nafasi yake katika kutafuta suluhu ya kudumu kwa mpasuko wa Zanzibar ni kutokutaka kutambua hali halisi ya siasa Zanzibar na athari yake kwa jamii yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kuachia mazungumzo kwa vikao 21 katika miezi 14 wakati mabilioni ya fedha za wananchi zimeteketea kwa vikao ambavyo *CCM* na *CUF* toka mwanzo haikuwa na nia ya kuvifikisha kwenye hatima kama inavyothibitishwa na hoja ya Kura ya Maoni, kama ilivyowasilishwa kwenye *NEC* Butiama na hasa Kamati ya Muafaka inapopeleka hoja kuwa, nanukuu: *"Kwa hili CCM imeipiku CUF"* Hivi tunafanya vitu kwa kupiku mwingine? Hili ni jambo la kusikitikiwa na wote wenye uchungu na nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya malengo makuu kwa mwaka wa fedha 2008/2009 ni pamoja na kuwezesha na kudumisha hali ya utawala bora wenye kuzingatia demokrasia, usawa na haki. Waziri Mkuu ndiye msimamizi mkuu wa shughuli zote za Serikali na mratibu wa Wizara, Idara na vyombo vyote vya Serikali za Mitaa. Kambi ya Upinzani inadhani Ofisi ya Waziri Mkuu ina nafasi kubwa sana katika kusimamia, kuimarisha, kukemea na hata kurekebisha pale ambapo kuna dosari katika masuala yote ya Utawala Bora na Haki za binadamu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala bora ni pamoja namna yetu ya kutenda kazi na kutoa huduma. Siku hizi hata barua hazijibiwi na Wizara au idara mbalimbali za Serikali na kama wanajibu ni kwa kuchelewa sana na hii ni pamoja na kuwa na *clients charter* na hata pale sheria zinapotoa muda maalumu, mathalan sheria ya uwekezaji. Utawala bora na haki za binadamu zisipoheshimiwa na kusimamiwa kikamilifu, yote tunayofanya yanapoteza maana, kwani maendeleo yote ni kwa ajili ya binadamu. Hivyo basi, Serikali itoe ufafanuzi katika maeneo yafuatayo:-

(i) Mauaji ya maalbino na wazee ni baadhi ya mambo yanayoaibisha Tanzania katika karne hii ya Sayansi na Teknolojia. Hata hivyo, cha kushangaza ni kuwa, iwapo ndani ya Bunge lenyewe mjadala wa uchawi ulishika kasi takriban kwa wiki nzima, hali ikoje huko nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumteua mwakilishi wa Maalbino Bungeni ni kitu kimoja na kizuri cha kupongeza, lakini kuchukua hatua na/au kusimamia kwa umakini sheria zinazolinda haki za binadamu ni kitu kingine. Kambi ya Upinzani inaamini Serikali haijasimamia kikamilifu sheria zilizoko kukomesha kabisa mauaji ya wazee na Albino.

Inatisha kusoma Taarifa ya *RPC* Mwanza – Ndugu Zeloth Stephen kuwa katika miaka miwili iliyopita wazee 238 wameuawa kwa imani ya kichawi (*LHRC/2007 page*

*21*). Mauaji haya yako zaidi Mikoa ya Kagera, Shinyanga, Mara na Tabora. Kulikoni? Mheshimiwa Waziri Mkuu ni vyema akalieleza Bunge hili Tukufu ni mkakati gani wa dhati wa kutokomeza janga hili linaloendelea kumaliza maisha ya wananchi wetu? *(Makofi)*

(ii) Taarifa mbalimbali zinaonyesha kwamba kuna unyanyasaji unaotokana na maamuzi mabovu katika ngazi ya Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya, kama vile utekelezaji usio na mpango wa kuwaondoa Wamachinga na akina mama na baba lishe ambayo imewasababishia upotevu wa mali na kuwarudisha katika lindi kubwa la umaskini na upotevu wa mali pamoja na wengi kukosa kazi na hivyo familia zao kuathirika sana.

(iii) Unyanyasaji wa Wafugaji uliotokea Ihefu mwezi Machi, 2006 kwa kuwaondoa bila utaratibu wala mipango mathubuti, wananchi hawa kutoka bonde la Usangu/Ihefu Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya, bado umeacha makovu mengi kwa wananchi wengi waliopoteza mali zao, mifugo, familia na kuumia kisaikolojia.

Tume ya Rais, iliyotumia mamilioni ya fedha za Watanzania iliyoongozwa na Mheshimiwa Jaji Chande hadi leo taarifa yake imewekwa makabatini na wala Watanzania hawakujulishwa kilichojiri na wala hatua iliyochukuliwa kwa wale waliotekeleza vibaya agizo la Serikali. Mkuu wa Wilaya ya Mbarali peke yake anasemekana kuhusika na matumizi yasiyo na maelezo ya zaidi ya Shilingi bilioni moja. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe Tamko la Serikali kuhusu Taarifa ya Tume/Kamati ya Rais iliyochunguza matukio ya Ihefu ili Watanzania waamini kuwa Serikali yao inawajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko pia Suala la adhabu ya kifo *(death penalty)*, bado halijafanyiwa kazi vya kutosha na Serikali yetu. Hadi mwaka 2007 nchi 133 duniani zilikuwa zimekwishafuta adhabu ya kifo na nchi 64... *(Hapa kengele ililia)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya kwanza hiyo.

**MHE. DR. WILBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi 64 ikiwemo Tanzania bado. Tunaomba sisi tujiondoe mapema iwezekanavyo kwa kufuta hiyo *death penalty* na zibaki 63, sisi tuweze kuweka rekodi. Bunge hili lilijulishwa kuwa Serikali bado inakusanya maoni ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka sasa Serikali kuliarifu Bunge hili matokeo ya utafiti huo. Sababu nilizotoa kufuta adhabu hiyo katika hotuba yangu ya mwaka jana bado ziko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa tamko lake leo asubuhi kuhusu Madiwani. Naamini kabisa baada ya kuwasaidia Madiwani, basi Serikali sasa itafikiria Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Mitaa na wa Vitongoji ambao ndio injini kubwa ya maendeleo na hela nyingi sasa ndiko zinakopelekwa. Hawa

tusipowasaidia matumizi ya fedha zetu hatutaweza kuyadhibiti na hayatakuwa mazuri. Ni nini tunaweza tukafanya? Najua wako wengi, basi ni suala la Serikali kuliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Desemba, 2008 tutakuwa tumekamilisha miaka mitatu kamili tangu Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika mwaka 2005. Mwaka kesho, 2009 tunaingia kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri Mkuu kutoa ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

(i) Nafasi nyingi katika Serikali za Mitaa zimeripotiwa kuwa wazi na wasimamizi wa uchaguzi wa ngazi hiyo, yaani Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri wamekuwa hawachukui hatua za kujaza nafasi zilizo wazi katika ngazi ya Wenyeviti wa Vijiji kama vile Kijiji cha Kambi ya Simba Wilayani Karatu, vijiji kadhaa vya Mpanda Kati, Wenyeviti wa Mitaa na hata Wajumbe wa Serikali.

Kambi ya Upinzani inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu kuliarifu Bunge kwamba hadi leo ni nafasi ngapi kwa kila ngazi ziko wazi? Ziko wazi kwa muda gani hadi sasa? Je, ni sababu zipi za msingi zimewafanya wasimamizi hao kutojaza nafasi hizo?

(ii) Kuna Taarifa kuwa hata pale uchaguzi ulipofanyika, wasimamizi kama vile Msimamizi wa Kijiji cha Ido Wilayani Mpwapwa, Pashungu Mbeya Vijijini ambapo upinzani ulipata viti saba na kimoja cha *CCM*, lakini baada ya miezi minne Mkurugenzi akaenda kufuta matokeo, japo hana mamlaka ya kisheria. Vitongoji vya Nanjilinji ‘A’ na Nanjilinji ‘B’ Wenyeviti wa Vitongoji walifutwa na hadi leo nafasi zao ziko wazi. Kijiji cha Nakiu, Serikali yote ya kijiji nayo imefutwa na hadi leo kijiji hakina uongozi uliochaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakurugenzi wamekuwa wakifuta matokeo ya uchaguzi kinyume na utaratibu wa Sheria. Mahali pengine vijiji vya upinzani vimekuwa vikizuiliwa maendeleo yao kwa misingi ya kisiasa kama ilivyotokea Kijiji cha Gongali Wilayani Karatu au Nanyanje Wilayani Lindi ambapo Shule ya Sekondari iliyokuwa imeanza, watoto wamehamishwa kwa vile imejengwa katika eneo la upinzani. Ofisi ya Waziri Mkuu imechukua hatua gani kuzuia hali hiyo inayochafua misingi ya utawala bora na imewachukulia hatua gani Wakurugenzi hao wanaojichukulia sheria mikononi mwao? Kahama nako Serikali ya Kijiji cha Kakola imetafuta fedha zake, wamejenga Soko la kisasa. Mara baada ya kukamilika *DC* amefika na Polisi kuikabidhi kwa *CCM*, Wilaya kama mali ya *CCM*. Hivi ni vituko.

(i) Kwa vile Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2009 hauko mbali tena, maandalizi yapi yanafanyika na wadau mbalimbali wameshirikishwa kwa kiasi gani?

(ii) Kwa vile kuna maeneo mengi yenye utata kwenye Katiba: Je, Serikali inafikiria nini kuhusu kuanzisha mchakato wa kufanyia Katiba yetu marekebisho makubwa kwa kushirikisha wadau wote, hasa ikizingatiwa kuwa ni jambo la kawaida siku hizi kusikia hata Idara za Serikali zikilalamikia mapungufu ya Katiba, mathalan *CAG*?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania waliweka saini Azimio la *AU* kuhusu wanawake kuwa asilimia 50 katika nafasi za maamuzi na uongozi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliarifu Bunge lako Tukufu hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya Bunge letu kufikia 50/50 katika Uchaguzi Mkuu wa 2010. Wadau wameshirikishwa kwa kiasi gani katika maandalizi hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Kambi ya Upinzani imeufanya mjadala wa kuhamisha Makao Makuu Dodoma ni mjadala wa kila mwaka, Kambi ya Upinzani inataka kujua mwaka huu pia, ni hatua zipi mahususi zimefanya kuhamishia Makao Makuu Dodoma? Je, kwa hatua hiyo, Serikali itakuwa imefikia asilimia ngapi ya malengo ya kuhamisha Makao Makuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali za Mitaa ni vyombo muhimu sana katika uongozi wa nchi kwa vile vyombo hivi viko karibu na watu na ndiyo ngazi inayokutana na wananchi kuliko ngazi nyingine zote. Katika hotuba yangu ya mwaka jana nilizungumzia mambo mengi ikiwa ni kuhusu namna ya kuimarisha vyombo hivi. Ninaomba nirudie tena machache mwaka huu, kwa lengo la kutoa mchango wa Kambi ya Upinzani katika kujenga Serikali imara za Mitaa na hivyo kujenga demokrasia ya kweli nchini mwetu. Mambo haya ni kama yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema, Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji, Madiwani na viongozi ambao mchana kutwa na usiku kucha wako kazini kusimamia programu zote zinazobuniwa na Serikali Kuu na Halmashauri, bado wanatakiwa kubuni mipango na miradi inayohusiana na maeneo yao. Hawa ndio walinzi wa amani na usalama katika maeneo yao. Ni dhahiri basi, hawa ni viongozi muhimu sana katika nchi yetu.

(b) Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kubuni mpango maalum wa kuwawezesha viongozi hawa kujengewa uwezo ili waweze kusimamia vizuri zaidi rasilimali nyingi zilizopelekwa chini na Serikali Kuu kupitia Programu hizi za kitaifa. Sio mara nyingi kusikia viongozi hawa wakienda Semina, Warsha au Kongamano, lakini sisi viongozi wa juu kila wakati tuko kwenye Semina, kuanzia Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wabunge. Ni vyema sasa tukapunguza Semina katika ngazi ya juu na tukazielekeza chini.

(c) Wenyeviti wa Vitongoji, vijiji, na Madiwani wawekewe mpango mzuri wa kuwapatia kipato cha uhakika, angalau kwa kiwango cha kima cha chini cha mshahara Serikalini. Haiwezekani mtu anayesimamia fedha na rasilimali nyingi kama zinavyopelekwa fedha za program zilizotajwa na yeye maisha yake yawe ya kubangaiza. Ni lini matokeo ya Kamati ya Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa iliyokuwa inaandaa mapendekezo ya maboresho ya maslahi ya Madiwani itatangazwa rasmi?

(d) Mheshimiwa Spika, siku za karibuni magazeti mengi yameripoti ubadhirifu unaofanywa katika ngazi za Vijiji. Yote haya kimsingi ni kwa sababu nafasi za vishawishi zimekuwa nyingi zaidi, tofauti na huko nyuma ambapo programu zilikuwa zinatekelezwa na kusimamiwa na ngazi za Wilaya. Vijiji viko chini ya 13,000 na Kata

ziko kama 2,500. Tukiwa na nia, hatutashindwa kuwalipa angalau mshahara wa kima cha chini viongozi hawa. Ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

(e) Tukisimamia vizuri fedha nyingi kama zinavyoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kila mwaka na kubuni vianzio vipya kama vilivyoonyeshwa na Waziri Kivuli wa Fedha, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa tutapata fedha za kutosha kuwalipa hawa viongozi wetu kwa kuanzia bila hata kwenda kuomba fedha kwa mfadhili. Wafadhili wakitusaidia itakuwa ni nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira na uzalendo ndicho kitu kinachotakiwa.

(f) Watendaji wa Kata ambao ni waratibu wakubwa wa maendeleo, wanaosimamia amani katika maeneo yao, wanamsaidia Mkurugenzi wa Wilaya *(DED)* katika utekelezaji wa majukumu yake. Hawa, wanahitaji vyombo vya uhakika vya usafiri mathalan pikipiki. Ni vyema Serikali ikabuni mpango wa kudumu *(sustainable programme)* wa kuwasaidia Watendaji hawa kupata vifaa hivi, hata kama ni kwa kuwakopesha kama tunavyofanya kwa Wabunge na kukata kwenye mishahara yao. Kimsingi hawa ndio wanaofanya kazi nyingi zaidi kuliko hata Makatibu Tarafa ambao tumewapatia pikipiki tayari. *WEO* wako karibu zaidi na maeneo ya kazi na Makatibu Tarafa wana umuhimu wa uratibu tu. Uratibu hauna tija iwapo mzalishaji hana tija.

(g) Serikali itazame upya sheria Na.7 na Na.8 ya Mwaka 1982 na kuweka wazi zaidi majukumu ya Wakuu wa Wilaya, kama kufuta nafasi hizo zimeshindikana, ili kuleta tija zaidi kati ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya *(DED)* ambaye ndiye mwenye Wataalam na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ambaye kimsingi ina viongozi wakuu wasiozidi watatu. Sheria zinazoongoza Serikali za Mitaa pamoja na Sheria ya *Regional Administration* inayounda Ofisi ya Mkuu wa Mkoa zirekebishwe haraka sana kuendana na mabadiliko makubwa yanayotokea sasa na kwa kuzingatia Mpango wa Maboresho.

(h) Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya wadau kwa siku nyingi ni kuwa ili uchaguzi katika ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa uonekane na utendeke kwa haki na huru, ni kurudishwa chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na utumie pia Daftari la Kudumu katika kujiandikisha badala ya kuwa na utaratibu wa sasa ambao unaruhusu udanganyifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kufahamu kwa kina kauli ya Serikali juu ya mapendekezo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatoa rai kuwa, ili tufanikiwe katika mipango yetu ya maendeleo yetu, ni lazima tuondokane na dhana ya itikadi katika masuala yanayogusa maslahi na ustawi wa Taifa, hayajui itikadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tumefurahishwa sana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambayo kwa mara ya kwanza katika kipindi changu cha kuwa Mbunge, nimeona inaunganisha Watanzania. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ni barabara tu, haijali chama na watu wa vyama vyote wanapita. Maji hayana sura na wananchi hawatajali chama bali wataangalia nani kawaongoza kupata maji?

Hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ndiyo Mratibu wa Vyama vya Siasa, ni vyema ikaandaa utaratibu wa kujenga imani kwa Watanzania kufanya kazi pamoja bila kuangalia itikadi za kisiasa. Utamaduni wa amani na mshikamano hujengwa, hauji tu kwa miujiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yetu kuwa Waziri Mkuu atakuwa kiungo kati ya Serikali na Vyama kama malengo ya Ofisi yake yanavyoeleza na atapanga mapema iwezekanavyo kukutana na Vyama vya Siasa ili kubadilishana mawazo na viongozi wa Vyama mbalimbali vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kupata Taarifa na majibu ya kina kuhusu hoja hizi. Mwenyezi Mungu atupe busara zake kama tunavyoomba kwenye Dua kila siku asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii, na pia nawashukuru waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. Aah, naomba kuwasilisha. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Wenzako hawakukuunga Mkono! *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona, muda uliobakia sasa ni dakika 45, kwa hiyo, nitakuwa na wasemaji watatu tu. Nitaanza na Mheshimiwa John Samwel Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Dayana Mkumbo Chilolo na hao watakuwa wanatosha kwa leo.

Mheshimiwa Mzee, John Malecela. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafsi hii ya kuwa msemaji wa kwanza katika mjadala huu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kama alivyoiwasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na kumhakikishia kwamba Chama cha Mapinduzi na Watanzania wote watakuwa naye bega kwa bega katika kuona kwamba sera za Chama cha Mapinduzi zinatekelezwa kwa ukamilifu kama tulivyozipanga na kwamba sisi Wabunge, tutampa kila ushirikiano. Lazima niseme hili kweli, kwamba Waziri Mkuu, ameanza vizuri na aendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, ningependa niwarudishe kwenye ajenda ya sasa hivi, nayo ni hotuba ya Waziri Mkuu ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake. Kwa sababu haya mengine yote yaliyosemwa tunaweza tukayachukua kama

ajenda ya siku nyingine, lakini kwa leo tuna ajenda ya hotuba ya Waziri Mkuu. Narudia tena hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ningependa na mimi niseme moja au mawili. Ninataka kulihakikishia Bunge hili na Watanzania wote kwamba Chama cha Mapinduzi kamwe hakitaficha maovu na kwamba Chama cha Mapinduzi, kila mara kitakuwa katika mstari wa mbele wa kuona kwamba uovu unaondolewa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye hatua za kweli, nani aliyeyaleta haya mambo ya *EPA* mara ya kwanza? Alikuwa ni Mheshimiwa Dr. Chegeni wa Chama cha Mapinduzi, kutoka Jimbo la Busega.

Halafu jambo la pili nitoe mfano tu, juzi hapa nyinyi wenyewe mliona Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Mbunge wa Same Mashariki amesema kwa nguvu zake zote, tunaye pia Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu - Mbunge wa Kishapu amesema kwa nguvu. Kwa hiyo, ninataka niwahakikishie kwamba, hata mimi ninarudia tena, hela za *EPA* zitarudi. Lakini nataka niseme kwamba, jamani hili suala la hela za *EPA* sifa tumpe Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Jakay Mrisho Kikwete, ndiye aliyeyaona maovu haya na yeye ndiye aliyeunda hiyo Tume ambayo tunasomewa hapa vipande na akaahidi kwamba itakapokuwa tayari ataileta kwenye Bunge hili tuje tuizungumze kihakika.

Sasa mimi nashangaa kwamba kitu ambacho Rais alikiunda na tunamshukuru sana na tunampongeza kwamba alichukua hatua ya Chama cha Mapinduzi kupambana na ufisadi na akasema kwamba hela zote lazima zirudishwe chini ya *EPA* na ripoti italetwa Bungeni, tutaizungumza. Sasa wenzetu kama wanataka, wangoje. Naona wanafanya haraka mno.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu! Nataka kusikiliza kuhusu utaratibu.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68.

**WABUNGE:** Isome!

**NAIBU SPIKA:** Naomba uisome Kanuni.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kama huna kanuni, wewe shauri yako. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua kama ni utaratibu kuzungumzia… *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wangwe, tafadhali soma kanuni.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaisoma. Wengine hapa hawasomi, Kanuni ya 68 inasema: "Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa?" (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Sasa ndiyo hiyo! Taja sasa. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kanuni ambayo imekiukwa ni Kanuni ya 68 (7) inasema: "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema." *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge naomba usipoteze muda, Mheshimiwa Mbunge … *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ngoja .... *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wangwe kaa chini. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, naomba unilinde nimalizie. Nilikuwa nauliza Kama ni sahihi kuzungumzia mwenendo wa Rais … *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge nimesimama, naomba ukae chini. Mheshimiwa Chacha Wangwe, Spika akisimama unatakiwa Mbunge ukae chini na Kuhusu Utaratibu ni vizuri ukajiandaa halafu unaenda kwenye kutoa maelezo. Tumeshapoteza dakika tano, kwa hiyo, naomba aliyekuwa anazungumza aendelee. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninapenda niendelee. Kama nilivyokuwa nikisema, CCM kamwe haitalinda ufisadi na tutapambana na ufisadi kwa nguvu zetu zote, nami nina hakika sisi wote tutamuunga mkono kama Rais wetu alivyosema kwamba hela za *EPA* zirudi na zitarudi na zisiporudi ni kweli kwamba tutakuwa na haki ya kuuliza kwa nini hazikurudi? Lakini mimi nina imani na Rais wetu na kwamba akishasema yale aliyosema nina hakika yatatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba viti vya Bunge letu vimesimikwa kwa *bolt, otherwise* kwa hali ya namna hii kusimama tu mtu hata hana *point* na wala

hajui ile *order* ni namba ngapi, katika Mabunge mengine watu huinua viti halafu kuanza kutupiana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu, kifungu namba gani?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu namba 64 katika (e) inasema: "Hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia utoaji wa haki, isipokuwa tu kama kumtolea hoja mahususi kuhusu jambo fulani." Sasa msemaji alikuwa anamzungumzia Rais na mwenendo wake kuhusiana na suala la *EPA*. Je, hajavunja kanuni hiyo? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize. Nadhani tunayo kazi kubwa ya kuweza kusoma kanuni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, swali la kumzungumzia Rais, anasema Rais ameahidi kwamba anameunda Tume ambayo ina miezi sita na alichosema msemaji, mimi nimesikia kwamba atakapotoa Rais kama hatujaridhika ndio tutauliza, sasa hapa hajamsema Rais. Naomba tuendelee Mheshimiwa Malecela. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba muda nitaongezwa.

**NAIBU SPIKA:** Unaongezwa.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huyo ni Makamu wa Mwenyekiti wa Chama cha *CHADEMA*, sishangai! Naendelea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa kwenda kwenye suala la Serikali za Mitaa.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kuhusu utaratibu. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, naona sasa tunaanza kutumia Bunge vibaya, tunaanza kutumia Bunge vibaya kwa sababu hakuna alichokisema Mzee Malecela toka wakati ule.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kipo hapa.

**NAIBU SPIKA:** Wewe siyo Makamu Mwenyekiti?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, maana unamlinda sana, usimlinde zaidi ya mahitaji. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya tunaendelea. Mzee Malecela unaendelea, kwa sababu sasa tunafanya utani ndani ya Bunge hili. Naomba tuendelee. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kama nilivyokuwa nasema. Sasa nataka nije kwenye suala la Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakumbuka kwamba tangu mwaka 1974 tulishughulika sana kuunda vijiji na haja yetu ilikuwa ni kuwaleta wananchi wetu pamoja ili tuweze kuwapa maendeleo. Sasa mimi kwanza pendekezo langu la kwanza ningependa nimwombe Waziri Mkuu kwamba aunde Tume ya Watendaji, sio ya Wabunge, hapana. Tume ya Watendaji, waende wakaangalie, hivi vile vijiji tulivyoviunda tukaambiwa viwe na Serikali na Serikali za vijiji zipo? Lakini je, zinaendesha mambo kama inavyotakiwa? Nia ya Marehemu Baba wa Taifa ilikuwa ni kupeleka madaraka kwanza Mikoani, Wilayani na baadaye vijijini. Je, tangu wakati huo ni madaraka gani tumepeleka huko vijijini na hayo madaraka yanatumiwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mimi niseme Mheshimiwa Waziri Mkuu ni hakika kabisa kwamba, sasa hivi vijiji vyetu vimekosa watu wa fani ya fedha. Kwa hiyo, hakuna mtu anayeshughulika na ukusanyaji wa mapato ya kijiji, matumizi yake na kuwaambia wanavijiji kama inavyotakiwa na sheria fedha zilivyotumika. Sasa mimi ningeomba jambo hilo liangaliwe sana. Tuliwaahidi wananchi wetu kuwapelekea vijijini vitu vikubwa vitatu, navyo ni maji, elimu na afya. Sasa je, tumefikia hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nianze kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wanavijiji wamejenga Shule za Msingi katika kila kijiji Tanzania na kwa kweli jambo hilo ni la kujivunia sana na hata tunapotaja takwimu za watoto waliokwenda Darasa la Kwanza, waliomaliza Kidato cha Nne ni kutokana na hiyo kwamba baadhi yao walianza kusoma chini ya mti, lakini kwenye vijiji ambavyo sasa vina majengo ya shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wakati umefika, Serikali iangalie namna ya kuboresha Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari. Wananchi wamejitolea kujenga shule, wamejenga nyumba za walimu, sasa linapokuja tatizo kwamba hakuna madawati, walimu hawatoshi, mimi nafikiri hilo linakuwa ni la kwetu kwa maana ya Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende upande wa afya. Ni kweli kwamba tamko lililotokea hivi karibuni kutoka Serikalini ni kwamba tunataka tuwe na zahanati kila kijiji, mimi nina hakika jambo hilo litawezekana kwa sababu tuliposema tuwe na Shule ya Sekondari kila Kata sasa hivi ni Kata chache ambazo hazina Shule za Sekondari, lakini ningeomba safari hii maadam tumepanga hivyo, basi Wizara inayohusika iwe na vitu vifuatavyo.

Kwanza, wananchi watakapoanza kujenga vile vitu ambavyo viko juu ya uwezo wao vitu kama mabati, mbao, hivi tuweze kuwasaidia na pili, tuhakikishe kwamba watumishi watakaokwenda kwenye zahanati hizo waanze kutayarishwa sasa kwa sababu tuna vijiji zaidi ya 10,000, kwa hiyo, kupata watumishi kwa vijiji vyote hivyo itakuwa ni vigumu kama hatukujitayarisha mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba miundombinu kwa upande wa vijijini. Ni kweli sasa hivi mambo haya ya simu za mkononi yanaenea vizuri sana, lakini naomba hii miundombinu ya simu za mkononi angalau ziende katika kila kijiji kama itawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye suala la barabara. Nataka kwenda haraka kwa sababu muda wangu mwingi umechukuliwa na usumbufu wa Mheshimiwa Wangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika kama tukiunganisha vijiji vyetu na barabara ya kudumu hata suala la usafiri litakuwa jepesi. Leo Dar es Salaam wamesema kwamba wao hawataki hivi vi-*hiace* wanasema vinaleta matatizo kwenye mji. Sisi vijijini tutavihitaji kwa usafiri kutoka kijiji hadi kijiji lakini kwa sasa hawawezi kuja vijiji kwa sababu barabara hazipitiki vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ningekuja kwenye upande wa kilimo. Mara nyingi sana tunasema wakulima wetu kilimo chao bado ni kilimo duni, sasa kitaachaje kuwa duni ikiwa leo Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Rukwa kila siku kilio chao ni mbolea? Kwanza mbolea haifiki kwa muda na haitoshi. Hapa nataka nisisitize hasa lile kwamba mbolea haitoshi, halafu tunamwambia mkulima ana kilimo duni, sasa hapa sijui ni vipi!

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo nije kwenye suala la mifugo. Mheshimiwa Waziri Mkuu kama kuna watu ambao kwa kweli wamesahaulika katika bajeti zetu mara kwa mara ni upande wa mifugo. Ningependa nisisitize kwamba wakati umefika wafugaji waangaliwe. Wengi tunasema wenzetu Botswana wana mifugo mizuri na wanapata bei nzuri, ndiyo. Lakini ukienda utakuta miundombinu yote, maji na kadhalika wanatengenezewa na Serikali. Sasa sisi bahati mbaya katika Tanzania mifugo wanastawi katika sehemu zilizo na ukame Dodoma, Singida, Arusha, Shinyanga na kadhalika. Sasa kote humu mimi nilitazamia kama kweli tunataka kuwahudumia wafugaji, basi suala la maji lingekuwa ni suala la msingi sana kwa binadamu na mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa madawa, kweli Serikali kama inaweza kutoa ruzuku kwa mbolea, basi kwa nini isitoe ruzuku kwa madawa ya mifugo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo ningependa tu kusema, ninamshukuru sana Waziri Mkuu kwa hotuba yake, tunamtakia kila jema na awe na hakika kwamba tutakuwa naye na tutamsaidia kuweza kufaulu na hasa katika kuleta maendeleo ya wananchi vijijini mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa pili katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, lakini niseme kwamba Watanzania wanafahamu baada ya miaka mitano watakipima Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ambayo ndiyo iliyoweka Serikali hii katika kipindi hiki cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukipima Chama cha Mapinduzi katika miaka hii mitano ziko hoja za msingi ambazo zitahesabiwa na katika kuzihesabu hoja hizo ndipo Chama hiki kitakapoona kama kinafaa kuendelea au hakifai, lakini ninakwambia, kwa hotuba na mwenendo wa utekelezaji wa ahadi za uchaguzi za Chama cha Mapinduzi tunakwenda mbele na ninasema nina uhakika kabisa baada ya miaka mitano tunayo hesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sikatai yako mambo mengine ya kimsingi yanayojitokeza na kama Chama cha Mapinduzi tunatakiwa kuyatazama, lakini hasa ni ahadi zetu kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia nimshukuru sana Waziri Mkuu kwa kutambua umuhimu wa Madiwani. Tumekuwa tukisema siku nyingi na leo kwa kweli hata mimi ninapata faraja kubwa kuona kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu imeamua sasa kuona umuhimu wa Madiwani na kuwasimamia. Naomba Sheria inayounda Baraza la Madiwani, sheria inayosimamia uwepo wa Madiwani iletwe haraka hapa Bungeni tuirekebishe na iweze kukidhi haja na matakwa ya kuwasaidia Madiwani katika utendaji wao wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba tunazungumza suala la umaskini katika nchi yetu ya Tanzania na katika mpango mzima wa MKUKUTA tumekubaliana kwamba ni lazima tutazame umaskini wa kipato kwa wananchi wa Tanzania. Tukisema umaskini ili Watanzania hawa wajumuike kwenye umaskini wao ni lazima tuanze na umaskini wa kaya moja moja katika maeneo tunayotoka. Kaya zile sasa zikikutana kwa pamoja ndio zinajenga hoja za umaskini huu tunaouzungumza katika nchi nzima ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Peramiho, ninawakilisha wananchi wa Jimbo la Peramiho. Wananchi wa Jimbo la Peramiho wameniambia ili waweze kuondokana na umaskini huo wao ni miongoni mwa asilimia 80 ambazo zinahesabiwa katika Pato la Taifa kutokana na sekta ya kilimo. Sasa katika sekta hii ya kilimo ili wananchi wale wa Jimbo la Peramiho waweze kufanya kazi zao vizuri na kuondokana na adha ya umaskini na hasa umaskini huu wa kipato kutoka katika kaya kuja katika vitongoji, kuja katika kijiji, hatimaye katika Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa

zima kwa ujumla ninadhani nikubaliane na mambo haya ya kimsingi ambayo yataweza kuwasaidia wananchi wote wa Tanzania, lakini hasa wapiga kura wangu wa Jimbo la Peramiho, tukitizame kilimo katika jicho la mzamo mwingine kabisa wa kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutizama kilimo katika Jimbo la Peramiho ni lazima kwanza twende moja kwa moja kwenye tatizo sugu na kubwa la pembejeo na pembejeo ninayoizungumzia nitaanza na mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwakomboa wakulima, lazima mbolea iwafikie kwa wakati kwa kiasi kinachotakiwa na ikiwezekana ipatikane kwa mwaka mzima. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ametueleza kwamba kuna mpango wa kuhakikisha kabisa Mbolea ya Mijingu inaweza kufanya kazi nzuri ya kuwafikia wakulima wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubali, lakini kama itafika kwa wakati na kwa idadi inayotakiwa kwa kweli huo ndio utakuwa ni ukombozi. Lakini mbolea peke yake haitoshi, kama hatutaangalia suala zima la kuwaondoa wakulima kutoka katika majembe ya mkono kwenda kwenye matrekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza hotuba zote na tumekubaliana kwamba tutaanzisha Benki ya Wakulima, silipingi hilo, ninaliunga mkono, lakini ninachotaka kusema mara nyingi ukishazungumza habari ya benki hapo umeshawakuta wakulima au wafanyabiashara ambao wako kwenye hatua ya kati na hatua ya kwenda juu. Sasa mimi nashauri suala hili la matrekta kwamba ni kwa nini lisiambatane na uwezeshaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo, yaani *SACCOS* katika maeneo yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yetu *SACCOS* zimefika karibu katika kila Kata tukizitumia *SACCOS* zetu kwenye suala zima la pembejeo, kwenye suala zima la matrekta, kwenye suala zima la kumwinua mkulima, nadhani tunaweza tukafanikiwa kuliko kuwaachia wafanyabiashara binafsi ambao mara nyingi wamekuwa wakiangalia kipaumbele katika maeneo yenye tija na siyo kumsaidia mkulima mdogo. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri hebu tuliangalie hilo vizuri, lakini vilevile ni lazima tujihakikishie kwamba tunapata masoko kwa ajili ya wakulima hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kuongeza fedha kwa ajili ya hifadhi ya chakula ya Taifa, Kitengo cha Hifadhi ya Chakula cha Taifa kama kikiwezeshwa, nasema ni ukombozi mkubwa kwa wakulima na hasa wa Jimbo la Peramiho.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumza wazalishaji wa chakula katika Mkoa wa Ruvuma ninaomba nikwambie kwamba, asilimia 80 wanatoka katika Jimbo langu la Peramiho, sasa kuongeza fedha kwenye kitengo hicho kutawasaidia wakulima kupata bei ambayo ni nzuri katika kununuliwa mazao yao, lakini naomba sana kama tunaongeza fedha kwa kitengo hiki ninaomba pia vituo vya kununulia mazao haya viongezeke. Tunacho kituo kule Kata ya Kilagano ingawa hakuna simu, nimemwomba Mheshimiwa

Waziri wa Mawasiliano apeleke simu kule. Maana kama ndio tunazalisha chakula kwa ajili ya nchi nzima, simu hatuna, kwa hiyo, watuangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninaomba tuongeze kituo kingine kwenye Tarafa ya Muhukuru na kwenye Tarafa ya Madaba. Tarafa ya Madaba tayari tunayo maghala makubwa mawili ambayo yangeweza kusaidia sana. Kama fedha imeongezeka, basi tuongeze vituo kwa ajili ya kununulia mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme kwamba kwa kweli ninaipongeza Serikali, ninaipongeza Serikali kwamba mwaka huu tutafungua daraja muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na kwa maendeleo ya wananchi wa Jimbo la Peramiho. Serikali imetujengea daraja la kutuunganisha na nchi ya Msumbiji katika Kata ya Muhukuru, kwa hiyo, sasa tutakuwa na madaraja mawili, tutakuwa na Daraja la Mtambaswala Mkoa wa Mtwara, lakini tutakuwa na daraja lingine la kutupeleka Msumbuji kupitia Mkoa wa Ruvuma kwenye Jimbo la Peramiho Kata ya Muhukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja hilo litafungua maendeleo kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na hususan Jimbo la Peramiho. Ninawapa taarifa wananchi wangu wasiwe na wasiwasi daraja lile likifunguliwa na tunaiomba Serikali sasa itujengee pale soko la Kimataifa, kwa hiyo, uchumi wetu utakuja juu na sasa tunaweza kujikuta na sisi tunaondokana na umaskini wa kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia niombe sana kwa Waziri wa Miundombinu atusaidie wakati tunapitisha Sheria ya Barabara ya mwaka 2007, barabara inayounganisha Wilaya tatu Wilaya ya Songea Manispaa, Wilaya ya Songea Vijijini na Wilaya ya Namtumbo, barabara hiyo inaitwa barabara ya Songea Matimila kwenda Mkongu.

Barabara hiyo ilihesabiwa kama ni barabara ya Wilaya lakini kwenye sheria ilipelekwa kuwa barabara ya Mkoa lakini bahati mbaya barabara hiyo haikutengewa fedha ninaomba sana Waziri wa Miundombinu atusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme kwamba iko barabara nyingine inayofungua Wilaya ya Njombe na Wilaya ya Songea kupitia Maweso kwenda mpaka katika kijiji kinachoitwa Mikongo, barabara hiyo inahitaji daraja tu itafungua mawasiliano mazuri yenye tija kwa wafanyabishara na itaongeza mapato kwa wananchi hao.

Lakini niendelee kusema kwamba *agenda* ya umeme bado ni *agenda* muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho, ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, alikuja akakutana na wananchi wa Jimbo la Peramiho na kwa kweli ninamshukuru sana na niseme nilimwomba katika Bunge lililopita, alitekeleza ahadi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza ahadi ile, ametoa ahadi ya uhakika, umeme wa gridi kutoka Makambako kuja Songea, sasa fedha zimepatikana, wananchi wa

Kata za Mahanje pale Madaba, Wino, Gumbilo mpaka Songea mjini kutakuwa na umeme. Lakini vilevile amehakikisha kwamba tatizo la umeme katika Kata ya Maposeni, yaani Perahimo ninashukuru sana kwamba sasa tatizo hilo litakuwa pia limetatuliwa. *(Makofi)*

Ninasema hivyo kwa nini? Tumeanzisha kilimo cha miwa, ili kilimo hicho cha miwa kiweze kuwa ukombozi kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho kama hakutakuwa na umeme ni kazi bure, lakini ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri ametusaidia na ninaamini sasa tutakwenda vizuri. Lakini niseme kwamba utekelezaji wa ilani unakwenda vizuri katika Jimbo langu la Peramiho kwa sababu Serikali imetusaidia na sasa hivi Shule yetu ya Sekondari ya Madaba na Maposeni tayari ina Kidato cha Tano kwenda Kidato cha Sita. Hiyo ni juhudi kubwa na ni hatua ya kupongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimshukuru sana Baba Askofu wa Kanisa Kuu Katoliki - Jimbo la Songea na yeye ameazimia kabisa kuanzisha Chuo Kikuu pale Peramiho kwa ajili ya fani ya Udaktari. Tulifanya naye mazungumzo, amekubali na ameanza kazi hiyo. Ninasema CCM tutapimwa kwa matendo yetu mwaka 2010 na mimi ninasema kwamba ninajivunia hayo yote ninayoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Waziri wa TAMISEMI kwamba barabara ya Ndongosi kwenda kule Nambendo nayo imepatiwa fedha. Kwa hiyo, kwa kweli hayo ni maendeleo makubwa sana. Lakini ninajua bado tuna tatizo la zahanati, bado tuna tatizo la watumishi katika zahanati zetu, tuna tatizo la walimu na tuna matatizo mengine madogo madogo kama matatizo ya maji na kadhalika. Ninaamini kabisa kwa kipindi hiki kilichobakia haya yote yanaweza yakatekelezwa na basi Jimbo hili la Peramiho likaonekana limepiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nachukua nafasi hii kwa kweli niseme kwamba yale yaliyobakia Serikali iyazingatie na hasa ugawaji wa vijiji, ugawaji wa Kata, Wilaya mahali panapowezekana na hata Mikoa kama itaonekana yanafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nichukue nafasi hii niishukuru sana hotuba ya Waziri Mkuu na nimwombe tu kwamba haya ambayo nimeyazungumza kwa niaba ya wananchi wa Peramiho, basi yakitiliwa mkazo na yakizingatiwa nina uhakika kabisa wananchi wa Jimbo la Peramiho watakuwa na imani na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguz,i agenda ambayo kwa kweli ni ya msingi zaidi kuliko kitu kingine chochote katika kuelekea katika maamuzi mengine makubwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Peramiho hawakuwezi! *(Kicheko)*

Sasa nitamwita Mheshimiwa Diana M. Chilolo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuwa kitinda mimba katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jioni ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii ambayo imeonyesha mwendelezo mzima na mkakati wa kutosha katika kuwaendeleza Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba niseme nataka niwaambie wananchi wangu wa Mkoa wa Singida na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupanda bei lipo na kweli bei zimepanda, lakini bei hazijapanda kwa sababu ya *EPA* wala *Richmond* wala masuala mengine. Bei zimepanda kwa sababu ya mafuta na hili sio suala la Tanzania, ni suala la dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tusiwapotoshe Watanzania, tuwaambie ukweli kwamba mafuta ndiyo yaliyosababisha bei kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo vilevile nataka niwaambie Watanzania kwamba siku za kufanyia kazi ni tatu tu jana, leo na kesho.

Ukianza kuhangaika na jana ya leo hutayaweza. Kama hukufanya jana subiri utafute mkakati mwingine uyafanye, kazi iliyo kubwa ni kuyafanya ya leo na habari ya leo ni bajeti ya Waziri Mkuu ndiyo tunayoijadili. Habari ya kesho ni ya mwenyezi Mungu. Anayejua kesho ni Mungu peke yake, sisi sote hapa hatufahamu. Kwa hiyo, ninaomba sana unapofika leo hakikisha mambo yako yote mazuri yafanye leo, kama ni kuwatumikia wananchi ni leo, kama ni kutafuta maendeleo ni leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo za awali, sasa nataka nichangie habari iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali iliwatua wananchi mzigo mwaka 2002 kwa kuondoa kodi ya kichwa pamoja na kodi za mifugo na baada ya kutoa hizo kodi, Serikali ilitoa ruzuku ya fidia katika Halmashauri zetu. Lakini toka tulivyopewa ruzuku za ziada 2002 makisio bado ni yale yale! Naomba Serikali iende na wakati kwani maisha yanabadilika. Kodi za Serikali zilivyopanda hivyo hivyo na mahitaji ya Halmashauri yamepanda ! Naomba sana tuelewe kwamba makisio ya mwaka 2002 yameshapitwa na wakati kwa hiyo, tutoe makisio yanayoendana na uchumi ulivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mfano wa Iramba. Mwaka 2002 Iramba tulikuwa na mifugo 200,000, kwa hiyo, kwa kodi ya Sh. 1,000/= kila mfugo tulikuwa tunapata Shilingi milioni 200 na walipa kodi walikuwa 65,000. Ukipiga mahesabu ya 3,000 tulikuwa tunapata Shilingi milioni 180,000 jumla milioni 380,000 lakini hayo ni

mahesabu ya mwaka 2002. Leo hii yamebadilika, tunaomba tuongezewe ruzuku za ziada kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo naomba nizungumzie juu ya suala la Redio ya Tanzania, yaani *TBC.* Ni kweli Mheshimiwa Rais ana nia nzuri na Watanzania huwa anatoa hotuba kila mwisho wa mwezi ili Watanzania wamsikilize. Kwa taarifa ni kwamba hotuba hizo ni hadithi za Alinacha Singida, hatusikii! Ninaomba kupitia bajeti hii Mheshimiwa Waziri Mkuu atutazame kwa jicho la huruma wananchi wa Singida, tuna hamu ya kusikia Redio ya Serikali *TBC*. Tunaomba na sisi tufikiriwe tupate hiyo redio.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo redio tu, hata televisheni ya Taifa Singida haifiki. Hivi kama wafanyabiashara binafsi wanafanya hivi, kwa nini Serikali tushindwe? Nina hakika kabisa haya yapo chini ya uwezo wa Serikali, bado tu Serikali ilikuwa inatupigia mahesabu, lakini kupitia bajeti hii wananchi wa Singida tuna matumaini makubwa na Waziri Mkuu wetu tutapata televisheni ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba niongelee suala la uwanja wa ndege wa Singida. Naipongeza sana Serikali. Uwanja wa ndege wa Singida kupitia uongozi wa Mkuu wetu wa Mkoa Ndugu Kone na Mtendaji Mkuu Ndugu Katanga, nataka nikwambie kwamba hawa ni wachapakazi, wanaipenda Singida, kuna Watendaji wengi wanapokwenda kwenye Mikoa ya wenzao huwa wanapiga blaa blaa tu wanakumbuka walikotoka, lakini hawa wako *committed* na Singida kuiletea maendeleo. Uwanja wetu umekamilika, sasa kupitia Bunge hili, nawaomba wawekezaji wenye ndege zao waje watue Singida.

Sasa hivi uwanja wetu una uwezo wa kumudu ndege yenye watu 20 na kuendelea, tutashukuru sana tukipata ndege za abiria Singida. Tutapata wawekezaji na huduma nyingine za kimaendeleo zitapatikana kwa sababu wawekezaji walio wengi wanapenda usafiri wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kiwanja hiki kuwa tayari, lakini tungefurahi zaidi kama tungewekewa lami. Sasa hivi kina uwezo wa kutua ndege na kuruka, lakini kama kitawekewa lami kitakuwa na uwezo wa kudumu zaidi kutua ndege za abiria na ndege nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hilo, naomba niongee juu ya kodi za wafanyakazi. Ni kweli wafanyakazi hulipa kodi kupitia mishahara yao, lakini kodi hizi mimi napata wasiwasi, naona kama ni kubwa sana. Nikimchukua Mkuu wa Idara aliyepo Halmashauri anayepata Sh. 900,000/= kodi anayokatwa ni Sh. 300,000/=. Kwa hiyo, *take home* yake ni 600,000/=. Hii kodi ndugu zangu ni kubwa sana, hebu tuwatazame wafanyakazi wetu tuwashushie kodi kidogo. Nafahamu wazi kwamba kodi lazima walipe na nchi huwezi kuiendesha bila kodi hilo nalitambua wazi lakini tuwapunguzie kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu vikao vya Halmashauri. Halmashauri ina vikao vingi, ndani ya hivyo vikao pia kuna kikao cha Kamati ya Mipango na Fedha ambacho Wajumbe wake wapo pia Waheshimiwa Wabunge. Lakini ziko Halmashauri ambazo zinawabagua Wabunge wa Viti Maalum. Nataka niambiwe, haki ya Mbunge wa Viti Maalum iko wapi? Uwakilishi wa Wanawake uko wapi? Ninaomba niambiwe kifungu kinachowabagua Wabunge mbona ndani ya Bunge hili Wabunge wote ni kitu kimoja? Kama ni Kamati tunakwenda sambamba, kama ni haki zozote za msingi tunakwenda sambamba, ni vipi ndani ya Halmashauri Wabunge wa Viti Maalumu tubaguliwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba wakati wa majumuisho haya Mheshimiwa Waziri Mkuu anipe jibu, nami nitashukuru sana ili mchango wangu uweze kutumika ndani ya Halmashauri. Siwezi kuingia kwenye kikao kile ni kama mkaribishwa, sina haki pale, sina kura, sina mchango wenye nguvu Nataka haki yangu ya msingi niipate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hilo, sasa naomba niongelee juu ya Benki ya Wanawake. Mbona Serikali ilishaonyesha kukubali Benki ya Wanawake? Kuna uchawi gani tena hapa unapita hii benki inasuasua mbona hatuoni? *Seriousness* yake iko wapi? Wanawake tunahitaji maendeleo, tunahitaji kujiendesha. Tunaiomba Serikali iingilie kati, kama ni fedha tumeshachangia na mimi mwenyewe nimeshachangia, bado kuna utata gani? Wanawake wanatuuliza, hii benki mnayosema iko wapi? Ninaamini Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati atakapokuwa anajumlisha hoja yake atawaeleza Wanawake benki hii imefikia hatua gani ili waweze kujenga imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu suala la kusomesha watumishi. Watumishi tunao wana nia ya kusoma, waliitikia wito wa Mheshimiwa Rais kuhusu watumishi kujiendeleza, lakini mbona wanapigwa danadana huko kwenye Halmashauri zetu? Huko Serikalini anapoamua kwenda kusoma anaambiwa hela ya kumsomesha haipo, kwa nini tuwakatishe tamaa watumishi? Ninaomba sana Halmashauri zetu, Serikali Kuu iwe tayari kuwasomesha watumishi ambao wana nia ya kujiendeleza, ndiyo wito wa Mheshimiwa Rais. Tunapowaambia hakuna pesa tunawakatisha tamaa, ukitaka maendeleo ni leo unapomwambia kesho! Ya kesho unayajua!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la barabara. Ni kweli Serikali yetu inajitahidi sana kuiletea Tanzania maendeleo, inajenga barabara kiwango cha lami, inatafuta wakandarasi. Nataka niambiwe hapa, kuna tatizo gani Dodoma – Manyoni? Mbona naona vyombo vimekaa tu pembeni havifanyi kazi? Kuna nini tena? Kulikoni? Tunahitaji barabara hiyo ikamilike jamani! Mimi nataka nitoke Singida nije niingie Bungeni hapa saa tatu, nimalize shida za wananchi na Bungeni nije nirudi. Nataka tuambiwe kuna nini? Kama kuna tatizo, basi naomba Serikali itatue ili hao wenzetu wamalize kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hilo, naomba niongelee kuhusu suala la kilimo. Nimeshasema Singida tuna wanaume, wanafanya kazi. Mkuu wa Mkoa

anafanya kazi nzuri, ukimgusa Katanga ndiye mwenyewe, tena Mheshimiwa Waziri ukiona Wizara haina Katibu Mkuu ukimpeleka yule kijana atakufanyia kazi. Wanafanya kazi wale watu! Nasikia kwingine Wakuu wa Mikoa hawashirikishi, lakini Singida sisi tunashirikishwa na kila Wabunge wenzangu wa Singida watanisaidia. Kwa kweli tunashirikishwa kwa kila jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kina wasimamizi wa Mkoa wazuri. Ukienda *Ma-DC* wanafanya kazi, Wakurugenzi wanafanya kazi, taabu ni pale chini.

Nimesikia kwamba tayari mnasomesha Watendaji wa Kata, sasa hawa Watendaji wa Kata tukishawasomesha tuwapeleke kwenye Kata zetu na tukishawapeleka huko watengenezeeni vitendea kazi na kitendea kazi namba moja ni pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtendaji, Afisa Kilimo usipompa pikipiki hujamuwezesha, atazungukiaje vile vijiji vyote bila pikipiki? Hujampa Ofisi, vitendea kazi hana! Ninaomba sana suala la kilimo pamoja na kupiga kelele pembejeo, pamoja na kupigia kelele mambo mbalimbali, vilevile msukumo wa kutosha na Watendaji wawepo. *(Makofi)*

Tutashukuru sana na wale Maafisa Kilimo wakimaliza mafunzo yao wapelekeni, sisi tuna Kata 88 tu, nyingine zinazo Maafisa Kilimo na nyingine hazina. Nina hakika zile zikipatikana sasa hivi Singida tunategemea kuvuna mazao zaidi ya asilimia 100, tuna *excess* hivi ukiboresha na Maafisa Kilimo kwa kila Kata unategemea Singida itakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema huyu alikuwa mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, mimi nafahamu kwamba Bunge letu kuanzia sasa na kuendelea mpaka 2010 litakuwa moto tu. Sasa hiyo siyo dalili nzuri, ndivyo inavyopaswa iwe. Sasa nawaombeni Wabunge someni Kanuni zenu kikamilifu kwa sababu Spika au atakayekalia Kiti atatumia Kanuni na siyo kingine chochote. Kwa hiyo, utakalishwa chini na unaweza kutolewa nje au vyovyote vile kama Kanuni haifuatwi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba kabisa kila mtu ajue Kanuni zake, hiyo ndiyo itakuwa kinga yenu, vinginevyo hapa itakuwa *rough* kabisa! Sasa na wanaojua kulalamika hovyo, msilalamike, Kanuni hizi hapa kila mtu asome. Lakini pia usisimame kama hujajiandaa.

Kwa hiyo, kwa kusema hivyo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 24 Juni, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*